# Kiini cha Demokrasia

## Eamonn Butler

**Kimetafsiriwa na Elias Mutani**

Toleo la kwanza 2021 Uingereza na
Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi (IEA)
2 Lord North Street
Westminster
London sw1p 3lb
kwa pamoja na kampuni ya London Publishing Partnership Ltd
www.londonpublishingpartnership.co.uk

Dhima ya Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi ni kuboresha uelewa wa mifumo mikuu ya jamii huru kwa kufanya uchanganuzi na kueleza kinagaunaga jukumu la masoko katika kuleta ufumbuzi wa matatizo ya kiuchumi na kijamii

Hakimiliki © Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi 2021
Haki ya kimaadili ya mwandishi imezingatiwa

Toleo la kiswahili limetafsiriwa na Elias Mutani

Kimetolewa na Taasisi ya Liberty Sparks, Tanzania 2021
*www.libertysparks.org*

Haki zote zimehifadhiwa. Bila kuathiri masharti ya hakimiliki hapo juu, hairuhusiwi kuchapisha sehemu ya kitabu hiki au kuitoa katika mfumo wa kukitoa tena, au kukihamisha, kwa namna au njia nyingine (kielektroniki, kimaandishi, kwa kunakili, kurekodi au vinginevyo), bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwenye hakimiliki na mchapishaji wa kitabu hiki.

Kumbukumbu ya CIP iliyoorodhesha kitabu hiki inapatikana kutoka Maktaba ya Tanzania.

ISBN : 978-9976-88-578-1

Machapisho mengi ya Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi yametafsiriwa katika lugha mbalimbali zaidi ya Kiswahili au kupigwa chapa tena. Ruhusa ua kutafsiri au kupigisha chapa tena sharti iombwe kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anuani iliyowekwa hapo juu.

# YALIYOMO

Kuhusu mwandishi......8
1. KUIELEWA DEMOKRASIA......9
Kuhusu kitabu hiki......9
Tatizo la 'demokrasia'......10
Ukomo wa demokrasia......11
Mvuto wa demokrasia......13
Matatizo zaidi ya uelewa......15
Hitaji la kuwa wazi na dhahiri......16
2. HISTORIA YA DEMOKRASIA......18
Demokrasia ya Kigiriki......18
Jamhuri ya Kirumi......20
Kipindi cha enzi za kati......21
Kipindi cha mwanzoni mwa enzi za kale......23
Falsafa ya jamhuri ya kikatiba......25
Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko......26
Kutanuka kwa demokrasia…......28
…kupita mipaka yake?......29
Kifo cha demokrasia?......30
3. TAASISI ZA KIDEMOKRASIA......32
Lengo na madaraka ya serikali......33
Jukumu la msingi la demokrasia......35
Demokrasia ya moja kwa moja......36
Demokrasia ya uwakilishi......37
Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko......38
4. MISINGI YA DEMOKRASIA......41

Umuhimu mkubwa wa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ........ 41
Tanzu zenye manufaa za uwakilishi unaopendelea mabadiliko ........ 46
Utendaji kazi wa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko .... 47
5. NCHI ZA DEMOKRASIA YA UWAKILISHI LEO HII ....... 51
Serikali ya kibunge ........ 51
Mifumo ya urais ........ 53
Tawala za kifalme zilizowekwa kikatiba ........ 53
Jukumu la umma ........ 54
Hakikisho la usalama wa mchakato ........ 55
Mifumo ya upigaji wa kura ........ 56
Uwajibikaji kwa umma ........ 58
Mvutano kati ya demokrasia na haki ........ 59
6. MANUFAA YA DEMOKRASIA ........ 60
Kuzuia ulimbikizaji wa madaraka ........ 60
Kupokea mabadiliko ........ 60
Kuhoji maadili yetu ........ 61
Kuinua kiwango cha sera inayoaminika ........ 63
Ukosoaji na kupiga hatua za maendeleo ........ 64
Kulinda haki za mtu binafsi ........ 65
Amani na ustawi ........ 66
Hitimisho ........ 67
7. UKOSOAJI WA DEMOKRASIA ........ 68
Watu wenye haki ya kupiga kura hawapo tayari kwa kazi ..... 68
Inafanya maamuzi yasiyofaa … ........ 71
…na mabaya ........ 72

Inatilia mkazo mipango ya muda mfupi ....................................73
Inategemea nguvu za dola....................................................74
Inachochea uundaji wa serikali kubwa kupita kiasi.................76
Ina gharama zilizojificha.....................................................77
8. DEMOKRASIA IMETIWA CHUMVI? ...................................79
Demokrasia ni mfumo bora kabisa ........................................79
Ni utawala wa watu..............................................................80
Ni serikali itokanayo na ridhaa ............................................80
Kila mmoja ana kauli ...........................................................82
Demokrasia inachochea usawa .............................................83
Demokrasia huleta hisia ya jumuiya ......................................84
Demokrasia hutulinda dhidi ya watawala wabaya...................85
9. JINSI MAAMUZI YA KIDEMOKRASIA YANAVYOFIKIWA............................................................87
Chaguzi za viongozi.............................................................87
Watu wenye haki ya kupiga kura...........................................88
Wagombea ..........................................................................89
Wabunge au wawakilishi ......................................................90
Maofisa wa serikali ..............................................................91
Wategemezi wa siasa ...........................................................92
Hitimisho.............................................................................93
10. SHINIKIZO JUU YA DEMOKRASIA................................94
Kukataliwa kwa siasa za wenye nguvu na ushawishi..............95
Mazingira katika dunia inayobadilika....................................96
Mabadiliko katika mfumo wa kisiasa ....................................97
Mabadiliko miongoni mwa watu wenye sifa ya kupiga kura ..98
Hitimisho............................................................................100

11. MUSTAKABALI WA USHIRIKI ..................................... 101
Aina za ushiriki ..................................... 101
Hoja zinazotetea ushiriki..................................... 103
Hoja zenye mantiki dhidi ya ushiriki ..................................... 104
Msingi wa hoja dhidi ya ushiriki ..................................... 106
Je, ni kweli tunahitaji ‘demokrasia zaidi’? ..................................... 107
Dhana ya demokrasia yenye ukomo ..................................... 109
12. DEMOKRASIA NA MIPAKA ..................................... 110
Makosa ya nchi za Magharibi ..................................... 111
Matatizo ya nchi changa za demokrasia ..................................... 113
Majaribio yaliliyoshindwa ya kulazimisha maadili ya kidemokrasia ..................................... 114
Taasisi za kimataifa..................................... 115
Dunia ya kidemokrasia?..................................... 116
Mfumo kwa ajili ya makundi madogo? ..................................... 117
13. FUNZO KUTOKANA NA UZOEFU ..................................... 119
Je, kweli tunahitaji demokrasia? ..................................... 119
Kipi kinahalalisha demokrasia? ..................................... 120
Ni ipi taswira ya demokrasia endelevu? ..................................... 121
Mbadala wa mifumo ya kidemokrasia ..................................... 123
Demokrasia siyo kila kitu ..................................... 125
14. NUKUU KUHUSIANA NA DEMOKRASIA ..................................... 128
Udhalimu wa walio wengi ..................................... 128
Madaraka hulevya ..................................... 128
Utamaduni wa demokrasia..................................... 129
NYONGEZA YA KUJISOMEA ..................................... 130
Maelezo kwa ufupi..................................... 130

Changamoto na wakosoaji ........................................................ 131
Rejea nyinginezo ........................................................ 134
Istilahi za msingi ........................................................ 138

## Kuhusu mwandishi

Eamonn Butler ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Adam Smith, mojawapo kati ya taasisi andamizi za washauri mabingwa wa sera duniani. Ni msomi mwenye shahada katika fani za uchumi na saikolojia, shahada ya uzamivu katika falsafa na shahada ya uzamivu ya heshima ya DLitt. Katikati ya miaka ya 1970 alifanya kazi mjini Washington katika Baraza la Wawakilishi la Marekani, na alifundisha falsafa katika Chuo cha Hillsdale, Michigan, kabla ya kurejea Uingereza ambapo alisaidia kuasisi Taasisi ya Adam Smith. Akiwa ni mshindi wa zamani wa Medali ya Uhuru inayotolewa na Freedom's Foundation of Valley Forge na Tuzo ya National Free Enterprise ya Uingereza, kwa sasa Eamon ni Katibu wa Mont Pelerin Society.

Eamonn ni mwandishi wa vitabu vingi, ikiwa ni pamoja na dibaji katika vitabu vya wachumi na wanazuoni ambao ni watangulizi wake: Adam Smith, Milton Friedman, F. A. Hayek, Ludwig von Mises na Ayn Rand. Pia amechapisha vitabu vya kisasa juu ya uhuru wa kujiamulia, chaguzi za umma, Magna Carta, Fikra za Wachumi wa Austria na wanazuoni mashuhuri wa uhuru wa kujiamulia, pamoja na *Utajiri wa Mataifa kwa Ufupi* na *Kitabu Kizuri Zaidi Kuhusu Soko.* Kitabu chake cha *Misingi ya Jamii Huru* kilishinda tuzo ya mwaka 2014 ya Fisher. Pia ni mwandishi mwenza wa *Karne Arobaini za Udhibiti wa Ujira na Bei,* na mfululizo wa vitabu juu ya akili na upimaji wa kiwango cha akili. Ni mchangiaji wa mara kwa mara katika uchapishaji, utangazaji na majukwaa ya mtandaoni.

# 1. KUIELEWA DEMOKRASIA

## Kuhusu kitabu hiki

Kitabu hiki ni utangulizi rahisi unaoeleza demokrasia ni nini, na jinsi inavyofanya kazi, uwezo na udhaifu wake, manufaa yake na mipaka yake. Lengo kuu la kitabu hiki ni kumwezesha *mtu yeyote* kuelewa demokrasia, hata pale ambapo kamwe hajapitia uzoefu wake. Hata hivyo, wengi *wanaofikiri* wanaielewa demokrasia watanufaika pia, kwa sababu mara nyingi hata wao hawatilii maanani sifa zake.

Kuielewa demokrasia ni jambo muhimu: ikizingatiwa kwamba theluthi mbili ya watu wote ya duniani, katika zaidi ya nchi mia moja, wanaishi chini ya serikali zinazojinadi kuwa za kidemokrasia. Na kwa kuwa idadi ndogo sana ya hizo serikali ndizo hasa zenye kuzingatia mifano mizuri ya demokrasia au kuheshimu misingi yake mikuu na taasisi zake, uelewa *bayana* wa demokrasia unakuwa muhimu zaidi. Kwa mifano halisi, tunapaswa kuwa macho na jinsi ambavyo ni rahisi kwa demokrasia kupotea au kutumiwa vibaya pale watu wanaposhindwa kuielewa kadri ipasavyo.

Ili kufanikisha malengo hayo, kitabu hiki kinatoa tafsiri ya demokrasia, kinaelezea malengo yake, na kuonesha tofauti baina ya demokrasia ya kweli na aina nyingi zilizopo za demokrasia bandia. Kinatoa kwa ufupi historia ya demokrasia, mabadiliko ya asili ya dhana yenyewe na njia tofauti za kuifikia. Kinatoa muhtasari wa manufaa ya demokrasia pamoja na kuonesha maelezo mengi potofu yanayofanya tushindwe kuona mipaka yake. Mwisho, kitabu hiki kinahoji sababu za watu leo hii kutoridhishwa sana na siasa za kidemokrasia — na kama kuna chochote kinachoweza kufanyika kuhusiana na jambo hilo.

## Tatizo la ‘demokrasia’

Tatizo kubwa kuliko yote kwa mtu yeyote anayejaribu kuelewa demokrasia ni kwamba neno limebadilisha maana yake. Kile tunachoita ‘demokrasia’ leo hii siyo kile ambacho Wagiriki wa kale (wanaosifiwa kwa kuvumbua dhana hii) walikuwa nacho akilini. Kwao ‘demokrasia’ ilimaanisha mfumo wa serikali ambapo wananchi wangekusanyika katika mabaraza ya wazi kutunga sheria, kuamua juu ya sera za msingi (kama vile uamuzi wa kwenda vitani) na kuteua maofisa wa serikali. Kwetu, hata hivyo, ‘demokrasia’ maana yake ni mfumo wa serikali ambapo umma hupiga kura, kila baada ya miaka michache, kuchagua wawakilishi (kama vile marais, wabunge au maseneta) ambao baada ya hapo huamua juu ya sheria, sera na teuzi za utumishi wa umma.

Lakini hata haya matumizi ya kisasa yanaweza kujumuisha maana nyingi tofauti. Neno ‘demokrasia’ linaweza kuelezea mifumo ambapo chaguzi ni huru na hufanyika kwa haki, kupitia kura za siri, zikiwa na wigo mpana wa wagombea kwa mtu kuchagua, na ambapo kuna mipaka ya nguvu za wawakilishi na maofisa wa serikali, na mfumo huru wa mahakama wenye kuhakikisha kwamba maofisa wa serikali wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria na ndani ya mipaka hiyo. Kwa upande mwingine, ‘demokrasia’ mara nyingi hutumika kuelezea mifumo ambayo baadhi ya sifa kama hizo hupatikana kwa kiwango cha chini kulinganisha na hiyo mifano bora ya ukamilifu au pengine hata isiwepo kabisa. Katika nchi nyingi zinazojiita zenyewe kuwa ni ‘nchi za kidemokrasia’, upigaji kura siyo wa siri kiuhalisia, maofisa wa tume za uchaguzi ndani ya serikali siyo waaminifu, wapiga kura na wagombea hupokea vitisho, vyombo vya habari hudhibiti mdahalo wa umma, na wawakilishi hupotoka.

Katika baadhi ya mifano, nchi huonesha viashiria vya demokrasia (kama vile chaguzi za viongozi, mabunge na mahakama za kisheria) lakini unakuta ni chama kimoja pekee ndicho

kinaruhusiwa kuweka wagombea. Watunga sera na majaji hawawezi kamwe kuhoji mamlaka ya mtawala, na maofisa wa serikali wanakaribia kuwa na nguvu isiyo na kikomo juu ya maisha na mienendo ya wananchi. Mfano ni Korea Kaskazini, ambapo idadi ya watu wanaojitokeza katika chaguzi za viongozi inakaribia asilimia 100 na mgao wa kura wanazopata wagombea kutoka Chama cha Kidemokrasia cha Muungano wa Nchi ya Asili unakaribia kufikia idadi ya kura zote zinazopigwa (jambo linalotoa mashaka makubwa).

## Ukomo wa demokrasia

Dhana potofu iliyozoeleka kuhusu demokrasia ni kwamba inawapa walio wengi haki ya kufanya chochote wanachotaka. Hata hivyo, wazo dogo tu linaonesha kwamba jambo hili ni kosa la wazi. Kwa mfano, inawezekanaje mafanikio tu katika uchaguzi yawapatie walio wengi haki ya kutaifisha makazi, biashara na utajiri wa walio wachache? Au kuwatupa jela au kuwatimua nchini, kuwatesha au hata kuwachinja? Wanadamu wana maadili yenye thamani ya juu zaidi kuliko utawala wa walio wengi — kama vile 'utukufu' wa maisha, uhuru na mali za watu. Kigezo kwamba walio wengi huamua kukiuka maadili hayo hakifanyi matendo yao kuwa sahihi kimaadili au kisiasa.

Takribani miaka 2,400 iliyopita, wanazuoni wa Ugiriki ya Kale kama vile Plato na mwanafunzi wake Aristotle walielewa jambo hili. Kusema kweli, walichukulia demokrasia kama aina hatari sana ya serikali, na siyo kwa sababu tu walikuwa matajiri wa tabaka la juu. Demokrasia inaweza kuwa utawala wa kundi la watu wenye fujo ambapo chini ya utawala wake, siyo maisha au mali za watu kinachokuwa salama. 'Mahali pasipo na uhuru wa kusimamia haki', aliandika Aristotle (350 KK) katika kitabu chake kiitwacho *Siasa*, 'watu wanakuwa tawala ya kifalme' na 'kitu pekee wanacholenga ni kupata nguvu na kuwa kama bwana'.

Miaka elfu mbili baadaye, jopo la watu 55 wakiwemo wamiliki wa ardhi, wamiliki wa watuma na watu binafsi wengine maarufu walioandika Katiba ya Marekani mpya walikuwa na shaka sawa na hiyo. Walitengeneza, siyo mtindo wa Kigiriki wa *demokrasia* ambapo kila kitu kiliamuliwa na watu, bali *jamhuri* ya kidemokrasia ambapo watu wangechagua wawakilishi wa kufanya maamuzi kwa niaba yao. Kwa umakini mkubwa walisanifu mchakato wa ufikiaji wa maamuzi ulioweka ukomo wa nguvu za wale waliopo madarakani kwa lengo mahsusi la kuwalinda watu binafsi na makundi ya walio wachache — ingawa ni aibu kwamba hawakufikisha ulinzi huo kwa robo ya watu wote katika nchi waliokuwa watumwa au Watu wa Asili ya Amerika.

Hitaji la taasisi za kidemokrasia kutumikia maadili yetu zaidi kuliko kupanga masharti katika maisha yetu ndiyo sababu inayofanya aina halisi zaidi ya demokrasia (kwa maana ya kisasa), na ambayo inatoa kiini halisi cha dhana ya kidemokrasia, kuwa kitu kinachoitwa *demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko*. Watetezi wa aina hii ya demokrasia wanaamini kwamba lengo kuu la demokrasia siyo kuzuia au kudhibiti watu bali ni kuwakomboa. Kwa hawa *wenye kupendelea mabadiliko* (katika mtazamo wa Ulaya), serikali haijaundwa ili kuwalazimisha watu binafsi kufanya chochote kile ambacho walio wengi wanaamua kuwa ni ‘sahihi’, bali zipo kwa ajili ya kila mmoja kuwa huru kadri inavyowezekana na kupunguza matumizi ya nguvu na uonevu — unaofanywa na watu wengine au serikali yenyewe (Butler 2015a).

Hata hivyo, hii amani na uhuru vinahitaji utawala wa walio wengi kuwa na sharti la ukomo wa nguvu zake. Katika demokrasia ya kweli yenye kupendelea mabadiliko, wanasema wenye kupendelea mabadiliko, hata walio wengi kwa uwiano mkubwa sana — tuseme watu elfu moja kwa mmoja, — hawawezi kufanya chochote kama wapendavyo: daima ni sharti kwa walio wengi kuheshimu na kuunga mkono haki za msingi na uhuru wa watu wote. Haki hizo na uhuru vinachukua kipaumbele cha mtazamo

wa walio wengi kwa kuwa sababu inayofanya serikali iwepo ni kulinda vitu hivyo.

Wenye kupendelea mabadiliko hawakubaliani sana juu ya maana halisi ya haki za binadamu na mahali zinapotoka. Hata hivyo, haki za mtu binafsi zinaonekana kuwa pana zaidi na kulindwa vizuri zaidi katika nchi zenye mwelekeo wa demokrasia inayopendelea mabadiliko kuliko kwingineko. Jambo hili, anatoa hoja mchumi wa siasa wa Kimarekani anayeitwa Jayme Lemke (2016), pengine hutokana na ushindani baina ya mifumo tofauti ya kisiasa, ikiwemo watu kuhamia kwenye mamlaka za kisheria zilizo huru zaidi na zenye kuheshimu tabia na sifa binafsi za wananchi wao.

## Mvuto wa demokrasia

Wale wanaounga mkono demokrasia wanatoa hoja kwamba sheria hazitakiwi kutungwa kwa wazo la ghafla kutoka tabaka la watu wenye uwezo katika jamii (kama vile mfalme au dikteta) au kundi (kama vile familia au ukoo unaotawala). Badala yake, *umma wote* ulipaswa kuamua watu waishi chini ya sheria zipi — au walau, umma ulipaswa kuchagua nani anayetunga sheria. Chaguzi hizi, wanasisitiza, zilipaswa kufanywa kwa msingi wa usawa katika medani ya siasa, ambapo kura ya kila mmoja ina uzito ulio sawa. Kimsingi, wananchi wengi kadri inavyowezekana walipaswa kuruhusiwa kupiga kura. Watu walipaswa kuwa huru kufikiri na kuongea kwa uwazi juu ya masuala umuhimu. Kimsingi, watu wenye haki ya kupiga kura wanapaswa kuwa na taarifa kamili, kuwa mahiri na kuwa na uwezo wa kufikiri kwa mantiki juu ya uongozi wao wenyewe. Na sharti kuwe na taasisi imara, zinazoaminiwa na zinazoaminika ambazo bila upendeleo zinatafsiri maamuzi ya umma katika sera.

Mifano hii mizuri ya kidemokrasia inaonekana kuwa na mvuto wenye nguvu. Licha ya yote hayo, nani asingependa kuwa na kauli juu ya namna anavyotawaliwa, kuliko kuwa na mtu mwingine yeyote tu anayeamua matukio kwa niaba yake? Nani asingependa kuwa salama dhidi ya nguvu za kikatili za madikteta? Nani asingependa kufikiri kwamba maoni yake yanathaminiwa na kuzingatiwa bila upendeleo?

Kusema kweli, mifano hii mizuri ya kidemokrasia inavutia sana kiasi kwamba, kwa bahati mbaya, karibia kila serikali inajinadi kuziishi sifa hizo, iwe ni kweli zinafanya hivyo au hapana. Nchi kuitwa ya 'kidemokrasia' ni alama ya kuheshimika na kibali mbele ya 'macho' ya dunia. Kama mwandishi wa riwaya na mkosoaji wa karne ya ishirini kutoka Uingereza anayeitwa George Orwell (1946) alivyoonesha: 'Ni hisia iliyoenea karibia duniani kote kwamba pale tunapoiita nchi kuwa ya kidemokrasia huwa tunaisifia; matokeo yake, watetezi wa kila aina ya utawala hudai utawala wao ni demokrasia…'.

Matokeo ni kwamba neno 'demokrasia' hatimaye linapoteza maana yake. Vyama vya Walio Wengi huchukulia ushindi katika chaguzi za 'kidemokrasia' za viongozi kama kitu kinachowapa mamlaka kamili ya kuwatesa wengine, kufuja fedha za umma kwa manufaa yao wenyewe, na kugawa ajira za serikali na mikataba kwa washirika wao. Madikteta huwatupa jela wapinzani wao wa kisiasa na kuitisha chaguzi bandia za viongozi ambazo huwapatia asilimia 100 ya kura na kisha wanadai kuwa 'wamechaguliwa kidemokrasia'. Katika maeneo mengi, kitendo cha kuwakosoa tu viongozi wa serikali na sera zao kinaweza kufanya ukamatwe kwa kosa la uhaini. Matumizi mabaya kama haya ya madaraka ni chukizo kwa dhana yenyewe ya demokrasia.

## Matatizo zaidi ya uelewa

Licha ya upotoshaji wa makusudi kama huo na kejeli katika maana ya neno, pia kuna uelewa mbaya na halisi ulioenea, wa nini hasa ni maana ya demokrasia na jinsi gani inafanya kazi. Watu wengi wa Asia, kwa mfano, wanaikataa demokrasia wakiiona kama kitu kinachozalisha mgogoro, kinachokawiza ufikiaji wa maamuzi na kilichojikita katika mambo ya muda mfupi. Hawatilii maanani uwezo, umashuhuri na unyumbulikaji wake. Kinyume chake, raia wengi wa nchi za Magharibi wanaamini kwamba demokrasia ni ufunguo pekee wa ustawi, uhuru, usawa na amani. Mtazamo wao wa demokrasia ni ule wa kutia matumaini sana kiasi kwamba wanashindwa kung'amua matatizo na mipaka yake.

Kusema kweli, kusifiwa mno kwa demokrasia pengine ndio kitisho kikubwa kuliko vyote dhidi yake. Mara nyingi, wenye na shauku na demokrasia wanadai kwamba ndio mfumo bora kabisa wa serikali kwa sababu unategemea kibali cha walio wengi. Hata hivyo, endapo ni kweli kwamba kura ya walio wengi ndiyo njia bora kabisa ya kufanya maamuzi, kwanini hatuitumii katika kila uamuzi? Hoja hii huwashawishi wengi kwamba tunapaswa kuitumia; lakini matokeo ya kusikitisha ni kwamba maamuzi ya kila siku ambayo hapo zamani yaliachwa kufanywa na watu binafsi — mfano jinsi wanavyoishi, wanakula au kunywa nini, au hata kitu wanachoweza kusema mbele ya umma — yanazidi kutawaliwa na utaratibu ambao maoni ya walio wengi yataruhusu.

Kulingana na wenye kupendelea mabadiliko, jambo hili huitwisha mzigo demokrasia kufanya kazi ambayo haikusanifiwa kwa ajili yake. Wanasema demokrasia, kamwe haikukusudiwa kufanya chochote zaidi ya kufikia maamuzi machache ya pamoja ambayo watu wasingeweza kufanya kupitia mtu mmoja mmoja — kama vile ulinzi wa pamoja. Iliendelezwa ili kuhakikisha usalama wa haki za watu binafsi, siyo kufifisha haki kwa wazo la ghafla la walio wengi. Ilikusudiwa kupanua uhuru wa watu, siyo

kuuminya. Ilitengenezwa kupunguza uonevu dhidi ya watu, siyo kuupa uonevu huo uhalali wa kisheria.

## Hitaji la kuwa wazi na dhahiri

Katika kuabudu manufaa ya demokrasia ni rahisi kushindwa kuona mipaka yake. Ufikiaji wa maamuzi kwa kura ya walio wengi siyo jibu la kila tatizo. Ni mbinu tu inayoweza kufanya kazi ya kufikia maamuzi (yanayopaswa kuwa machache) ambayo yanaweza tu kufanywa kwa pamoja. Wenye kupendelea mabadiliko wanatoa hoja kwamba demokrasia siyo njia ya kupindua au kujitwalia nafasi ya kufanya maamuzi (mengi sana) ambayo watu binafsi wanaweza kuyafanya vizuri kabisa wao wenyewe, na kwamba mahali pekee inapoweza kufanya kazi ni pale ambapo uhuru huo unaheshimiwa.

Pia kuna pengo kubwa baina ya mifano bora ya demokrasia na uhalisia wenye dosari wa mchakato wa kisiasa unaoiwezesha demokrasia kufanya kazi. Mahali ambapo ufikiaji wa maamuzi kwa kura ya walio wengi umepanuka kupita kiasi, hapo siasa — ambayo sasa huwa sehemu isiyoepukika ya ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja — hujipenyeza katika kila nyanja kubwa na ndogo za maisha, ikichafua dhana yenyewe ya demokrasia. Hatari inayofuatia hapo ni kwamba watu wanajenga uhasama dhidi ya 'demokrasia', wakidhani ipo kwa dhumuni pekee la kujipatia nguvu na maslahi ya kisiasa — na kwamba tunatelekeza mfumo huohuo ambao ulipaswa kutulinda dhidi ya maslahi hayo.

Hii ndiyo sababu ni muhimu sana kuwa bayana katika kueleza demokrasia ni nini — na siyo nini. Tunahitaji kuwa na uwezo wa kubainisha ni upi kati ya mifumo mingi ya kisiasa inayojidai kuwa 'ya kidemokrasia' ambao ndio kweli unazingatia mifano mizuri na misingi ya demokrasia. Kuelewa lengo kuu la demokrasia na kutambua mipaka yake. Kujifunza ni masuala gani

demokrasia inafaa kuamua na yapi haifai kufanya hivyo. Kugundua ni kitu gani huchochea serikali bora ya kidemokrasia na kitu gani huipotosha. Kukubali kwamba kuna maadili ya juu zaidi ambayo hatuna budi kuyalinda hata katika mazingira yenye uwiano mkubwa sana wa maoni ya walio wengi. Kutambua kwamba ni sharti kwa demokrasia kubaki ndani ya mipaka yake. Kufahamu kwamba demokrasia inajengwa juu ya misingi mikuu ya kimaadili, kitamaduni na kitaasisi inayohitaji kutunzwa na ambayo siyo rahisi kuiunda upya. Na kubakia na tahadhari kwamba demokrasia inahitaji jitihada za kutosha ili kueleweka, kutenda kazi yake na kuhifadhiwa.

# 2. HISTORIA YA DEMOKRASIA

Neno ‘demokrasia’ liliingia katika lugha ya Kiingereza kutoka Ufaransa ya karne ya kumi na sita, lakini chimbuko lake ni la kale zaidi. Takribani miaka 4,000 hadi 5,000 iliyopita, Wagiriki wa enzi ya shaba waliyaita makundi ya watu wote katika nchi kama *damos*, ingawa neno hili nalo laweza kuwa linatokana na *dumu*, neno lenye dhana kama hiyo ambayo inapatikana hata katika ustaarabu wa Wasumeri wa kale, mahali ambapo kwa sasa ni kusini mwa Iraq. Katika Kigiriki cha Kale neno hili likawa *demos*, likiwa na maana ya ‘watu’ au ‘halaiki’ ya wakazi maskini sana. Pamoja na *kratos*, ikiwa na maana ya ‘nguvu’ au ‘udhibiti’, linatoa chimbuko la neno linalotumika sasa.

## Demokrasia ya Kigiriki

Wasumeri walioishi Mesopotamia — ‘uwanda mithili ya mwezi mchanga na wenye rutuba’ uliopatikana baina ya mito Tigri na Eufrate — takribani miaka 5,000 iliyopita wanasifiwa kwa kuasisi ustaarabu wa kwanza uliopata kujulikana duniani. Baadhi ya wasomi wanashikilia kauli kwamba huenda hata walikuwa na aina fulani ya awali ya demokrasia, na kwamba wafalme wa majiji yao yaliyokuwa himaya huru, kama Gilgamesh wa Uruk, hawakuhodhi madaraka yote bali walitenda kazi ndani ya mabaraza ya wazee. Hata hivyo, ushahidi wa jambo hili ni mdogo sana.

Hata mashariki zaidi, huenda kulikuwa na aina fulani za demokrasia zilizochomoza miongoni mwa ‘jamhuri’ huru za bara dogo la Hindi takribani miaka 2,600 iliyopita. Tunaona kwa mara nyingine tena, watawala wake wa kifalme, walioitwa Raja, walitawala ndani ya mabaraza ya ushauri, ambayo yalikuwa wazi

kwa wote waliokuwa ‘watu huru’, yaliyokuwa na mamlaka mapana ya kisiasa na yaliyokutana mara kwa mara. Hata hivyo, ni maelezo machache yaliyopo, na wasomi kwa namna hiyohiyo wamegawanyika endapo taratibu hizo zilikuwa kweli mifano ya utawala wa watu.

Hata hivyo, upo ushahidi mwingi kwamba demokrasia ilifikia kilele chake huko Ugiriki (hasa Athens) takribani miaka 2,500 iliyopita. Ukweli ni kwamba, kulikuwa na nchi ndogo-ndogo za kidemokrasia takribani 1,000 katika Ugiriki ya Kale: kila moja ilikuwa jiji lilikokuwa himaya huru (kwa jina la *polis* lililozaa neno la Kiingereza ‘politics’ ambalo tafsiri yake ni ‘siasa’). Hata hivyo, katika jumuiya ndogo-ndogo kama hizo, nguvu ingeweza kujilimbikiza kirahisi katika mikono ya wachache waliotoka kwenye tabaka la watu wenye uwezo katika jamii. Dhana ya demokrasia ilikuwa ni kuzuia kutokea kwa jambo hili na kupelekea sera kuamuliwa na kundi pana zaidi. Demokrasia ilikuwa bado ikihusisha tu kundi la walio wachache miongoni mwa watu wote katika nchi, kwa kuwa hata katika Athens ya ‘kidemokrasia’, watumwa, watoto, wanawake na wageni kutoka nchi za nje - wote hawa hawakushirikishwa. Licha ya hivyo, wanaume wa Athens takribani 6,000 hadi 10,000 waliokusanyika katika mikutano ya wazi, walifanya mdahalo na kuamua juu ya masuala kama vile sheria, vita na uteuzi wa maofisa wa serikali.

Mfano bora wa kidemokrasia ulitamkwa kwa ufasaha na mtawala mashuhuri na jenerali wa Athens aliyeitwa Pericles (c. 404 KK): himaya huru ya pamoja, usawa katika medani ya siasa, uhuru na ustahimilivu, na uzingativu wa sheria, kwa wengine na kwa mtu mwenyewe. Hata hivyo, nguvu na kigeugeu cha mabaraza yaliyokuwa wazi kwa watu wote viliwaogofya wanazuoni wa kale kama vile Plato na Aristotle. Waliamini kwamba halaiki ya wananchi maskini sana ilikuwa na taarifa nusu-nusu na ilikosa maono ya kujua kwa ubora, hata maslahi yao wenyewe, na ingeweza kuyumbishwa kirahisi na viongozi wenye kushawishi watu kupitia hisia badala ya fikra zao. Walihofia kwamba

demokrasia inayofuata utashi wa watu wote ingeweza kugeuka na kuwa aina mpya ya udhalimu — utawala wa kundi la watu wenye fujo. Na waliogopa kwamba kundi la watu wenye fujo lingeishia tu kuwapora watu wenye maisha mazuri zaidi (kama wao wenyewe), kwa madai kwamba kura ya walio wengi ingepelekea kufanya uporaji huo kuwa wa haki na wenye uhalali kisheria.

Suluhisho la Plato lilikuwa ni kuacha shughuli za utawala mikononi mwa 'wafalme na mwanafalsafa' wenye hekima, lakini Aristotle alitambua kwamba kifani bora kama hicho hakikuwepo duniani. Alifikiri kwamba demokrasia (ambayo katika Ugiriki ya Kale ilikuwa ni utawala wenye nguvu wa watu maskini) ingeweza kuwaokoa wananchi dhidi *utawala wa serikali ya wachache* (utawala wenye nguvu wa matajiri) lakini demokrasia nayo kwa upande wake ilitakiwa kudhibitiwa na wananchi wenye utajiri wa kati — ambao nao pia walikuwa wachache sana.

## Jamhuri ya Kirumi

Wanazuoni wa Roma ya kale nao walikuwa na wasiwasi kama huo; lakini aina yao ya demokrasia walau ilidhibitiwa kupitia utaratibu wa kitaasisi. Ingawa baadaye mfumo huu ulikuja kupinduliwa na nafasi yake kuchukuliwa na udikteta wa Kaizari, Roma ilikuwa *jamhuri* (kutokana na neno la Kilatini *res publica* au 'jambo la watu').

Jamhuri ni mfumo wa serikali unaojiendesha kulingana na mkusanyo wa kanuni unaobainisha jinsi inavyopasa kutenda kazi na mipaka ya kile inachoweza kuamua. Kanuni hizi — nyakati fulani zikiwa zimeandikwa dhahiri katika *katiba* — zipo ili kudhibiti nguvu ya watu waliopo katika nafasi za mamlaka na kulinda makundi ya walio wachache na watu binafsi dhidi ya maamuzi holela. Jamhuri inaweza kuwa 'ya kidemokrasia' (kwa umma wote kuteua wabunge au wajumbe wa kuwawakilisha) au

inaweza kuwa ‘ya utawala wa wachache’ (ikiendeshwa na tabaka la watu wenye uwezo katika jamii wanaojichagua wenyewe); lakini mifumo yote miwili ikabaki kuwa na ukomo wa madaraka yake kupitia kanuni zilizokubaliwa.

Jamhuri ya Kirumi ilikuwa na baadhi ya sifa za kidemokrasia na baadhi ya sifa za utawala wa wachache. Haikuwahi kamwe kuwa ‘jambo la watu’. *Maliwali* wake wawili walikuwa na nguvu ya kiutawala iliyokaribia kuwa ya kifalme na walichaguliwa, siyo na watu, bali na kamati ya watu wa tabaka la juu. Seneti pia ilikuwa ni kusanyiko la watu wa tabaka la juu, wasiochaguliwa na umma. Hata hivyo, waliokuwa na haki ya kuitwa wapiga kura — *raia kamili* wa kiume (wananchi) — waliweza kuchagua (na muhimu sana, kuwaondoa) baadhi ya maofisa wengine muhimu wa serikali kama vile *maofisa wateule*, waliokuwa na kura ya turufu juu ya sheria zilizopitishwa, na *mahakimu* waliotekeleza sheria hizo.

Uhusika wa watu wote uliwekewa hata ukomo zaidi katika nyakati za dharura, pale ambapo Seneti na maliwali walipoweza kuteua *madikteta* — watu binafsi waliopewa mamlaka yote ya utawala lakini kwa kipindi fulani tu cha muda. Haikuchukua muda mrefu kabla ya madikteta kugeuka na kuwa wafalme wakuu, sasa wakihodhi nguvu za utawala kwa maisha yao yote. Na wakati ambapo wafalme wakuu wa mwanzoni walikuwa hodari katika kudumisha viashiria vya kitaasisi vya Jamhuri ya zamani, hapakuwa na shaka kuhusu mahali ambapo nguvu ilikuwa imejilimbikiza.

## Kipindi cha enzi za kati

Bunge la Iceland linaloitwa *Althing*, lililoanzishwa mwaka 930 na ambalo bado lipo, linadaiwa kuwa bunge la kale kuliko yote duniani. Lilikuwa wazi kwa wote waliokuwa ‘watu huru’, ambao walikutana mara moja kwa mwaka mbele ya jiwe kubwa

lililobarizwa jina la ‘Jabali la Sheria’ katika mji wa Thingvellir. Mtu mmoja aliyeitwa spika wa Sheria, alikariri kwa sauti sheria iliyokuwepo (kitu kinachoashiria kwamba kulikuwa na sheria chache nzuri) na kulikuwa na mdahalo wa pamoja. Hata hivyo, ni wananchi maarufu hamsini pekee ambao ndio hasa *walifanya maamuzi juu ya* sheria.

Mwaka 1215, Mfalme John wa Uingereza aliyekuwa dhalimu alikabiliwa na malodi wake, wakimdai akubaliane na *Magna Carta* — ‘mkataba mkuu’ ulioweka ukomo katika nguvu za mfalme na hasa uliotoa sharti kwa malodi wa ngazi za chini kutoa idhini ya kutungwa sheria au kuanzishwa kwa kodi mpya. Hili lilikuja kuwa msingi mkuu ambao juu yake bunge la Uingereza lingekuja kujengwa (Butler 2015b).

Kwingineko barani Ulaya katika nyakati hizo hizo, majiji ya kibiashara yalikuwa yanaanza kuchipua, kila moja likijitengenezea kanuni zake lenyewe. Hii ilileta changamoto kwa kile kilichodhaniwa kuwa mamlaka ya tawala za kifalme yalitoka kwa Mungu; lakini dhana mpya ilijengeka kwamba maamuzi yalipaswa kufanywa kupitia muafaka wa wote badala ya mtawala mwenye nguvu kuwa na madaraka yote.

Hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya 1400, majiji ya Kitaliani yaliyokuwa himaya huru yaliweza kwa maana hiyo kuitwa *jamhuri*. Kwa usahihi zaidi, yalikuwa ni *serikali za kikatiba za utawala wa wachache*: ingawa uongozi ulikuwa wa makundi madogo zaidi kuliko umma wote, ufikiaji wa maamuzi ulikuwa bado ukitawaliwa na kanuni zilizokubaliwa. Na umuhimu wa maoni ya umma kwenye mchakato wa kisiasa ulitambuliwa vema: katika kazi yake maarufu juu ya ujuzi wa uongozi, mwanadiplomasia na mwanafalsafa Niccolò Machiavelli (1513) aliwashauri watu wachache waliokuwa wanatawala kwamba himaya zao zingeimarika zaidi na zaidi endapo wangeambatana na watu pamoja nao.

## Kipindi cha mwanzoni mwa enzi za kale

Kaskazini mwa Ulaya, hasa katika nchi za kibiashara zenye kupendelea mabadiliko kama vile Uholanzi, kiwango cha kulimbikiza nguvu za kisiasa kwa watu wachache kilishuka. Kukua kwa fikra za kidemokrasia kulisaidiwa zaidi na Mageuzi ya miaka ya 1500 na 1600, yaliyosisitiza usawa mbele za Mungu na kuinua kiwango cha elimu na kufuta ujinga: Waprotestanti wazuri walitakiwa kuwa na uwezo wa kujisomea Neno la Mungu wao wenyewe, kuliko kutegemea mamlaka ya kasisi.

Katika Visiwa vya Uingereza, mapambano ya utawala wa kifalme (*utawala wa mtu mmoja*) wenye nguvu zote dhidi ya fikra za kidemokrasia yalizaa vita ya wenyewe kwa wenyewe katika miaka ya 1640, pale ambapo Mfalme Charles I alijaribu kupandisha kodi bila ya ridhaa ya Bunge. Mwaka 1647, 'Wapinzani wa Mfumo wa Utawala wa Kifalme', waliopinga upendeleo wote kwa watu wa tabaka la juu, walifanya mdahalo wa kupata mbadala wa kuchukua nafasi ya utawala wa kifalme. Walitoa wito wa kuanzishwa kwa idadi ya kushangaza ya taasisi na taratibu za kisasa: serikali ya kidemokrasia, kupitia haki ya kupiga kura kwa wote (ijapokuwa wa kiume tu), chaguzi za mara kwa mara za viongozi na mipaka ya maeneo ya upigaji wa kura yaliyogawanywa kwa haki, watu wote kuwa sawa mbele ya sheria, kuvumiliana baina ya watu wa dini tofauti, na kuacha matumizi ya nguvu ya kuwalazimisha watu kujiunga na jeshi. Hata hivyo, aliposhika madaraka baada ya kumpindua Mfalme Charles I, kiongozi 'aliyetokana na mfumo wa bunge' aliyeitwa Oliver Cromwell hakuonesha nafuu yoyote ya utawala wa mtu mmoja kulinganisha na tawala ya kifalme aliyokuwa ameiondoa: aliamuru Wapinzani wa Mfumo wa Utawala wa Kifalme kukamatwa na alianzisha utawala wa kijeshi kwa miaka kumi na mbili.

Msukosuko huu ulisukuma watu kufikiri kwa kina juu ya chimbuko na lengo la nguvu ya serikali. Mwanafalsafa wa karne

ya kumi na saba kutoka Uingereza aliyeitwa Thomas Hobbes (1651) aliashiria kwamba serikali ilitokana na 'mkataba wa kijamii' ambao watu binafsi walipaswa kuwa wamekubaliana nao kwa ajili ya kuwapa hifadhi dhidi ya vitendo vya uchokozi na ulafi kutoka pande zote mbili. Aliamini kwamba mtawala wa kifalme, kama 'mkuu' wa serikali hii mpya, alipaswa kuwa na udhibiti tu kama kichwa kinavyofanya katika mwili wa mwanadamu. Hapakuwa na haki ya kuasi, kwa kuwa changamoto yoyote dhidi ya mamlaka ingeweza kuirudisha jamii katika hali ya vita. Hata hivyo, mwanafalsafa mwenzake wa Uingereza, John Locke (1689) alitumia dhana hiyohiyo ya 'mkataba wa kijamii' kuja na mwelekeo tofauti kabisa. Aliwafikiria watu waliounda taasisi za kitaifa nje ya serikali kwa minajili hasa ya kulinda haki zao za mtu mmoja mmoja na kupanua uhuru wao. Kwa hiyo, nguvu pekee ambazo serikali ilikuwa nayo juu yao ilikuwa ni ile nguvu pekee ambayo watu binafsi walikuwa wameihamisha kwa hiyari yao kutoka kwao hadi serikalini kwa ajili yakujilinda wao wenyewe. Wafalme walikuwepo ili kuwatumikia watu: hawakutakiwa kufanya chochote kile walichofikiri kinafaa. Na watu walikuwa na haki ya kupindua tawala ya kifalme iliyosaliti imani ya watu na kutawala kwa udhalimu.

Hadi wakati huo, mtawala mwingine tena wa kifalme, James II alikuwa amepinduliwa. Tawala ya kifalme ilirejeshwa tena pale tu aliyetazamiwa kuwa Mfalme William III alipokubali kuheshimu mamlaka ya Bunge pamoja na watu, kama yalivyowekwa katika Sheria ya Haki za Binadamu (1689). Kutokana na madaraka ya utawala wa kifalme kuwekewa ukomo kupitia utaratibu huu wa kikatiba, Uingereza ikawa *tawala ya kifalme ya kikatiba*. Bado inachukuliwa kuwa hivyo hadi leo hii — ingawa kwa kuwa sasa nguvu ya tawala ya kifalme imewekewa mipaka zaidi na mamlaka makuu yapo chini ya Bunge linalochaguliwa na umma kwa ujumla wake, ingekuwa sahihi zaidi kuiita kisasa, Uingereza, nchi inayofuata *demokrasia ya kikatiba*.

## Falsafa ya jamhuri ya kikatiba

Fikra za John Locke zilikuwa na ushawishi mkubwa kwa waasisi wa kile kilichokuja kuwa taifa la Marekani. Kama ilivyokuwa kwake, nao pia walikataa madaraka holela ya tawala za kifalme — wakitoa orodha ndefu ya 'matumizi mabaya ya madaraka na unyang'anyi wa Mfalme George III katika *Azimio la Uhuru* (1776). Walisisitiza usawa katika medani ya siasa, lakini bado walihofia demokrasia ingekuwa hatari kwa sababu ingeweza kuangukia kirahisi katika utawala wa kundi la watu wenye fujo. Walifanya mdahalo juu ya suala hilo na kuhitimisha kwamba uhusika wa watu wote katika mambo ya umma ulikuwa sehemu moja tu ya serikali bora. Kile walichohitaji kilikuwa ni *jamhuri* — serikali iliyoundwa kwa uangalifu kulingana na kanuni na misingi, ambapo maamuzi yangefanywa na wawakilishi wanaochaguliwa na watu, lakini ambao wangethibitiwa na sheria hizohizo kama ilivyo kwa mtu mwingine yeyote, na madaraka yao yakiwekewa ukomo na kutafsiriwa ndani ya katiba iliyoandikwa.

> Demokrasia siyo uhuru. Demokrasia ni mbwa mwitu wawili na mwanakondoo mmoja wanaopiga kura kuchagua kitoweo cha kula wakati wa mlo wao wa mchana. Uhuru unatokana na kuzingatiwa kwa haki fulani ambazo mtu hapaswi kunyimwa, hata kwa asilimia 99 ya kura.
> — Marvin Simkin (1992) 'Haki za Mtu Binafsi', *Los Angeles Times*

Mwanafalsafa wa Kifaransa aliyeitwa Montesquieu (1748) alikuwa ametoa hoja kwamba demokrasia isingeweza kamwe kufanya kazi vizuri kwa sababu watu wanayapatia maslahi yao wenyewe uzito wa juu zaidi kuliko maslahi ya jumla. Katika mifano halisi, wale waliopewa madaraka waliyatumia vibaya — hoja ambayo ndiyo hasa ilikuwa ikimtatiza Locke, Wamarekani, na wengi waliofuatia. Tiba pekee ya matumizi mabaya ya madaraka yanayofanywa na wenye mamlaka, alifikiri Montesquieu, ilikuwa ni *taratibu za mihimili ya dola kudhibitiana*: kupima kwa usahihi nguvu zote kupitia mlingano wa madaraka. Na miaka arobaini baadaye, fikra hizi zilichangia

katika uandishi wa Katiba Mpya ya Marekani, iliyobainisha utenganisho wa madaraka, wajumbe wenye nguvu ya wapiga kura, mipaka baina ya mamlaka na vyombo vingine vya kiutawala vilivyokusudiwa kuunda serikali ya uwakilishi *yenye ukomo*. (Japokuwa haki hizi na ulinzi wa kisiasa havikuwahusu watu takribani 800,000 waliokuwa watumwa na wenyeji wa asili walioishi huko kwa wakati huo).

Kwa mara nyingine tena, mambo yalikuwa tofauti nchini Ufaransa. Enzi ya Hofu (1793-4) iliyofuatia baada ya Mapinduzi ya mwaka 1789 iliwathibitishia waasisi wa taifa la Marekani kwamba walikuwa sahihi kuhofia juu ya uwezekano wa demokrasia kuteleza hadi kuwa machafuko. Imani ya wanamapinduzi wa Ufaransa kwamba utawala wao wa serikali ya wachache uliopatikana kwa njia ya kura ungeweza kuongozwa na ‘utashi wa pamoja’ wa umma ilikuwa potofu; kulikuwa tu na hali ya kutoafikiana na mabishano iliyochagizwa na vurumai za kikatili. Hofu ilisababisha mnadharia wa kisiasa wa Uingereza aliyeitwa Edmund Burke (1790) kulalamika katika kitabu chake cha *Tafakari za Mapinduzi nchini Ufaransa*, kwamba: ‘Katika demokrasia, walio wengi miongoni mwa wananchi wana uwezo wa kutekeleza ukandamizaji wa kikatili sana dhidi ya walio wachache’.

## Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko

Mwaka 1835, mwanazuoni mwingine wa Ufaransa, Alexis de Tocqueville, alichapisha kitabu kilichoitwa *Demokrasia nchini Marekani*. Mafanikio yanayoonekana wazi ya jamhuri ya Kimarekani, alihitimisha, hayakutokana na ugatuzi wa madaraka, au mlingano wake wa nguvu baina ya mihimili ya utawala, au mamlaka yake ya uamuzi (‘shirikisho’) na sifa nyingine za kikatiba, ingawa mambo haya yalikuwa na umuhimu mkubwa. Utamaduni wa kimaadili na kijamii wa Marekani, alifikiri,

ulikuwa na umuhimu wa kipekee pia. Asasi za kiraia — wingi wa makanisa, vyama vya kujitolea, vilabu vya uanachama, makundi ya msaada binafsi na jumuiya mbalimbali za watu wa Marekani — zilitumika kutoa elimu na kusimamia mijadala ya upigaji kura kwa umma. Maslahi ya pamoja na mwenendo mwema, alihitimisha, viliweza kudhibiti uwezekano wa kutumbukia katika utawala wa kundi la watu wenye fujo; lakini vilipaswa kuwa sehemu ya utamaduni ili viweze kufanya kazi.

Mwanafalsafa mkuu wa karne ya kumi na tisa wa Uingereza, John Stuart Mill, alikwenda mbele zaidi na kuweka misingi ya demokrasia ya kisasa yenye kupendelea mabadiliko (1861). Kama ilivyokuwa kwa Wagiriki, aliogopa udhalimu wa walio wengi, mbumbumbu na vigeugeu, waliofuata maslahi binafsi na kuwasikiliza viongozi waliokuwa na kipaji cha kushawishi watu kwa hisia badala ya fikra zao. Na wala demokrasia ya moja kwa moja halikuwa jambo ambalo lingewezekana katika dunia ya leo hii, ambapo jumuiya za watu ni kubwa zaidi kuliko Athens ya kale na ambapo haiwezekani kuwaleta wananchi wote pamoja. Mfumo pekee ambao ungeweza kufaa kwa sasa, alifikiri, ungekuwa *serikali ya uwakilishi*. Hata hivyo, wawakilishi hawakupaswa kuwa *wajumbe* tu, walioteuliwa kwa minajili pekee ya kuwa mwangwi wa hisia za wapiga kura wao. Badala yake, wanapaswa kufikiri na kutenda kwa kujitegemea na kuwajibika, hata endapo jambo hilo lilimaanisha kwenda kinyume na maoni ya watu wote. Kama Edmund Burke (1774) alivyokuwa ametangulia kusema hapo awali, katika 'Hotuba kwa Wapiga Kura wa Bristol': 'Unachomdai mwakilishi wako siyo bidii yake pekee, bali ni uwezo wake wa kufanya maamuzi mazito; na anafanya usaliti, endapo badala ya kukutumika, anautoa sadaka uwezo huo na kufuata maoni yako'.

Bado katika mfumo wowote wa serikali, haki na uhuru wa watu binafsi vinatangulia kwanza na sharti vilindwe, alisisitiza Mill. Hakufikiri kwamba haki kwa namna fulani zilitoka kwa Mungu au zilikuwa sehemu ya asili yetu, kama Locke na Wamarekani

walivyofikiri. Alifikiri zilikuwa kanuni za kimaadili tulizozifuata kwa sababu zilikuwa zinafaa. Na serikali inaweza kufanya kazi na kudumu endapo tu inaheshimu haki hizo na kulinda maisha, uhuru na mali za wananchi wake. Katika kitabu: *Kuhusu Uhuru*, Mill (1859) alionesha ni ukomo wa kiasi gani, aliofikiri ulipaswa kuwekwa katika uingiliaji kati wa serikali. Hata pale kulipokuwa na walio wengi waliopendelea kwa uwiano mkubwa sana kuweka vikwazo kwenye matendo ya watu, 'Lengo pekee ambapo nguvu inaweza kutumika kwa haki dhidi ya mtu yeyote kinyume na utashi wake katika jamii iliyostaarabika ni kuzuia madhara kwa wengine'.

## Kutanuka kwa demokrasia...

Hadi kufikia hapa misingi ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ilikuwa inaanza kujengeka, licha ya Bunge la Uingereza kuendelea kutokuwa la kidemokrasia. Hata hivyo, ukuaji wa falsafa ya kupendelea mabadiliko katika miaka ya 1800 ulizaa madai ya kukomeshwa kwa mfumo potofu wa upigaji wa kura — ambapo wamiliki wa maeneo makubwa zaidi ya ardhi ndio pekee walioweza kupiga kura, na ambapo baadhi ya wamiliki wa ardhi walidhibiti eneo la wilaya zote za kibunge, na ambapo rushwa, ufisadi na vitisho vilikuwa vimetapakaa. Sheria ya Mageuzi Makuu ya mwaka 1832 ilisaidia kuboresha hali ya mambo, ingawa matunda yake yalionekana katika kutanuliwa kwa wigo wa watu wenye sifa ya kupiga kura, ambapo sasa wamiliki wa maeneo yasiyokuwa makubwa sana ya ardhi na wakodishaji wa ardhi walipewa haki ya kupiga kura. Mageuzi mengine ya mwaka 1867 yalitanua zaidi haki ya kupiga kura katika chaguzi za umma na kujumuisha hadi tabaka la wafanyakazi 'walioheshimika' na waliopokea kipato cha wastani.

Ilichukua miaka mingi zaidi kabla ya wanawake kuweza kupiga kura nchini Uingereza — na kusema kweli, hata katika nchi

nyingine nyingi. Waasisi wa haki ya kupiga kura kwa wanawake walikuwa upande mwingine wa dunia, huko New Zealand na Australia (ijapokuwa wenyeji wa asili ya Australia walikuwa bado hawashirikishwi katika baadhi ya majimbo hadi baadaye sana mwaka 1965). Finland na Norway ziliruhusu wanawake kupiga kura kabla ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, kama Austria, Ujerumani, Poland, Urusi, Uholanzi, Marekani na Sweden zilivyofanya miaka michache baadaye. Uingereza ilitanua wigo wa kupiga kura kwa wanawake waliomiliki mali mwaka 1918, halafu kwa ujumla zaidi mwaka 1928. Lakini wanawake wa Ureno na Uswisi walilazimika kungoja hadi miaka ya 1970; na kuna baadhi ya nchi ambapo bado wanawake hawashiriki katika chaguzi za viongozi.

## …kupita mipaka yake?

Kutanuliwa kwa wigo wa haki ya kupiga kura katika chaguzi za umma, kutoka kwa wanaume waliomiliki mali hadi kwa wananchi wote, kuliongeza uhalali wa kisheria wa serikali ya uwakilishi (inayojulikana sasa duniani kote kama ‘serikali ya kidemokrasia’) na kupiga jeki dhana ya kwamba mbinu hii inapaswa kutumika katika wigo mpana zaidi wa masuala. Kutanuka huku kulitokea sambamba na mlipuko wa ustawi wa kiuchumi, jambo lililochangia wigo huo kutanuka zaidi (ingawa unafuu wa kiuchumi pengine ulitokana na kukubalika zaidi kwa fikra zenye kupendelea mabadiliko kama vile biashara huria na masoko wazi, kuliko kitendo pekee cha watu wote kupiga kura).

Karne ya ishirini ilishuhudia ‘demokrasia’ hii iliyopewa uhalali zaidi wa kisheria ikienea katika nyanja nyingi zaidi za maisha, ikisababisha chaguzi za mtu binafsi katika maeneo kama huduma za afya, elimu, akiba ya kiinua mgongo na utoaji wa misaada ya hisani kuwa chaguzi za pamoja. Kadri serikali ilivyozidi kuwa pana, ndivyo zilivyoibuka fursa zaidi na zaidi kwa makundi yenye maslahi kutumia ushawishi wao kupata upendeleo maalumu,

ufadhili, ruzuku, upendeleo katika kodi na manufaa mengine. Hadi kufikia mwishoni wa karne, tabaka la kisiasa la watu wenye uwezo katika jamii lilikuwa limechipua, likijumuisha wanasiasa, washawishi wa wanasiasa, watu kutoka katika mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, tume mbalimbali, mahakamani, wakala wa udhibiti, mashirika tanzu ya serikali, vyombo vya habari vya kisiasa, washauri bingwa wa sera na wengine — na kufuatia umakini wao, ni nyanja chache za maisha ya mtu binafsi ambazo hazikuguswa.

> Jenga picha kichwani mwako endapo masuala yote katika maisha yangekuwa yakiamuliwa kupitia utawala wa walio wengi. Kila mlo ungekuwa na piza. Suruali zote…zingekuwa dangirizi. Vitabu vya mapishi ya watu mashuhuri na mazoezi vingekuwa ndio kitu pekee kwenye shelfu za maktaba.
> — P. J. O’Rourke (1991) *Bunge la Makahaba*

## Kifo cha demokrasia?

Licha ya uhalali wa kisheria unaoonekana wazi wa serikali ya uwakilishi, baadhi ya wakosoaji wanaona uhalisia wake ni kushindwa kwa viwango vya juu. Kwa upande wao, tulichotengeneza siyo demokrasia bali ni utawala unaopatikana kwa njia ya kura, wa serikali ya watu wachache, wanaotafuta kumfurahisha kila mtu, ambapo maslahi yao binafsi, mkazo katika mipango ya muda mfupi na ukosefu wa msingi wa kuusimamia huishia kwa serikali kuongeza urasimu, kufanya teuzi kwa upendeleo na matumizi ya kizembe ya fedha ambayo ni makubwa kupita kiasi bila udhibiti wowote - na kukandamiza uhuru wa watu binafsi kwa kisingizio cha maoni ya walio wengi. Wanalalamika kwamba wengi miongoni mwa watu wa kawaida wametokea kuchukulia siasa kama kitu kisichokuwa na maana kwao au kilicho nje ya udhibiti wao - kitendo cha kujitenga kinachofanya hata iwe rahisi zaidi kwa tabaka la wanasiasa kuwanyonya. (Kama Pericles alivyowaambia Waathene, kwa

sababu tu hauna maslahi katika siasa haina maana kwamba siasa hiyo haina maslahi kwako.)

Hata hivyo, maisha na siasa katika nchi zenye mwelekeo wa demokrasia inayopendelea mabadiliko vinabaki kuwa huru na wazi zaidi kuliko katika tawala za wachache za nyakati zilizopita. Hata hivyo, mfano bora wa kidemokrasia unaweza kwa hakika kupotoshwa, na wala siyo tu kwa kuupuuza. Hata katika zama hizi za leo hii zinazochukuliwa kuwa nyakati za maarifa makubwa, serikali zinazojinadi zenyewe kuwa za ‘kidemokrasia’ mara nyingi sana zinahusika bado katika wizi wa kura, kunyima watu haki ya kupiga kura katika chaguzi za umma, udhibiti, utaifishaji, ukamataji holela, uingizaji wa siasa katika mahakama za kisheria na kuwaweka watu kizuizini bila ya kuwafungulia mashtaka. Kipaumbele cha kwanza katika kubadilisha hali hii ni kuwa bayana kuhusu maana hasa ya demokrasia na kufahamu ni taasisi na misingi gani inayoitegemeza.

# 3. TAASISI ZA KIDEMOKRASIA

Wakati ambapo karibia serikali zote duniani zinajinadi kuwa za kidemokrasia, huku zikifurahia uhalali wa kisheria ambao tafsiri hii inaashiria, ni chache sana zenye kuzingatia mfano bora. Nchi zinazochukuliwa kuwa ni tawala za ‘kidemokrasia’ huiba kura katika chaguzi za viongozi, huzuia ukosoaji kwa kudhibiti vyombo vya habari, hutumia polisi na mahakama za kisheria kuwatesa wapinzani, na viongozi wake hutumia vibaya nguvu za dola – kisheria na kifedha – kujitajirisha wao wenyewe na washirika wao. Ripoti iliyotolewa na Kitengo cha Intelejensia ya Kiuchumi (2019) ilihitimisha kwamba ni nchi 22 pekee, zenye asilimia 5.7 tu ya watu wote duniani ndizo zilizoweza kuitwa kihalali kuwa ni nchi ‘kamili’ za kidemokrasia, na 15 kati ya hizo zilipatikana Ulaya Magharibi. Ukweli ni kwamba, nchi zinazoweka neno ‘jamhuri ya kidemokrasia’ katika majina yao rasmi (kama vile Algeria, Ethiopia, Korea Kaskazini, Laos na Nepali) zina kawaida ya kuwa miongoni mwa tawala zenye kulazimisha utii kupita kiasi.

Kwa hiyo ni muhimu kutambua kwamba tunapaswa kuwa na dhana bayana ya demokrasia ni nini hasa, kuliko kudanganywa na tawala zenye kulazimisha utii ambazo zinajipotosha zenyewe kwa kujitafsiri kwamba ni tawala za kidemokrasia, ama kwa kukusudia au kutokana na kudanganyika. Tunahitaji kubaini misingi mikuu ya demokrasia ili tuweze kutofautisha nchi za demokrasia ya kweli na nchi za demokrasia bandia.

## Lengo na madaraka ya serikali

Kuanza mchakato, tunaweza kwanza kuhoji lengo la *serikali* ni nini, na kisha kuuliza jinsi ambavyo demokrasia husaidia kufikia lengo hilo.

Jibu kutoka kwa Locke, Mill na wanadharia wengine wenye kupendelea mabadiliko ni kwamba, licha ya wanadamu kuwa ni viumbe wa kijamii ambao kwa kiasi kikubwa huendana, mara nyingi wanaweza kushurutishwa na watu ambao wapo radhi kutumia nguvu kuwatawala, kuwapora au kuwafanyia hila. Kuwa na serikali huwezesha watu binafsi kuongeza uhuru wao hadi upeo wa juu kabisa kwa kuweka vikwazo dhidi ya matumizi ya nguvu kupitia mfumo uliopangiliwa wa kusimamia haki. Serikali, kwa maana hiyo, haina maisha yake ya kujitegemea au utambulisho wake yenyewe: ipo kwa sababu pekee ya kuwahakikishia wananchi  usalama na kulinda uhuru wao.

Wananchi wanahitaji kuipatia serikali nguvu ya kiasi fulani ili kufanikisha malengo haya — kwa mfano,  uwezo wa kutumia nguvu kukamata na kuadhibu wakosaji. Hii haina maana kwamba serikali inahitaji kutumia nguvu kubwa sana: bali ni sharti kwa serikali kutumia nguvu ilizonazo kwa niaba ya watu. Nguvu za serikali hazitakiwi kutumiwa kwa dhumuni la kuwadhibiti watu — jambo linalopingana na lengo lake kamili. Ni sharti utaratibu uwe *maridhiano ya pamoja*. Na kwa kuwa maamuzi ya serikali yanamgusa kila mmoja, watu wote wanapaswa kuhusika katika mchakato, huku mitazamo yao ikipewa uzito ulio sawa. Kwa sababu hiyo, kuna hitaji la aina ya fulani ya mfumo wa ufikiaji wa maamuzi kidemokrasia.

> Madaraka yana kawaida ya kupotosha, na madaraka yenye nguvu zote hupotosha kupindukia. Karibia mara zote, watu wakuu ni watu wabaya hata pale wanatumia ushawishi badala ya mamlaka; ni wabaya zaidi pale unapoongezea mazoea yao au unapokuwa na uhakika wa ufisadi unaofanywa na mamlaka.
> — Lord Acton (1887) *Barua kwa Askofu Creighton.*

Hata hivyo, kwa kuwa serikali *ina* nguvu za mabavu, kunabakia kitisho kwamba upande wa walio wengi unaweza kutumia nguvu hiyo dhidi ya wengine. Halikadhalika, kutokana na ukweli kwamba kila mwanadamu ana maslahi binafsi, tuna haki kukisia kwamba walio wengi watafanya hivyo. 'Katika mfumo wa serikali uliopangwa kwa ustadi', alionya mwanafalsafa wa Kiskochi wa karne ya kumi na nane, David Hume (1758), 'kila mtu hana budi kuwa kama laghai, na kutokuwa na ukingo mwingine…mrefu kuliko maslahi yake binafsi'. Miaka mia mbili baadaye, katika kitabu chake cha wakati wa vita: *Kuuendea Utwana*, mwanazuoni wa asili ya Uingereza na Austria, F. A. Hayek (1944), alionesha jinsi ilivyokuwa rahisi kwa demokrasia kutumbukia katika utawala wa imla wa genge la udikteta. Na kusema kweli, wakati wa janga la korona mwaka 2020, raia wengi wa nchi za kidemokrasia walishangazwa na nguvu kubwa walizokuwa nazo wanasiasa wao za kulazimisha vizuizi visivyoeleweka katika mienendo ya maisha ya kila siku.

Bila ya kuwepo udhibiti, utawala wa walio wengi hauyapatii makundi ya walio wachache na watu binafsi ulinzi dhidi ya maslahi ya walio wengi madarakani. Kwa sababu hiyo, kuna hoja ya kuwa na *demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko* iliyowekewa ukomo, ambapo haki za msingi za watu binafsi na uhuru wao daima vinaupiku uamuzi wowote wa walio wengi, na ambapo serikali huingilia kati kwa ajili tu ya kuhifadhi vitu hivyo (Butler 2013). Mipaka hii inaweza kuwekwa bayana kwa njia rasmi ndani ya katiba.

Hata hivyo, baadhi ya wanadharia wanaamini kitisho cha demokrasia kutumbukia katika ukandamizaji, ingawa kweli kipo, kimetiliwa chumvi kupita kiasi. Kwa mfano, mchumi mwenye asili ya Uturuki na Marekani anayeitwa Daron Acemoglu na mwenzake James Robinson wa Uingereza (2006) waligundua kwamba demokrasia inaweza kuchipua na kudumu mahali ambapo taasisi za kisiasa, mfumo wa kiuchumi na asasi za kiraia

ni imara. Vivyo hivyo, wanasayansi wa siasa André Alves na John Meadowcroft (2014) waligundua ukweli kwamba demokrasia imeenea na ipo imara katika nchi za demokrasia ya kiasi zinazofuata mifumo mseto ya kiuchumi (serikali na binafsi) — wakati mifumo ya utawala wa imla ikipambana ili kudumu kwa muda mrefu. Inaeleweka kirahisi tu, wanatoa hoja Alves na Meadowcroft, kwamba kuna ukomo wa mwisho katika ukubwa wa genge linalotawala na washirika wake, kwa kuwa kadri idadi ya wanyonyaji inavyozidi kuongezeka, ndivyo idadi ya wananchi zalishi wa kuwanyonya inavyopungua.

## Jukumu la msingi la demokrasia

Licha ya demokrasia kukubalika bila shaka kuwa ni *njia ya haki ya kufanya chaguzi kwa pamoja*, wanadharia wameiunga mkono kwa sababu nyinginezo. Baadhi wanadai kwamba demokrasia ni *nzuri kwa jinsi ilivyo* kwa sababu ni mfumo pekee wa serikali ambao msingi wake ni usawa wa kimaadili na kisiasa. Wengine wanasema inazalisha *matokeo mazuri* kama vile ushiriki wa kijamii, wajibu wa mtu binafsi, amani au ustawi. Ushahidi wa yote haya ni suala la mjadala.

Bado kuna faida moja bayana ya demokrasia ambayo mara nyingi haitiliwi maanani. Tuna kawaida ya kuichukulia demokrasia kwa sehemu kubwa kama njia ya *kuwachagua* watu wa kufanya uamuzi kwa niaba yetu. Hata hivyo, umuhimu wake hasa ni katika *kuwadhibiti* — na *kuwaondoa* kwa amani. Licha ya yote hayo, wabunge au wawakilishi siyo malaika: ni wanadamu tu kama sisi sote. Wanashawishika kirahisi na kupotoshwa na madaraka. Wakiwa madarakani, wanaweza kuanza kutanguliza maslahi yao wenyewe juu zaidi ya maslahi yetu. Au pengine, kadri muda unavyokwenda, mitazamo yao (au yetu) hubadilika na tunahisi kwamba hawafai tena kutuwakilisha. Kwa sababu yoyote ile iwayo, uwezo wetu wa kuwaondoa watu kutoka madarakani

wakati wa chaguzi za viongozi husaidia kuwazuia wasiweze kujilimbikizia na kutumia vibaya madaraka na kuwafanya wajikite katika umma ambao wanatakiwa kuuwakilisha. Kama alivyopata kusema mwanafalsafa wa karne ya ishirini mwenye asili ya Uingereza na Austria,  Sir Karl Popper (1945): '…siyo rahisi hata kidogo kupata serikali ambayo mtu anaweza kutegemea wema na hekima yake kwa imani yote. ... [Suala hili] linatushurutisha kubadili swali: *Nani anapaswa kutawala?* kwa swali jipya: *Tunawezaje kupangilia taasisi za kisiasa kiasi kwamba watawala wabovu au wasio mahiri  wasiwe na uwezo wa kusababisha madhara makubwa sana?'*

## Demokrasia ya moja kwa moja

Demokrasia, kama ambavyo tumeona, inaweza kuwa *ya moja kwa moja* au *ya uwakilishi*. Katika *demokrasia ya moja kwa moja*, umma wote huamua moja kwa moja juu ya masuala ya kisiasa (kama vile sera za viwango vya kodi, ulinzi au ustawi). Hata hivyo, ni nadra kwa demokrasia ya moja kwa moja kuonekana leo hii.

Sehemu mojawapo ambapo bado demokrasia ya moja kwa moja inadumu ni nchini Uswisi. Huko, nguvu kubwa za kisiasa zipo katika majimbo 27 na halmashauri zipatazo 3,000 kuliko katika serikali ya shirikisho. Majimbo yanatofautiana katika ukubwa, kuanzia Zurich lenye idadi ya watu milioni 1.5 hadi Appenzell Innerhoden lenye watu 16,000 tu. Kura za maoni zimezoeleka na majimbo madogo zaidi hutumia mabaraza ya wananchi. Mfano mwingine ni Mikutano ya Mji iliyofanyika katika miji takribani 1,000 ya New England. Tukirejea nyuma katika karne ya kumi na saba, mabaraza haya ndiyo yaliamua juu ya masuala yaliyohusu mahali fulani kama vile ujenzi wa barabara, utoaji wa leseni na bajeti — ingawa mchanganyiko halisi unatofautiana. Baadhi ya mabaraza haya, hata hivyo, yamebadilika na kuwa vyombo vya

uwakilishi, kufuatia miji mikubwa zaidi kuchagua wajumbe wa kuiwakilisha katika Mikutano ya Mji, badala ya kila mwananchi kuhudhuria. Na nchi za mataifa ya kisasa nazo pia ni kubwa sana kwa wananchi wao wote kukusanyika pamoja katika mabaraza ya utungaji wa sheria. Mara mojamoja zinaweza kuitisha *kura ya maoni* — ambapo watu wote wenye sifa ya kupiga kura huamua juu ya jambo mahsusi — lakini hii ni njia yenye usumbufu ya kufanya maamuzi yanayohitaji taarifa za kina katika masuala mazito yanayolikabili taifa la kisasa.

Baadhi ya wanaharakati wanatoa hoja kwamba demokrasia ya kisasa ingeweza kufanywa kuwa ya moja kwa moja zaidi kupitia upigaji wa kura kwa njia ya mtandao wa intaneti. Hata hivyo, bado kungekuwa na mipaka katika mambo ambayo walio wengi wangeweza kihalali kuamua. Na kuna mashaka endapo umma una shauku na stamina ya kutosha kwa ajili ya kutafiti sera na kufanya ufuatiliaji usio na mwisho wa maamuzi magumu ya kisiasa.

## Demokrasia ya uwakilishi

Kufuatia sababu kama hizi, desturi ya sasa ni *demokrasia ya uwakilishi* — ambapo umma wote kwa kwa ujumla wake hautungi sheria kwa pamoja, bali huchagua wawakilishi (kama vile mameya, wabunge na marais) wa kufanya maamuzi juu ya sheria na sera kwa niaba yao.

Wakosoaji wanatoa hoja kwamba hii siyo demokrasia ya kweli, kwamba kitendo cha kuajiri fundi mpaka rangi wa nyumba siyo sawa na kuipaka rangi nyumba yako wewe mwenyewe; na kwamba jukumu pekee la umma linabaki kuwa lile lililowekewa ukomo sana, la kuchagua tu watu watakaoendesha mambo. Hata hivyo, walau umma unahusika katika uchaguzi huo, kuliko kuwekewa watu wa kuutawala; na unabaki kuwa huru kujihusisha

kwa kina zaidi, kama vile watu kugombea uongozi na kushiriki katika mdahalo unaoendelea wa masuala ya umma.
Kwa kuongezea, mifumo mingi ya uwakilishi leo hii bado inaendeleza tanzu za udhibiti wa moja kwa moja wa umma, kama vile *kura za maoni* (ambapo umma kwa ujumla wake hupigia kura juu ya masuala ya msingi), *matamko ya umma* na *harakati za kudai mabadiliko* (ambapo makundi ya wapiga kura yanaweza kushinikiza kura ipigwe bungeni au kuitisha kura ya maoni), *ukomo wa mihula ya uongozi* (ambapo wawakilishi hawawezi kushika madaraka kwa zaidi ya muda uliowekwa) na *kura ya kutokuwa na imani* (ambapo wapiga kura wanaweza kumfukuza mwakilishi kutoka madarakani). Hata hivyo, kwa ujumla, wapiga kura wengi hupendelea kuacha siasa za kila siku kwa watu wenye muda wa kutosha, uwezo zaidi wa kufanya maamuzi na wenye maslahi katika siasa hizo, kuliko kufuatilia kila jambo wao wenyewe.

Hivyo, watu wanapoongelea 'demokrasia' leo hii, kwa kawaida wanamaanisha *serikali ya uwakilishi*, na hii imekuwa ndio maana ya kisasa ya neno lenyewe. Hata hivyo, matumizi haya ya neno 'demokrasia' yanazaa mkanganyiko. Yanarundika katika neno moja mchanganyiko mpana wa mifumo mingi tofauti. Vilevile yanaashiria kwamba unyofu wa demokrasia ya moja kwa moja (kama vile ushiriki wa umma wote katika utungaji wa sheria) nao pia unapatikana katika mifumo ya uwakilishi, hata ingawa katika baadhi ya mifumo kama hiyo, umma kwa ujumla wake una kauli ndogo sana au hauna kauli hata kidogo.

## Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko

Ndani ya wigo huohuo mpana wa mifumo ya uwakilishi kuna *demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko*. Hii ni mifumo ya uwakilishi ambayo inatawaliwa na misingi mashuhuri yenye mwelekeo wa mabadiliko. Kwa umuhimu mkubwa sana, inadai

kwamba haki za mtu binafsi — kama vile haki ya uhai, uhuru na mali — daima hazina budi kuheshimiwa: hakuna uamuzi ‘wa kidemokrasia’ unaoweza kuingilia misingi hiyo. Kwa mapana zaidi, hata hivyo, nchi ambazo huelezewa zaidi kama nchi za demokrasia ya mabadiliko mara nyingi huwa na sifa nyingine zinazofanana ambazo husaidia kufanikisha ulinzi huu, kama vile kanuni za kisheria zilizokubaliwa za jinsi ambavyo maamuzi hufikiwa, mipaka ya kikatiba ya nguvu za serikali, utenganisho wa madaraka ya mhimili wa kutunga sheria na mhimili wa serikali, na mfumo huru wa kusimamia haki. Pia zimeweka wazi uhusika wa umma katika mambo ya umma, kama vile chaguzi za uongozi kwa uhuru na haki ambapo mtu yeyote anaweza kugombea uongozi, kuruhusu ushindani wa vyama, vyombo huru vya habari na mdahalo wa wazi wa kisiasa.

Nje ya hapo, zinatofautiana katika namna nyingi. Baadhi ya mifano ya nchi ambazo kwa kiasi chake zinafuata demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ni *tawala za kifalme zilizowekwa kikatiba* (kwa mfano, Denmark, Japan, Hispania na Uingereza) — serikali huongozwa na tawala ya kifalme kwa jina tu, yaani ni tawala za kifalme ambazo madaraka yake yamewekewa ukomo kupitia kanuni za kikatiba. Nyingine ni *jamhuri* (kwa mfano, Ufaransa, Ireland na Marekani) ambapo viongozi huchaguliwa, lakini madaraka yao nayo pia yamewekewa ukomo kikatiba. Na katika kila mfumo, vipengele tofauti vya kikatiba — kama vile mkuu wa nchi (kwa mfano, mfalme au rais) na mabaraza mbalimbali ya kibunge (kwa mfano, Seneti au Baraza la Wawakilishi) na mihimili ya dola (serikali, bunge na mahakama) — vinaweza kuwa na viwango tofauti vya madaraka.

Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko siyo rahisi kuwa sahihi. Jinsi gani inapaswa kutenda kazi, au ni haki na uhuru gani inapaswa kuupa kipaumbele ufikiaji wa maamuzi kwa kura ya walio wengi ni maswali mazito na yenye utata. Kwa mfano, ni jambo linaloonekana wazi kwamba walio wengi katika nchi yenye kupendelea mabadiliko hawapaswi kuwa na nguvu ya kukamata

kiholela, kuwatupa jela au uhamishoni walio wachache wasiokubaliana nao; lakini kwa mfano; Je, wanaweza kihalali kuyatoza kodi makundi ya walio wachache — na kuamuru kodi za juu zaidi kwa matajiri? Je, wanaruhusiwa kuingilia kati mitindo ya maisha ya watu (kama vile kuwawekea ukomo wa matumizi yao ya dawa za usingizi au dawa za kulevya, pombe au sukari) katika tumaini la kuwaokoa wananchi dhidi ya madhara binafsi? Au kupanga masharti katika chaguzi za kiuchumi za watu (kama vile mahali pa kuishi au kufanya kazi) kwa maslahi ya taifa? Je, mamlaka katika nchi yenye kupendelea mabadiliko ziwe na uwezo wa kuminya uhuru fulani katika nyakati za vita au janga, au kupeleleza na kudukua mawasiliano ya wananchi wao kwa ajili ya kusaidia kupambana na kitisho cha ugaidi?

Hakuna majibu rahisi ya ndiyo au hapana ya maswali kama haya. Ingawa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko inasifika kwa kunyumbulika, mustakabali wake unaweza kuhakikishwa endapo tu kuna uelewa wa pamoja wa misingi inayoitegemeza.

# 4. MISINGI YA DEMOKRASIA

## Umuhimu mkubwa wa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko

Pale tunapotazama nchi ambazo mara nyingi huelezewa kama mifano ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko, kuna sifa na taasisi fulani ambazo huonekana wazi.

**Wigo mpana wa haki ya kupiga kura katika chaguzi za umma.** Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko inajengwa juu ya *wigo mpana wa haki ya kupiga kura katika chaguzi za umma na usawa katika hadhi ya kisiasa*: idadi karibia yote ya watu wazima wanakuwa na haki ya kupiga kura na kura zao zinapewa uzito ulio sawa. Watoto na watu wazima wenye ulemavu mkubwa wa akili wanaweza kuzuiwa kwa kigezo kwamba hawana umahiri wa kupiga kura; na katika baadhi ya nchi wafungwa waliopo gerezani (na hata waliomaliza vifungo na kutoka gerezani) wanaweza kuzuiwa kwa msingi kwamba uhalifu wao unawanyima sifa ya kushiriki katika masuala ya kijamii. Vinginevyo, wananchi wote wanajumuishwa.

Hata hivyo, nani hasa anayechukuliwa kuwa mwananchi, nalo ni suala la mjadala. Wakati fulani, ni wamiliki wa mali – wanaume pekee – ndio walionekana kuwa na maslahi ya kutosha ya kuwawezesha kupiga kura kwa kuwajibika nchini. Kufuatia sababu kama hizo, baadhi ya watu leo hii huwanyima haki ya kupiga kura wahamiaji wa hivi karibuni na wakazi wa muda.

Tatizo jingine ni kwamba, himaya inaweza kuwa na wakazi tofauti, waliogawanyika kupitia hisia zao za utaifa (kwa mfano, Warusi nchini Ukraine), lugha (kwa mfano, wazungumzaji wa Kifaransa nchini Kanada) rangi (kwa mfano, nchini Afrika

Kusini) au dini (kwa mfano, nchini Somalia, Bosnia, Iraq, Pakistan na kwingineko). Kila kundi linaweza kukataa haki ya wengine ya kufanya maamuzi ya pamoja ambayo yanawagusa. Misingi yenye mwelekeo wa mabadiliko hutoa tafsiri ya uananchi (uraia) kuwa ni jumuishi kadri inavyowezekana; lakini kanuni za uraia nazo pia zinatakiwa kuwa bayana na kukubalika kwa watu — jambo linaloweza kuwa gumu kufanikisha.

**Chaguzi za wazi za viongozi.** Nchi za demokrasia ya mabadiliko huruhusu mtu yeyote kugombea uongozi wa umma. Kwa mara nyingine tena, watoto, wafungwa au wale wenye ulemavu wa akili wanaweza kuzuiwa. Lakini watu hawapaswi kuzuiwa kuwa wagombea kwa msingi wa chama, dini, tabaka, familia, kabila au jinsia. Na wale waliopo madarakani hawajapewa mamlaka ya kuwatawala wapinzani wao kana kwamba ni watu wasioweza kushika uongozi. Nchi ya demokrasia ya mabadiliko huwaamini raia wake kufanya maamuzi yao wenyewe kuhusu nani anayefaa kuwawakilisha.

Chaguzi za viongozi katika demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko *mara nyingi*, ni *huru* na huendeshwa kwa *haki*. *Kila wakati*, nchi tofauti huwa na mitazamo tofauti juu ya vipindi vya muda ambapo chaguzi za viongozi wa nafasi tofauti unapaswa kufanyika. Marekani, kwa mfano, huchagua wawakilishi kila baada ya miaka miwili, marais kila baada ya miaka minne, na maseneta kila baada ya miaka sita. Ufaransa ilimchagua rais wake kila baada ya miaka saba hadi kura ya maoni ya mwaka 2000 ilipopunguza kipindi hicho kuwa miaka mitano. Na maeneo mengi huweka ukomo katika idadi ya mihula ambayo viongozi wa kuchaguliwa wanaweza kutumikia. Suala muhimu ni kuona kwamba chaguzi za viongozi zinafanyika mara kwa mara kadri inavyowezekana, na mihula ya uongozi kufupishwa kadri inavyowezekana, kwanza kwa ajili ya kuzuia mtu yeyote kujilimbikizia nguvu za utawala wa mtu mmoja, na pili kushawishi upande ulioshindwa kwamba itakuwa na maana zaidi

kungoja kwa amani hadi uchaguzi unaofuatia kuliko kukimbilia kwenye vurumai za kikatili.

*Chaguzi huru za viongozi* ni zile ambazo watu wote wenye haki ya kupiga kura wanaweza kupiga kura, na kuchagua nani wa kumpigia kura, bila ya kutishwa. Jambo hili kwa upande wake linahitaji matumizi ya kweli ya kura za siri. Nchi za demokrasia ya mabadiliko mara nyingi hutumia vyombo huru vya kusimamia uchaguzi ili kuhakikisha masharti haya yanafikiwa.

*Chaguzi za haki za viongozi* ni zile ambazo watu binafsi na vyama wanakuwa na haki sawa ya kushiriki katika uchaguzi, kuendesha kampeni na kufanya mikutano kwa amani, ambapo mipaka ya maeneo ya upigaji wa kura huamuliwa bila upendeleo na vyombo huru vya kusimamia uchaguzi (siyo kuamuliwa na wanasiasa walio madarakani), ambapo kura zinahesabiwa kwa kwa usahihi na ambapo kura hizo ndizo huamua matokeo. Hata hivyo, nchi mbalimbali bado zina mitazamo tofauti ya ‘sifa bainifu’ za kile kinachoitwa ‘haki’. Uingereza imeweka ukomo wa matumizi ya fedha za uchaguzi, kwa mfano, lakini siyo kwenye michango ya fedha kwa vyama vya siasa; wakati ambapo Marekani imeweka ukomo wa viwango katika michango ya fedha lakini siyo kwenye matumizi.

**Mdahalo huru.** Chaguzi za uongozi zinazofanyika kwa uhuru na haki hutenda kazi endapo tu masuala yanaweza kuibuliwa na kujadiliwa kwa uhuru. Hii inamaanisha haki ya uhuru wa kutoa maoni — ikiwa ni pamoja na haki ya kuwakosoa viongozi waliopo madarakani bila ya kufunguliwa mashtaka ya uchochezi au kutishwa vinginevyo. Ina maana ya kuwa na vyombo huru vya habari, visivyokuwa chini ya udhibiti wa serikali kwa manufaa ya viongozi waliopo madarakani. Na inahitaji watu kuwa na uwezo wa kupata taarifa sahihi kuhusiana na serikali — siyo ukiritimba wa serikali kwenye taarifa rasmi.

**Uwakilishi unaoaminika.** Watu wanaoshika nafasi za uongozi hawana budi kuwa wawajibikaji wa kweli mbele ya umma — kupitia mahakama huru za kisheria zinazotoa haki bila upendeleo, majaji na maofisa wa serikali ambao wananchi wanaweza kukata rufaa kwao endapo wanaamini kwamba wawakilishi wanatumia nguvu zao za madaraka kupita kiasi au wanakiuka haki za watu. Kunaweza hata kukawa na sheria inayoruhusu kuitisha kura ya kutokuwa na imani ya kuwaondoa wabunge au wawakilishi muda wowote endapo wapiga kura wao wameona kwamba wawakilishi wao wanatumia vibaya nafasi zao.

Na katika mkondo huu wa lengo la msingi la chaguzi za viongozi, ni sharti kwa wawakilishi kuheshimu matokeo ya uchaguzi na kujiweka tayari kukubali kushindwa pale wanapokosa kura za kutosha. Licha ya yote hayo, sehemu ya lengo la demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ni kuufanya mpito wa kisiasa kuwezekana na kufanyika kwa amani. Haitakiwi kutumia nguvu za dola kuwasaidia viongozi waliopo madarakani kudumu madarakani; kinyume chake, nguvu za dola zinapaswa kutumiwa katika kuhakikisha chaguzi za watu wenye haki ya kupiga kura zinaheshimiwa.

**Haki na misingi.** Pia ni muhimu kwa haki za msingi za watu binafsi kujulikana, kukubaliwa na watu, kuheshimiwa, na kuwekewa hakikisho la kisheria kiasi kwamba hakuna uwiano wowote wa wapiga kura walio wengi unaoweza kuingilia haki hizo. Haijalishi endapo haki hizi zinaonekana kama sehemu ya asili ya kuwa mwanadamu, au zinapitishwa kwa sababu zinaonesha kuwa zinafaa, ni sharti kuwe na makubaliano ya wazi juu ya haki gani watu wanapaswa kuwa nazo, na jitihada ya pamoja ya kuzilinda.

Kwa hakika, nchi tofauti za demokrasia ya mabadiliko zina mitazamo tofauti kidogo juu ya haki gani zinazopaswa kuwa ndiyo hizo haki za msingi. Nchi hizo zote zinakubali kwamba kila mtu ana haki ya uhai, uhuru, kutafuta furaha binafsi na umiliki wa

mali. Hata hivyo, kanuni zenyewe haswa — kwa mfano, kitu gani una ruhusa au hauna ruhusa ya kujenga kwenye ardhi yako, au makosa yanayoweza kuhalalisha mamlaka kukufunga jela — zinaweza kutofautiana.

**Katiba.** Nchi nyingi za demokrasia ya mabadiliko zimeandika katiba ambazo hulinda haki za msingi za watu, hubainisha mipaka ya nguvu zitokanazo na kura na hutoa utaratibu wa kufanya mambo kama vile kutenganisha madaraka ili kuwe na udhibiti. Hata hivyo, siyo lazima katiba iliyoandikwa kuwa katika kitita kimoja cha waraka: nchini Uingereza, kwa mfano, sheria na mapatano mbalimbali kuanzia Magna Carta, na Sheria ya Haki za Binadamu hadi Sheria ya Bunge na Sheria za Mgawanyo wa Madaraka hufasili kiini cha haki za watu na jinsi ambavyo serikali inapaswa kutenda kazi.

Kuhakikisha kwamba walio wengi hawawezi kirahisi kuhatarisha ulinzi wa namna hii, katiba nyingi zinahitaji uwiano mkubwa miongoni mwa walio wengi na mchakato unaofanyika kwa uangalifu kabla ya kuweza kubadilishwa. Mabadiliko katika Katiba ya Marekani, kwa mfano, yanahitaji kuungwa mkono kwa theluthi mbili ya kura katika Seneti na Baraza la Wawakilishi, pamoja na kuidhinishwa na robo tatu ya wawakilishi kutoka mabunge ya majimbo. Uingereza ni mfano wa peke yake: ambapo kinadharia Bunge linaweza kufanyia mabadiliko sehemu yoyote ya muundo wake wa kikatiba — ingawa kwa kawaida pendekezo lolote kama hilo linapasa kupitia mdahalo mrefu na mgumu sana wa umma.

Hatima yake, hata hivyo, hata katiba iliyoandikwa haiwezi kuhakikisha usalama wa haki na uhuru wa mtu binafsi: mambo yanayohitaji jitihada ya kina ya kitamaduni na kiakili miongoni mwa wananchi wote.

## Tanzu zenye manufaa za uwakilishi unaopendelea mabadiliko

**Ushiriki.** Kwa kuongezea katika sifa hizi zenye umuhimu wa lazima, kuna sifa nyingine zenye manufaa. Kwa mfano, inadhaniwa ni jambo linalofaa kuwa na utamaduni wa *ushiriki mpana, ulio hai na hiyari* katika mchakato wa kidemokrasia. Kufanya hivi huwezesha kupatikana kwa fikra tofauti na kuongeza uhalali wa kisheria wa mchakato — ingawa wenye kupendelea mabadiliko hukumbushia kwamba kinachoipatia demokrasia uhalali wa kisheria siyo kupandisha *uhusika wa kisiasa* hadi upeo wa juu bali ni kupandisha *uhuru na usalama wa mtu binafsi* hadi upeo wa juu kabisa.

**Wagombea.** Vyama vya siasa ni sifa yenye manufaa ya demokrasia kwa sababu vyama vinawapa watu wenye haki ya kupiga kura 'chapa' ya kufungamana nayo. Hata hivyo, jambo hili kwa mara nyingine tena linahitaji kuwekewa ukomo: endapo vyama vinajaribu kukumbatia kwa nguvu sana chapa zao (kwa mfano, kwa kupanga nini cha kusema katika jukwaa la uchaguzi la kila mgombea na 'kuratibu' kura zao bungeni), wagombea hupoteza uhuru wao na umma unanyimwa uwezo wa wakilishi wao wa kufanya maamuzi. Jambo hili linaashiria kwamba wagombea *wanapaswa kuchaguliwa kwa uwazi*, badala ya kutokana na orodha ya chama ya wagombea waliopitishwa (jambo linalofanya wajuzi wa mambo ndani ya chama kukamata kwa nguvu zaidi siasa za nchi).

**Shirikisho.** Kimsingi, maamuzi yanapaswa kufanyika kutokea ngazi ya chini kadri inavyowezekana, ili watu wanaofanya chaguzi wawe ni wale ambao chaguzi hizo zinawagusa, siyo watu wa mbali wenye ufahamu mdogo wa mazingira ya mahali husika. Lakini kiasi fulani cha udhibiti wa mamlaka kuu juu ya maamuzi ya mahali husika kinafaa. Kwa mfano, endapo eneo fulani mahsusi lina watu wengi zaidi wa kabila au dini moja, kama ambavyo mara nyingi hutokea, makundi ya walio wachache

yanaweza kukandamizwa na walio wengi. Katika maeneo makubwa zaidi, mwelekeo unakuwa wa mseto zaidi na kwa hiyo makundi ya walio wachache yana uwezekano mkubwa zaidi wa kuheshimiwa na kulindwa.

**Ustahimilivu wa raia .** Hata hivyo, ili kuyategemeza yote haya, demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko hufanya kazi vizuri zaidi mahali ambapo kuna kuvumiliana katika mitazamo inayopishana, uthabiti wa kijamii na kiuchumi, na amani.

Inabaki kuwa suala la kuhoji kuhusu idadi gani ya sifa hizi zifaazo kama ni kweli zimethibitika miongoni mwa nchi ambazo hujinadi kuwa za 'kidemokrasia' leo hii.

## Utendaji kazi wa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko

**Kusimamia haki.** Kama ambavyo tumeona, demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko kimsingi ipo kulinda na kupanua uhuru wa mtu binafsi na kuwakinga watu binafsi dhidi ya uonevu. Kwa hiyo inahitaji mfumo wa kusimamia haki kuzuia na kuadhibu vitendo vya udanganyifu na mabavu — ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka yanayofanywa na wenye mamlaka.

Ili jambo hili liweze kufanyika, *ni sharti sheria zitokane na msingi wa kanuni za maadili, ziwe bayana na thabiti* ili ziweze kwa ujumla wake kueleweka. Zinahitaji kuwa na uwezekano wa kutabirika kwa mapana zaidi, siyo kiholela, na sharti iwe ni jambo linalowezekana kuzitii. Mchakato wenyewe wa kusimamia haki ni sharti nao pia utokane na msingi wa kanuni za maadili na wenye uwezekano wa kutabirika, unaofuata 'mchakato stahili wa sheria', (kwa mfano) bila ya ukamataji holela na kuwaweka watu kizuizini, na ambapo watuhumiwa wanakuwa na haki ya kujua

mashtaka dhidi yao, kukabiliana na washtaki wao katika mashtaka ya haki au kubaki kimya bila ya uamuzi huo kuchukuliwa kuwa ni hatia dhidi yao.

Ili kulinda zaidi haki na uhuru wa mtu binafsi, ni sharti polisi, mahakama za kisheria na majaji kuwa huru — bila ya kuongozwa na nyendo za kufanikisha maslahi ya wale waliopo katika madaraka ya kisiasa. Kwa mfano, endapo watawala wanatuhumiwa kuiba fedha za umma, mfumo wa kusimamia haki unahitaji kuwa na uwezo wa kudai maelezo bila woga na kufungua mashtaka. Na endapo watawala wanajaribu kupindisha au kutafsiri vibaya katiba ili kutumikia maslahi yao wenyewe, ni sharti jambo hilo lipingwe pia.

**Haki ya kumiliki na kutumia rasilimali.** Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko huchukulia umiliki na matumizi ya mali siyo tu kama haki ya msingi bali kama ngome dhidi ya uonevu na kichocheo cha kupiga hatua za maendeleo ya kiuchumi. Mtu aliyewekeza muda na nguvu katika kutengeneza mali ana haki ya kuitumia na kuifurahia mali hiyo. Kwa hiyo mfumo wa kusimamia haki hulinda mali za watu kwa namna ileile unavyolinda wamiliki wake. Kanuni halisi zinaweza kutofautiana baina ya nchi tofauti, lakini ni sharti kwa watu binafsi kuwa na uwezo wa *kuwazuia* wengine kutumia mali zao, *kutumia* mali zao kwa uhuru wao wenyewe, na *kuzihamisha* mali hizo kama zawadi au kwa kuuza. Ni sharti kanuni hizi kuzingatiwa katika mahakama za kisheria.

**Utozaji wa kodi.** Kinga ya uhuru inahitaji mfumo wa ulinzi na usimamiaji wa haki, na kwa maana hiyo utozaji wa kodi huonekana njia ya maana ya kugharamia mambo hayo. Hata hivyo hii ina maana kwamba mali za watu —mfano fedha zao — huchukuliwa na serikali kwa lazima kutoka kwao, wakati serikali inapaswa kulinda mali hizo. Kutegemea michango ya hiyari kungefungulia mlango tatizo la ‘kupe’, ambapo baadhi ya watu wangetumia huduma zinazotolewa na serikali bila ya kulipia.

Endapo malipo ya lazima ndiyo uchaguzi pekee unaowezekana, demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko hufanya kazi ya kuhakikisha viwango vya kodi vinakuwa chini na kwamba kodi inatumiwa tu kwa ajili ya kuhifadhi haki na usalama wa wananchi. Hata hivyo, urahisi ambao walio wengi waliweza kutumia kigezo cha kodi kuyanyonya walio wachache (kama vile 'matajiri') umepelekea baadhi ya wapenda mabadiliko kama vile wachumi wa siasa wa Kimarekani, Geoffrey Brennan na James Buchanan (1980) kutoa hoja kwamba utozaji wa kodi unapaswa kuwekewa ukomo katika ukubwa wake, ulioundwa kuzuia matumizi mabaya, na ufanyike tu kwa ridhaa inayokaribia kuwa ya watu wote.

**Uhuru wa mtu binafsi.** Kama John Stuart Mill alivyoonesha, serikali hazina mamlaka juu ya maisha, uhuru na mali za watu isipokuwa kufanikisha malengo yaliyowekewa ukomo ya usalama na uhuru. Endapo kazi ya serikali ni kulinda uhuru, uhalali wa udhibiti wowote dhidi ya uhuru wa watu binafsi ni sharti uthibitishwe kikamilifu mapema kabla kutumika kwake. Serikali haiwezi kuzuia matendo ya watu kiholela au bila ya kuzingatia picha kamili.

Kuzingatia picha kamili ya sera ya umma inamaanisha kwamba, ni sharti watu binafsi wawe na haki ya kufikiri na kuongea kama wapendavyo, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kukosoa sheria na serikali bila ya hofu ya kudhibitiwa au kuadhibiwa. Ni sharti wawe huru kukutana pamoja, kuunda vyama vya siasa na kufanya kampeni katika chaguzi za viongozi. Haya mambo ni muhimu katika utendaji kazi wa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko; uhalali wa vizuizi vyovyote dhidi yake unapaswa kuthibitishwa kwa mapana.

Vivyo hivyo, watu wanapaswa kuwa na uwezo wa kuishi kadri wapendavyo. Serikali ipo kulinda uhuru wetu, siyo kupanga masharti katika mtindo wetu wa maisha. Pia, kuwa na mchanganyiko mbalimbali wa fikra na njia za kuendesha maisha

husaidia jamii kukua, kuendelea na kudumu. Na uhuru wa kudhibiti maisha yako mwenyewe ni jambo lenye umuhimu wa lazima kwa maendeleo ya mtu binafsi na kimaadili na katika kujifunza. Taifa la watu duni linalodhibitiwa na mamlaka halina uwezekano wa kupiga hatua za maendeleo, au kudumu katika dunia inayobadilika.

Kwa sababu uhuru na usalama ni shughuli ya msingi ya serikali, tuna kila haki ya kuiondoa serikali ambayo haitupatii mambo hayo — na hasa ile inayokiuka mambo hayo. Kimsingi mchakato huu unapaswa kupitia njia za amani, jambo ambalo ndiyo sababu kwa nchi za demokrasia ya mabadiliko kufanya chaguzi za viongozi. Lakini bado tuna haki ya kujilinda sisi wenyewe na mali zetu dhidi ya matumizi mabaya yanayoweza kufanywa na wengine, hata na serikali. Utaratibu wa amani wa kisiasa au kijamii una msingi wake katika imani, ushirikiano na mawasiliano: siyo katika nguvu, bali uhuru.

**Uhuru wa kiuchumi.** Uhuru wa kiuchumi hauwezi kutenganishwa na uhuru wa mtu binafsi. Taifa linalodhibiti rasilimali za kiuchumi hudhibiti maisha. Taifa linalodhibiti vyombo vya habari, linalomiliki maeneo ya kukutania, linalofanya ukaguzi wa machapisho na kuweka vizuizi kwa watu kusafiri linaweza kuzima ukosoaji wa umma na mdahalo.

Uhuru wa kiuchumi, katika hali yoyote ile, ndiyo njia ya uhakika zaidi ya ustawi kuliko udhibiti wa kisiasa wa rasilimali za kiuchumi. Kama mwandishi Matt Ridley wa Uingereza (2020) anavyoonesha, uvumbuzi wa mtu binafsi na ujasiriamali, na matumizi ya watu wengi, ndiyo mambo yenye umuhimu wa lazima endapo bidhaa na huduma zinatakiwa kuwa nafuu na bora zaidi. Uchumi huru unaweza kuendana na mabadiliko kwa haraka zaidi kuliko uchumi unaodhibitiwa.

# 5. NCHI ZA DEMOKRASIA YA UWAKILISHI LEO HII

## Serikali ya kibunge

**Madaraka ya mhimili wa kutunga sheria na mhimili wa serikali.** Kwa sehemu kubwa ya historia, mabaraza ya kutunga sheria yalikuwa vyombo vya watu wa tabaka la juu: dhana kwamba yanaweza *kuchaguliwa* na *kuwakilisha* umma wote ni dhana ya hivi karibuni. Bunge la Uingereza, kwa mfano, lilichipuka kutoka kwenye baraza la malodi wa ngazi za chini ambao walitafuta njia ya kudhibiti madaraka ya mfalme. Polepole, wamiliki wa ardhi wasiotokana na tabaka la juu waliongezwa kwenye orodha kama wanachama, lakini lengo la mabunge ya enzi za kati (kati ya mwaka 1100 hadi 1500) bado lilikuwa ni kulinda watu wenye mali dhidi ya nguvu ya kifalme, siyo kuwanufaisha watu wa kawaida.

Baada ya mivutano zaidi, sehemu kubwa ya madaraka katika tawala za kale za kifalme ilichukuliwa na Bunge lenyewe. Na Uingereza ilipeleka katika nchi nyingine aina hii ya *serikali ya kibunge* — ambapo madaraka ya serikali na chombo cha kutunga sheria hayajatenganishwa bado, ambapo mawaziri wakuu na mawaziri hukaa bungeni — (ikiwa ni pamoja na makoloni mengi ya zamani yakiwa sasa katika Jumuiya ya Madola).

Faida moja ya mtindo huu ni kwamba mawaziri wanawajibika moja kwa moja kwa watu wenye haki ya kupiga kura. Hata hivyo, kuwa na serikali bungeni kunadhoofisha jukumu lake la kulinda umma dhidi ya nguvu na madaraka ya serikali. Kinyume chake, mtindo wa Marekani wa mgawanyo wa madaraka huwezesha serikali kuchaguliwa kutoka kwenye wigo mpana zaidi wa weledi, na madaraka yake kupimwa kwa usahihi kupitia bunge huru; lakini tena, kunakuwa na umbali mkubwa zaidi baina ya mawaziri

na umma, na kwa kiasi kikubwa hawawajibiki moja kwa moja kwa watu.

**Mfumo wa baraza moja na mabaraza mawili.** Nchi nyingi za demokrasia ya mabadiliko zimeendeleza utaratibu wa mabunge yenye *mabaraza mawili*. Kuwa na mabaraza mawili ya kutunga sheria huwezesha kila baraza kuhoji na kudhibiti matendo ya baraza jingine. Tofauti zao hazina budi kupatiwa ufumbuzi kabla ya sheria kupitishwa, na kufanya iwe vigumu zaidi kuvunja haki za binadamu au haki za makundi madogo. (Hata hivyo, baadhi ya nchi zenye mfumo wa bunge lenye *baraza moja*, kama vile Norway, Iceland, Denmark, Sweden au New Zealand, zinaheshimu haki za mtu binafsi kimadhubuti zaidi; wakati baadhi ya nchi nyingine zenye mfumo wa bunge lenye *mabaraza mawili*, kama vile Urusi au Zimbabwe, pengine zinaheshimu haki kama hizo kwa kiwango cha chini.)

Endapo wabunge kutoka katika kila baraza wanachaguliwa kwa njia tofauti, inaweza kuleta wigo mpana zaidi wa mitazamo ya maoni kwenye mdahalo wa umma. Kwa mfano, Marekani huchagua wawakilishi kwa uwiano wa watu unaokaribia kuwa sawa kwa maeneo; lakini kila jimbo huchagua maseneta wawili tu, bila ya kujali ukubwa wake; hii husaidia katika kuhakikisha kwamba maslahi ya majimbo madogo zaidi yanasikilizwa. Maseneta wa Australia huchaguliwa kupitia mfumo wa *upigaji kura unaopelekea eneo moja kutoa mwakilishi zaidi ya mmoja*, ambao unazalisha hali ya kuwa anuwai kwa kiwango kikubwa zaidi katika baraza hili kuliko *kura ya marudio* au mfumo *wa upigaji wa kura ambapo mpiga kura huweka alama kuonesha chaguo lake la kwanza hadi la mwisho kwa wagombea wote waliopo kwenye karatasi ya kura* unaotumiwa katika Baraza la Wawakilishi.

## Mifumo ya urais

Pale ambapo madaraka ya kutunga sheria yametenganishwa na madaraka ya serikali, mara nyingi serikali huongozwa na rais. Majukumu ya rais hutofautiana baina ya nchi na nchi. Katika baadhi ya nchi kama vile Ireland, kwa kiasi kikubwa ni cheo cha heshima tu. Katika nchi nyingine, kama vile Marekani, rais ana nguvu kubwa katika serikali: miongoni mwa mambo mengine, rais wa Marekani ana madaraka ya kuteua mawaziri na maofisa wa serikali, kutoa mapendekezo ya bajeti, kukataa sheria zilizopitishwa, kufanya mapatano ya mikataba na hata kutangaza vita.

Marais wanaweza kuchaguliwa kwa njia ya kura ya watu wote au kuchaguliwa na wabunge au wawakilishi. Hata hivyo, endapo wanachaguliwa kupitia haki ya watu wote ya kupiga kura katika chaguzi za umma, wanakuwa na uhuru na uhalali wa kisheria wa kuzuia taratibu za sheria zilizowekwa na bunge zinazoweza kuwa kitisho kwa uhuru na usalama wa umma kwa mapana yake — kizuizi cha nyongeza chenye manufaa dhidi ya madaraka ya rais.

## Tawala za kifalme zilizowekwa kikatiba

Ukweli ni kwamba, idadi ya kushangaza ya nchi za demokrasia ya mabadiliko ni *tawala za kifalme zilizowekwa kikatiba* — ambapo, kama ambavyo tayari imetajwa, madaraka ya tawala ya kifalme yamewekewa ukomo kupitia mapatano au kanuni za katiba iliyoandikwa. Nchi hizo zinajumuisha Uingereza na nchi za Jumuiya ya Madola kama vile Australia, New Zealand na Kanada. Ulaya pia ina tawala za kifalme zilizowekewa ukomo kama vile Ubelgiji, Denmark, Uholanzi na Hispania.

Madaraka halisi ya tawala hizi za kifalme hutofautiana. Hata hivyo, tawala za kifalme ambazo kwa kiasi kikubwa ni hadhi ya

heshima tu (kama ambavyo nyingi zilivyo) zinaweza bado kuwa na kiasi fulani cha mamlaka. Kwa mfano, wakati wa jaribio la mapinduzi nchini Hispania mwaka 1981, mfalme mpya aliyekuwa amerejeshwa enzini, Juan Carlos, alitoa amri kwa vikosi vya jeshi kurejea makambini — kwa mafanikio. Suala lenye umuhimu mkubwa katika tawala za kifalme zilizowekwa kikatiba linaweza kuwa siyo madaraka waliyonayo, bali madaraka wanayowanyima watu wengine, kama vile maofisa wa jeshi, majaji na wanasiasa.

## Jukumu la umma

Wakosoaji wengi wanaona 'umbumbumbu wa wapiga kura' kama dosari kuu katika demokrasia. Hata hivyo watu wenye haki ya kupiga kura hawana haja ya kufuatilia wao wenyewe na kuelewa maelezo ya kila sera: kazi yao ni kuchagua tu wawakilishi watakaofanya hivyo kwa niaba yao. Utambulisho wa chama wenye maelezo, wenye kuonesha msimamo mpana wa mgombea juu ya masuala, inaweza kuwa ndiyo taarifa yote wanayohitaji watu wenye haki ya kupiga kura.

Kwa watu wenye haki ya kupiga kura, mifumo ya uwakilishi ina manufaa zaidi kwao kuliko mifumo 'shirikishi' inayomhusisha kila mmoja katika ufikiaji wa maamuzi. Wanaweza kutingwa na matatizo yao wenyewe au kuwa na muda au maslahi kidogo katika midahalo ya kisiasa; hivyo, kuna mantiki kumwachia kazi hiyo mtu mwingine mwenye shauku na muda wa kufanya mambo hayo. Na wapiga kura wanaweza kuamini kabisa kwamba wabunge au wawakilishi wanaowachagua wana weledi wa juu na uwezo mzuri zaidi wa kufanya maamuzi ya kisiasa kuliko wanavyoweza kufanya wao wenyewe.

Kitu gani basi huwazuia wanasiasa wasitumie vibaya madaraka ya ufikiaji wa maamuzi ambayo wapiga kura wamewapatia? Ukiweka pembeni mapinduzi, ni kitisho cha kushindwa katika

uchaguzi. Kwa mara nyingine tena, jukumu la msingi la umma katika demokrasia siyo *kuchagua* viongozi bali ni *kuwaondoa*.

Ni kweli kwamba umma unaweza kabisa kupendelea viongozi imara, na kuwapatia madaraka makubwa; lakini hakuna kiongozi anayeweza kuendelea kwa muda mrefu kuwa imara endapo anapoteza ridhaa ya watu. Kupitia chaguzi za uongozi kwa uhuru na kufanyika kwa haki, mabadiliko katika uongozi yanaweza kutokea kwa amani. Na kupitia uhuru wa kutoa maoni, mdahalo wa wazi na chaguzi za viongozi zinazoaminika, wanasiasa hawana budi kushindana ili kupata kibali na ridhaa ya umma, na kuwa mfano mzuri kwa ajili ya kuchaguliwa tena.

## Hakikisho la usalama wa mchakato

Upigaji wa kura siyo kitendo chenye umuhimu wa lazima kwa mtu binafsi, ingawa katika demokrasia kitendo hicho huamua nani — au siyo nani — wa kuunda serikali. Hata hivyo, kuunda serikali huambatana na madaraka, hivyo daima kuna kitisho kwamba makundi yenye maslahi maalumu na makundi ya kisiasa yanaweza kutumia udanganyifu, rushwa, uonevu, wizi wa kura na njia nyingine haramu kugeuza matokeo ya uchaguzi. Kinachotia wasiwasi zaidi, wale waliopo madarakani wanaweza kufanya jaribio la kubadilisha kwa hila mipaka ya maeneo ya uchaguzi, kutumia rasilimali za taifa kushawishi wapiga kura, kutumia vyombo vya umma vya habari kudhoofisha wagombea, kutumia polisi, jeshi na mahakama za kisheria dhidi ya wapinzani wao, au kudanganya kirahisi tu kuhusu idadi ya kura zilizopigwa kwa kila mgombea.

Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko inahitaji utaratibu wa kufanya mambo ili kupambana na vitisho hivi, kama vile kuwa na tume huru za mipaka na uchaguzi, uangalizi wa kimataifa wa chaguzi za viongozi, kanuni juu ya matumizi ya wagombea ya rasilimali za taifa na vyombo vya umma vya habari, na adhabu

kwa kufanya udanganyifu katika uchaguzi. Hata hivyo, kizuizi bora kabisa ni utamaduni unaokataa ufisadi kama huo.

## Mifumo ya upigaji wa kura

Kuna mifumo mingi tofauti ya upigaji wa kura, na mara nyingi watoaji wa maoni wanakuwa na mitazamo mikali juu ya mfumo upi unaozalisha matokeo 'bora kabisa'. Hata hivyo, kitu 'bora kabisa' ni suala lala mjadala; katika uhalisia, kila mfumo una yote mawili; uimara na udhaifu wake.

*Ushindi kwa wingi wowote wa kura* (UWWK) ni mfumo uliozoeleka, ambapo mgombea mwenye kura nyingi zaidi huchaguliwa. Ni mfumo rahisi, mwepesi kuuelewa, haupotezi muda na hutoa matokeo bayana. Pia huwapa watu wenye haki ya kupiga kura mwakilishi mmoja wa kumwendea endapo wana matatizo na serikali au wanataka kuelezea mitazamo yao. Kwa upande mwingine, endapo kura zilizopigwa zitakuwa zimegawanywa baina ya wagombea wengi, mtu mwenye kuungwa mkono na walio wachache tu anaweza kuchaguliwa. Mfumo huu hutoa upendeleo kwa siasa ya vyama viwili, jambo linalopunguza uwezekano wa kuenea kikamilifu kwa maoni ya umma. Na endapo wilaya za upigaji wa kura ni ndogo, mara nyingi mfumo huu hutengeneza urahisi wa mwakilishi aliyepo madarakani kutetea kiti chake, kitu kinachowanyima kabisa wapiga kura wa upande ulioshindwa nguvu zozote za kura .

Ili kupunguza matatizo haya, mifumo mbalimbali ya *uwakilishi kwa uwiano wa kura* imebuniwa. Mmojawapo ni mbinu ya *kura mbadala*. Wapiga kura huonesha chaguo lao la kwanza hadi la mwisho kwa wagombea wote waliopo kwenye karatasi ya kura, na wagombea wenye kura chache huenguliwa mmoja baada ya mwingine, na kura za uchaguzi wao wa pili wakipewa wengine, hadi mmoja wao anapofikisha kura za walio wengi. Manufaa yake ni kwamba uchaguzi wa kila mmoja unathaminiwa — walau kwa

kiasi fulani. Lakini tena, mfumo huu ni mgumu kuuelewa na kuusimamia. Unatoa upendeleo zaidi kwa wagombea kutoka nje ya vyama vikuu kuliko UWWK, lakini tena, jambo hili linaweza kutoa mwanya kwa vyama vyenye mrengo mkali.

Kibadala ni kuwa na majimbo yenye mwakilishi zaidi ya mmoja, ambayo yanaweza kuwa makubwa zaidi na kwa maana hiyo uwezekano wa kiwango cha chini kwa chama kimoja tu kutetea kiti chake, ambapo wagombea huchaguliwa kupitia mfumo wa *upigaji kura unaopelekea eneo moja kutoa mwakilishi zaidi ya mmoja*, kwa wagombea walioshindwa kuenguliwa hadi idadi ya wagombea inapooana na idadi ya viti vinavyogombewa. Lakini mchakato huu ni mgumu zaidi hata kuuelewa na kuufanyia kazi. Unaweza pia kuwaacha wapiga kura bila uhakika wa nani anawawakilisha. Wagombea wanaweza pia kuwa na shauku zaidi ya kupitishwa katika orodha ya chama kuliko kuwakabili wapiga kura.

Kwa bahati mbaya, mifumo kama hii ya uwiano mara nyingi huzaa serikali iliyojengwa katika msingi wa 'muungano wa masharti' (mara nyingi ukihusisha vyama vidogo vyenye mrengo mkali), jambo linalopunguza uwezekano wa kutafakari maoni ya umma na inaweza kuwa vigumu kuwaondoa. Kwa upande mwingine, UWWK na mifumo mingine isiyokuwa ya uwiano hupelekea hatari ya kutoa uwakilishi wa chini kwa vyama visivyokuwa vikuu katika nchi.

Vibadala vingine vingi vimezoeleka, kama vile *mifumo ya uwakilishi mseto* ambapo, endapo chama kinapata mgao mkubwa wa kura kitaifa lakini kinashinda viti vichache, kinapewa viti vya nyongeza vilivyotengwa kutoka katika orodha ya wagombea wa chama hicho. Lakini kwa mara nyingine tena, jambo hili huzalisha wagombea waliojikita zaidi kuingiza majina yao katika nafasi za juu kwenye orodha ya chama kuliko kuwakabili wapiga kura.

Kwa ajili ya chaguzi za urais, Marekani hutumia mfumo wa *baraza la wapiga kura*. Watu hawapigi kura moja kwa moja kumchagua rais, bali huchagua wawawakilishi kutoka eneo lao ambao ndio hupiga kura kuchagua rais. Mfumo huu umesanifiwa ili kuepusha wapiga kura kutoka majimbo makubwa sana kuwaelemea wale wanaotoka katika majimbo madogo zaidi, ili kuhakikisha kwamba kila sehemu ya nchi inapewa uzito; lakini pia inamaanisha kwamba rais anaweza kuchaguliwa kwa kura zilizopigwa na walio wachache, kama ilivyotokea kwa Donald Trump mwaka 2016 na George W. Bush mwaka 2000.

Kwa kuhitimisha, hakuna mfumo wa 'haki' wa upigaji wa kura usiotia shaka yoyote. Hata hivyo, endapo mfumo wa upigaji wa kura kwa ujumla wake ukiwa wazi, wa haki na wenye kuruhusu mabadiliko, basi walau walioshindwa wanaweza kukubali kushindwa na kuwa radhi kungojea uchaguzi mwingine, badala ya kubeba silaha.

## Uwajibikaji kwa umma

Nchi za demokrasia ya mabadiliko — kwa namna ya kipekee — huwajibishwa katika matumizi yake ya mali ya umma kupitia njia nyingi tofauti. Kwa mfano, bunge linaweza kuchelewesha au kuiwekea vikwazo shughuli ya serikali. Mahakama za kisheria zinaweza kuhakikisha kwamba maamuzi yanafikiwa na kutekelezwa kisheria, na kwamba haki za watu zinalindwa. Vyombo vya habari na wataalamu walio huru wanaweza kujadili ustadi wa sera za serikali. Watu wenye haki ya kupiga kura wanaweza kuiadhibu serikali kupitia masanduku ya kura. Mtindo wa Kimarekani wa kura za mchujo na taratibu nyingine za uchaguzi vinaweza kusaidia katika kuhakikisha kwamba wagombea wanafaa kweli katika uongozi. Kura za maoni na haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya mabunge vinaweza kuwadhibiti zaidi waliopo madarakani. Mfumo wa shirikisho, ambapo madaraka huanzia ngazi za chini kadri inavyowezekana

(ngazi ya chini kabisa ikiwa ni mtu binafsi), huwezesha watu kuepuka mamlaka dhalimu yaliyojiweka mbali nao. Na aina nyingi za makundi ya wananchi yana sauti kubwa katika mdahalo wa kitaifa.

Katiba ni udhibiti wenye manufaa zaidi na inaweza kutoa hakikisho lenye thamani katika haki za msingi na uhuru wa watu binafsi. Lakini mchakato wa kutunga katiba unahitaji uangalifu: unaweza kuhodhiwa kirahisi na vyama vinavyotawala au kutekwa na makundi yenye itikadi kali au makundi yenye maslahi yanayotafuta kuongoza taasisi za kisiasa kwa manufaa yao wenyewe.

## Mvutano kati ya demokrasia na haki

Demokrasia inatarajiwa kuwa mizani inayotafuta usawa baina ya haki za mtu binafsi na utashi wa walio wengi. Kipaumbele cha demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ni haki. Hata hivyo, mlingano halisi wa usawa hauwezi kamwe kufikiwa, kwa sababu kamwe hakutakuwa na makubaliano kamili katika hali ya mambo. Kitu gani watu wana haki ya kufanya au kusema hadharani, au kujenga kwenye ardhi zao, au kununua kwa kutumia fedha zao (kama vile kucheza kamari, kununua mahaba, dawa za kulevya au pombe) ni masuala la mdahalo. Haki siyo mambo yasiyopingika: ni maoni ya kisiasa ya misingi ya kimaadili — ambayo watu wanaweza kupingana juu yake. Kazi ya wapenda mabadiliko ni kuhakikisha kwamba, kwa kadri inavyowezekana, kile kinachozingatiwa kuwa ni uhalali wa kisheria wa maamuzi ya walio wengi kisitumike kunyonga uhuru wa walio wachache — na hatimaye, uhuru wa kila mmoja.

# 6. MANUFAA YA DEMOKRASIA

## Kuzuia ulimbikizaji wa madaraka

Pengine manufaa makubwa kabisa ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ni kwamba huwezesha umma kubadili viongozi wao kwa amani, bila ya kuwa na hitaji la kufanya vurumai za kikatili. Kwa upande wa tawala za kidikteta, kitisho cha uasi na mapinduzi daima ndilo jambo kuu zinazohangaika nalo, na zina kawaida ya kuwa na majeshi makubwa ili kuzuia jambo hilo lisitokee. Hata hivyo, nguvu za kijeshi kama hizo zinaweza pia kutumika kwa ujumla wake kuzuia ukosoaji na kujilimbikizia madaraka.

Kinyume chake, mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi husaidia kuzuia viongozi au makundi ya kisiasa kujiongezea na kujilimbikizia madaraka. Na hata pale ambapo serikali inapoteza umaarufu miongoni mwa watu, bado kunakuwa na uwezekano mdogo wa kutumia mabavu kwa sababu kitisho cha mapinduzi ya kikatili ni mdogo andapo chaguzi za viongozi zinafanyika mara kwa mara. Kunapokuwa na amani, jitihada na akili ya mwanadamu vinaweza kuelekezwa katika shughuli zalishi zaidi na kujitajirisha.

## Kupokea mabadiliko

Nchi za demokrasia ya mabadiliko zina kawaida ya kujirekebisha. Zina uwezo wa kuendana na mabadiliko katika matukio, na katika mitazamo ya umma. Zinaweza kufanya hivyo vizuri zaidi kuliko mifumo mingine mingi, kwa sababu hazifungwi na mwelekeo mmoja wa mtazamo au itikadi au hisia potofu za upendeleo kuhusu jinsi ambavyo jamii inapaswa kwenda. Itikadi na hisia

potofu za upendeleo hulazimisha njia moja iliyowekwa ya kufanya mambo, na kupinga mabadiliko au mchepuko wowote nje ya njia hiyo; lakini demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko hukumbatia mabadiliko na kuyaingiza katika matumizi mazuri. Kwa mfano, demokrasia huvumilia fikra na mitindo mingi tofauti ya maisha. Hivyo, pale ambapo mazingira hubadilika, tuna chaguzi nyingi za kufaa kati yetu, zinazoweza kutusaidia kuyashinda, kuyapokea, kuyachepusha au kuyatumia mabadiliko hayo kujinufaisha. Na kwa miaka nenda rudi, maoni ya umma yanaweza kubadilika katika masuala mengi muhimu — kama vile uhamiaji, huduma za ustawi wa jamii, hitaji la uingiliaji kati wa kijeshi au haki za kijinsia; midahalo na maamuzi ya kidemokrasia hubadilika kuendana na harakati hizo. Demokrasia ni mfumo kwa ajili ya aina yoyote ya jamii.

Kupitia kuvumiliana, uwazi, hali ya kuwa anuwai na wepesi wa kulegeza msimamo katika nchi za demokrasia ya mabadiliko, nchi hizo zinaweza kuonekana dhaifu sana na zenye kutilia mkazo wa jambo kwa kiwango cha chini kulinganisha na tawala za kidikteta, hasa pale zinapokabiliwa na vitisho vikubwa au mabadiliko ya ghafla kama vile vita na majanga ya asili. Lakini sifa hizo huzipatia pia nchi hizo hali ya kunyumbulika na uwezo wa kushangaza — kama mafashisti na viongozi wengine wa kidikteta walivyogundua huko nyuma.

## Kuhoji maadili yetu

Faida nyingine ambayo watoaji wengi wa maoni wanaiona katika demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ni kwamba inakumbatia na kuhifadhi maadili muhimu ya mwanadamu, kama vile usawa katika medani ya siasa kwa watu binafsi. Bila kujali namna yoyote ambavyo wananchi wanaweza kutofautiana sana katika mambo mengine, mfano katika kipato au utajiri, bado kila mmoja wao anaweza kushiriki katika mchakato wa upigaji wa kura.

Wapo huru kuwa wapiga kura, kujiunga na chama chochote cha siasa, kugombea au kuwa wapiga kampeni bila hofu ya ubaguzi au ukandamizaji. Haijalishi endapo watu hao ni matajiri au maskini, wana ujuzi au hawana ujuzi, wanatoka mjini au mashambani, wamezaliwa ukoo wa kifalme au ukoo wa kitwana, au vyovyote vile asili yao ya kikabila au dini au rangi au tabaka au familia au mitazamo yao ya siasa inavyoweza kuwa. Kwa upande wa kisiasa, mitazamo yao inapewa uzito unaolingana.

Wachunguzi wengine wanasifia kigezo cha namna demokrasia inavyoweza kutia moyo ushiriki katika jamii — au walau, haimzuii au kumbagua mtu yeyote kushiriki katika siasa kwa sababu tu kuna watu serikalini wanaoamini kuwa mtu huyo hana sifa, hafai, ni msumbufu au anaweza kuwa mhaini. Na wala watu katika nchi ya kidemokrasia hawajagawanyika katika kundi la watu wanaodhaniwa kwamba wanafaa kutawala na watu wanaodhaniwa kwamba wanafaa tu kutawaliwa — ambazo ni hisia potofu za upendeleo wa ajabu uliozoeleka katika tawala nyingine. Chini ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko, kila mmoja yupo huru kuwa mwananchi 'hai' na kugombea uongozi, na halaiki pana ya watu ndiyo huamua ni mambo gani yaliyo muhimu zaidi kwao.

Hali iliyoenea ya watu kuhusika katika masuala ya kijamii husukuma mbele maendeleo ya wananchi kitaaluma, kimaadili na kisiasa pia, wanasema mashabiki wa mfumo huu. Huwapa watu mambo mawili; jambo la kwanza ni fursa na motisha ya kutafakari na kushiriki mdahalo juu ya chaguzi za kisiasa na kimaadili, na jambo la pili ni kuhusu hatua za kisera zinazoweza kutoa suluhisho la mambo hayo katika njia bora kabisa.

## Kuinua kiwango cha sera inayoaminika

Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ina maana ya kwamba tunaishi chini ya serikali na sheria ambazo tunachagua sisi wenyewe — walau kwa kiwango fulani — badala ya kuishi chini ya madaraka ya viongozi waliowekwa juu yetu. Hali hii hupunguza matumizi ya nguvu katika jamii au hitaji la kulazimisha watu wakubaliane na maamuzi ya serikali ya kidikteta. Ni mbinu ya maridhiano zaidi ya kufanya mabadiliko ya kisiasa ambayo huepusha migogoro.

Chaguzi huru za viongozi na zinazoendeshwa kwa haki pamoja na serikali ya uwazi inayozingatia demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko huchochea pia uwajibikaji na uwazi miongoni mwa watu wanaogombea au kuchaguliwa kuwa viongozi. Kadri wanasiasa wanavyoshindana kupata kibali cha umma katika chaguzi za viongozi, ndivyo ambavyo kumbukumbu za utendaji wao, uwezo na tabia zao hupitia uchunguzi makini. Au kama raia wa Marekani, H. L. Mencken (1956) alivyowahi kusema: 'Chini ya demokrasia daima chama kimoja hutumia nguvu zake zote kikijaribu kuthibitisha kwamba chama kingine hakina uwezo wa kutawala — na mara nyingi sana vyote viwili hufanikiwa na vyote huwa sahihi'. Hata hivyo, licha ya mchuano baina ya vyama, wagombea wataangaliwa kwa karibu na watu wenye haki ya kupiga kura; mapungufu yao yatawekwa wazi; na wengine watakabiliana na maswali ya kichunguzi kutoka vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; na makundi yenye maslahi yatawachimba juu ya misimamo yao ya sera.

Wataadhibiwa pia, wale wasiokuwa waminifu. Endapo wananchi wanatokea kuamini kwamba watu waliowachagua ni wala rushwa, au hawatoshi katika nafasi zao, au wamefanya maamuzi mabaya – wanaweza kupiga kura ya kuwaondoa — ama kwenye uchaguzi unaofuatia au kupitia kura ya kutokuwa na imani kama ilivyo katika baadhi ya nchi. Kinyume chake, katika mifumo ya utawala wa mtu mmoja, viongozi wabaya hawawezi kuondolewa

kirahisi; na mara nyingi wale waliopo katika uongozi watang’ang’ania madarakani, na katika sera zao pia, hata pale ambapo zinawaangusha.

## Ukosoaji na kupiga hatua za maendeleo

Ustahimilivu ambao ni mmoja kati ya misingi mikuu ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko huwezesha ukosoaji wa wazi wa uongozi wa nchi — kitendo ambacho mara zote huwa si busara kufanya na pengine hata isiwezekane kufanya hivyo katika tawala za kidikteta. Kufuatia kuwa na kinga dhidi ya ukosoaji, madikteta wanaweza kuficha kashfa na kuhakikisha kwamba makosa yao yanasetiriwa au kupuuzwa. Mara nyingi huwa inasemwa kwamba mabunge ni sehemu ya kupigia porojo tu, lakini uwezo wa kuongea kwa uhuru katika jukwaa la wazi ni muhimu katika kuwaanika viongozi na kuhoji fikra zao. Mdahalo huo wa umma ndiyo chanzo cha taarifa kwa wapiga kura pale wanapotaka viongozi wao kutoa majibu katika uchaguzi unaofuatia.

Jambo hili ni kigezo muhimu pia kwa mwanadamu katika kupiga hatua za maendeleo. Ukweli ni kwamba, kuna manufaa ya wazi ya kupima mapendekezo ya sera mpya ya umma na fikra zote juu ya jambo lolote kupitia mdahalo wa wazi, ambapo watu wanaweza kuonesha uwezo na udhaifu wa fikra hizo. Jambo hili huwezesha fikra zenye mwelekeo wa kuwa nzuri kufanyiwa maboresho zaidi, na fikra dhaifu kufanyiwa mabadiliko au kutupiliwa mbali kabla ya kusababisha madhara. Kwa kuzingatia ‘busara ya watu’, wanasema mashabiki wa mfumo huu, demokrasia inaweza kupelekea maamuzi mazuri zaidi ya kisera kuliko mifumo ambayo maamuzi ya mamlaka hayapitii changamoto wala kujaribiwa katika mdahalo wa wazi.

## Kulinda haki za mtu binafsi

Bruce Bueno de Mesquita na wenzake (2003) waligundua kwamba zilizounda taasisi za kidemokrasia zenye ubora wa hali ya juu hufanya vizuri katika upande wa kulinda haki za binadamu. Pengine huenda siyo kweli kwamba demokrasia hujizalia tu manufaa haya; bali yawezekana nchi zenye kuthamini zaidi haki zinaamini pia kuwa demokrasia huzilinda haki hizo kwa njia iliyo bora kabisa. Kwa njia yoyote ile, nchi za demokrasia ya mabadiliko zina kawaida ya kulinda sana haki kama vile maisha, uhuru, umiliki wa mali, uhuru wa kukusanyika, uhuru wa kutoa maoni na ushiriki sawa katika mchakato wa kisiasa.

Japokuwa mifumo ya kidemokrasia na suala la kuheshimu haki kwa kawaida huambatana pamoja, kuna mvutano ambao huwa unabaki kati ya utashi wa walio wengi na haki za binadamu. Walio wengi, na wanasiasa wao wa kuchaguliwa, wanaweza kabisa kuamini kwamba kuna sababu nzuri ya kudhibiti haki za watu. Kwa mfano, wanaweza kuamua kwamba, kwa ajili ya kuukinga umma dhidi ya kitisho cha ugaidi, polisi na mamlaka za usalama wanapaswa kuwa na uwezo wa kukamata na kuweka watu kizuizini kwa vipindi virefu vya muda, kufanya msako holela mitaani na msako wa nyumba kwa nyumba, na kuzuia uchapishaji wa mitazamo mikali ya kisiasa. Au, katika kupambana na majanga, wanaweza kuamua kufunga biashara na kuwafungia watu katika makazi yao. Kwa bahati mbaya, hakuna mipaka bayana kati ya ulinzi wenye uhalali kisheria wa maisha, mali na usalama wa wananchi na ukandamizaji haramu wa wananchi kwa jina la serikali ya kidemokrasia. Kwa maana hiyo, mapendekezo yote hayo ya kudhibiti haki yanapaswa kuchunguzwa vikali na kupimwa kwa uangalifu na umakini mkubwa sana.

## Amani na ustawi

Mara nyingi huwa inasemwa kwamba nchi za kidemokrasia huwa hazibebi silaha na kutangaza vita kati yao. Huu siyo ukweli kamili: katika matukio kadhaa zimefanya hivyo. Hata hivyo, bado kuna sababu nyingi kwanini nchi za kidemokrasia zinaweza kuishi pamoja kwa amani zaidi kuliko aina nyingine za serikali. Wapiga kura kwa ujumla wao hawapendelei sana migogoro ya kivita kama walivyo madikteta wa kijeshi; kwa kuwa wana kikubwa cha kupoteza, na licha ya yote hayo, serikali ya kidemokrasia haiwezi kirahisi kupuuza maisha, usalama na mali za raia wake.

Inaweza kukubalika kwamba, nchi za demokrasia ya mabadiliko pia zimepiga hatua zaidi katika ustawi wa kiuchumi. Serikali bora na ustawi vimekuwa bega kwa bega kwa kipindi cha karne mbili zilizopita. Lakini haipo wazi sana dhana ya kwamba demokrasia *hutengeneza* ustawi zaidi. Nchi nyingi, ikiwa ni pamoja na Uingereza, zilipata utajiri muda mrefu kabla ya kuruhusu haki ya kupiga kura kwa wote au kufanya chaguzi zao za viongozi kuwa za haki na zenye kuaminika. Hivyo, haiwezekani demokrasia kuwa ndiyo sababu iliyozaa utajiri wao. Endapo kuna kigezo kimoja pekee chenye kuchochea ustawi, basi inaweza kukubalika bila shaka yoyote kwamba siyo demokrasia bali ni utamaduni wa *kuheshimu haki za mtu binafsi*, kama vile kuruhusu watu kufanya kazi, kuzalisha bidhaa na kufanya biashara kwa masharti wanayojiwekea wao wenyewe. Na tunaona kwa mara nyingine tena, nchi za kidemokrasia zina uwezekano mkubwa zaidi wa kuheshimu haki hizo.

Ingawa demokrasia ina sifa njema ya kushangaza, ina uwezekano pia wa kuchelewesha mabadiliko haya ya uhuru na ustawi. Maadili ya kuwa na upande wa walio wengi kupitia masanduku ya kura yanaweza kuipa serikali hali ya kujiamini ya kuwanyonya wanaotengeneza utajiri. Jambo hili hupunguza tunzo zitokanazo na shughuli za biashara na kukatisha tamaa uvumbuzi, uwekezaji

na kujituma katika kazi, wakati huohuo linaongeza uzembe na ulafi. Hali hii hudhoofisha afya ya ustawi.

## Hitimisho

Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko inaweza kabisa kuwa na manufaa ya kweli walau kuliko mifumo mingine — na hasa uwezo wake wa kukubali mabadiliko na kubadili viongozi au sera kwa amani. Inaweza kuchochea utungaji mzuri zaidi wa sera, kulinda haki za watu binafsi, kusaidia ustawi na kuhamasisha amani. Lakini mengi kati ya haya yanayochukuliwa kama manufaa yapo bayana kwa kiwango cha chini kuliko inavyoweza kudhaniwa. Na demokrasia haikosi wakosoaji wake.

# 7. UKOSOAJI WA DEMOKRASIA

Demokrasia inaweza kuwa na manufaa yake, lakini pia ina gharama zake. Inatatua matatizo mengi, lakini inatengeneza mengine. Wakosoaji wanatoa hoja kwamba ni vigumu kwa demokrasia kuwa sahihi, pia ni rahisi kukosea. Kumbukumbu za utendaji wake siyo kitu kisichokuwa na dosari. Ongezeko la vyama vyenye malengo ya kumfurahisha kila mtu linaweza kuwa ni ushahidi kuwa wengi miongoni mwa wapiga kura hudhani kwamba demokrasia haikidhi mahitaji ya watu kadri inavyotakiwa. Ina hatari ya kufanya teuzi za upendeleo, urasimu, serikali kubwa kupita kiasi, unyonyaji, ukosefu wa maono miongoni mwa wapiga kura (na miongoni mwa wanasiasa wanaoweza kuwa madarakani kwa muda mfupi tu) na ukiukwaji wa haki za watu binafsi. Je, ni kweli kwamba demokrasia inazingatia sifa zake bainifu za kiutendaji au hata sifa za kimsingi?

## Watu wenye haki ya kupiga kura hawapo tayari kwa kazi

Jambo moja muhimu ni swali endapo wapiga kura wanaweza kuwa msingi mkuu unaotegemewa wa kujenga mfumo wowote wa baraza lolote linaloweza kuaminiwa katika kufanya maamuzi muhimu. Dalili siyo nzuri: kwa kiasi kikubwa watu wenye haki ya kupiga kura hawana taarifa kamili juu ya masuala ya kisiasa. Hii inaweza kusababishwa na mpiga kura kuona kwamba kura yake moja ni kama haina nafasi hata ndogo ya kuamua matokeo ya uchaguzi. Inaweza kuwa ni kura moja dhidi ya mamilioni. Hivyo, hakuna haja ya usumbufu wa kutafuta taarifa kuhusiana na

masuala ya sera pale ambapo kura yako inasababisha tofauti ndogo sana au haisababishi tofauti yoyote hata kidogo.

Bila kujali kipi ni chanzo cha msingi, umbumbumbu wa kina kwa wapiga kura unashtua. Kulingana namchumi wa Kimarekani, Bryan Caplan (2007) katika *Kisa cha Kufikirika cha Mpiga Kura mwenye Kufikiri kwa Mantiki:*

> Karibia nusu ya Wamarekani hawajui kwamba kila jimbo lina maseneta wawili, na robo tatu hawajui urefu wa vipindi vya mihula yao. Karibia 70% hawawezi kusema chama gani kinadhibiti Baraza la Wawakilishi na 60% hawawezi kusema chama gani kinadhibiti Seneti. Zaidi ya nusu hawawezi kutaja jina la mwakilishi wao, na 40% hawawezi kutaja jina la yeyote kati ya maseneta wao…. Licha ya hayo, viwango hivi vya chini vya maarifa vimekuwa hivyo tokea mwanzoni mwa historia ya upigaji wa kura, na mlingano wa kimataifa unaonesha maarifa ya ujumla ya kisiasa kwa Wamarekani kuwa chini ya wastani.

Na wala hawatumii kura zao mara zote kumchagua mgombea wanayempenda – kama wanadharia wa demokrasia wanavyochukulia. Kinyume chake, wanaweza kumpigia kura mgombea mwingine, na nyakati fulani huwapigia kura wagombea wenye msimamo mkali kwa minajili ya kupeleka tu ujumbe wa kutoridhishwa na serikali yao, au hata kwa nia ya kupaza sauti juu ya maoni yao mazito lakini yasiyofanyiwa kazi kufuatia umbumbumbu wao, ubaguzi au hisia potofu za upendeleo. (Inasemekana kwamba, mwanasiasa na mwanadiplomasia wa Kimarekani wa karne ya ishirini anayeitwa Adlai Stevenson II alipoambiwa na watu waliomuunga mkono kwamba angepata kura ya kila mtu mwenye akili nchini Marekani, alijibu ‘Ninafurahi kusikia hivyo; lakini nahitaji kura ya walio wengi!’).

Kwa upande wake, mazoea haya ya watu kupiga kura kwa hisia zaidi kuliko mantiki huchochea wagombea “kucheza” na hisia hizo. Katika kutafuta umashuhuri na kura, wagombea wa uongozi (na wanasiasa wa kuchaguliwa pia) huteka hisia za wapiga kura, kwa kutumia zaidi kaulimbiu na vipande vifupi vya sauti

iliyorekodiwa kuliko hoja tarajiwa na zenye mantiki. Yote haya, wanasema wakosoaji wa demokrasia, huzalisha matokeo ya uchaguzi na sera ya umma inayotokana na msukumo mkubwa zaidi wa mtu kung'ang'ania mawazo au imani yake pamoja na umbumbumbu kuliko ushahidi na mantiki.

Wagombea na wanasiasa wa kuchaguliwa hujielekeza pia katika maslahi binafsi ya washawishi wa wanasiasa wanaoweza kuteka ngome kubwa na iliyojizatiti ya wapiga kura ambao uungaji mkono wao unategemewa — katika chaguzi za viongozi, katika kampeni za vyombo vya habari na nyakati fulani kifedha.

Tunzo zenye uwezekano wa kupatikana kutokana na ushawishi zinaweza kuwa kubwa sana. Unaweza kupata tahafifu ya kodi katika sekta yako, au kushinikiza kanuni za kisheria za kuwaondoa washindani wako, au kupata mkataba mnono wa serikali, na inaweza kupelekea tofauti kubwa sana kwenye biashara yako au kusudio lako. Ukweli ni kwamba, tunzo zenye uwezekano wa kupatikana ni kubwa sana kiasi kwamba vituo vya serikali ya kidemokrasia — kama ilivyo katika eneo la barabara za mjini zenye njia nyingi huko Washington DC au katika 'Kijiji' ambacho ni eneo la Westminster la jiji la London — vimefurika makampuni ya ushawishi na ofisi za mahusiano ya umma za mashirika makubwa.

Hata hivyo, ushawishi hugharimu muda, jitihada na fedha. (Kampuni moja ya washauri mabingwa kutoka Washington inakadiria gharama za za kifedha peke yake kuwa takribani dola za Kimarekani bilioni 3.5 kwa mwaka.) Kwa maana hiyo, watu wanaohusika katika ushawishi kwa ujumla ni wale wanaotoka katika kundi lililojizatiti au lenye maslahi binafsi ya kubadilisha sera ya umma, au wanaotafuta upendeleo na huduma maalumu kutoka kwenye mamlaka za serikali. Maslahi yao yanaweza kuwa (na mara nyingi huwa) tofauti sana na maslahi mapana zaidi ya umma. Yote haya hufanya ushawishi kuwa njia ya gharama kubwa, iliyojaa ubaguzi, isiyotoa uwakilishi na isiyo na mantiki

ya kuathiri maamuzi ya kisera ambayo watu wote nchini hawana budi kuyaheshimu; lakini wakosoaji wanasema kwamba, hiki ni kitu cha asili katika demokrasia yenyewe.

> Pendekezo la sheria yoyote mpya au hatua za udhibiti wa biashara litokanalo na maslahi hayo, halina budi kuchukuliwa kwa tahadhari kubwa sana, na halipaswi kuungwa mkono hadi kwanza lifanyiwe tathmini makini na ya muda mrefu na kulichunguza kwa kina, siyo tu kwa uangalifu mkubwa, bali kwa kulitilia mashaka ya hali ya juu. Pendekezo la namna hii hutokana na genge la watu, ambao maslahi yao hayafanani na maslahi ya umma, ambao kwa ujumla wao wana dhamira ya kudanganya na hata kukandamiza umma, na ambao vivyo hivyo, kwa nyakati mbalimbali, walidanganya na kukandamiza umma.
> — Adam Smith (1776) Utajiri wa Mataifa, Kitabu I, Sura ya XI

## Inafanya maamuzi yasiyofaa …

Kwa kiasi kikubwa, nchi za kidemokrasia zinachukuliwa kwamba hazifanyi vizuri katika kufikia maamuzi magumu, yenye utata au ya dharura. Kwa sababu ya mitazamo tofauti mingi sana inayotolewa miongoni mwa pande mbili za umma na wanasiasa, inaweza kuwa vigumu kufikia muafaka na isiwezekane kufanya mchakato wa chaguzi kwa haraka. Masuala ya dharura ya kitaifa, yanayohitaji mwitikio wa haraka, siyo mazuri kwa muda wa mijadala mirefu ya bunge . Na pale ambapo madaraka yamegawanywa baina ya mabaraza tofauti ya kutunga sheria au baina ya bunge, serikali na mahakama, inaweza hata kuchukua muda mrefu zaidi kukubaliana juu ya sera.

Aidha, pale ambapo masuala yana utata wa hali ya juu, hata kama siyo dharura, idadi ya mitazamo inayohitaji kupatanishwa inaweza kupelekea midahalo mirefu na mitata ya bunge na umma. Kama waziri mkuu wa zamani wa Uingereza aliyeitwa Clement Attlee (1957) alivyopata kusema: ‘Demokrasia ina maana ya serikali inayoendeshwa kwa njia ya mjadala, lakini inafanya kazi kwa ufanisi pale tu unapoweza kuwazuia watu kuongea’. Na pale ambapo mtazamo wa maoni ni nusu kwa nusu, au ambapo kuna

uwezekano wa chaguzi nyingi tofauti, mchakato unaweza hata kuishia kwenye mkwamo. Mara nyingi, mambo huweza kupatiwa ufumbuzi kwa njia mithili ya ‘mapatano ya bei’ — katika kufanya upendeleo wa aina mbalimbali kwa makundi tofauti, mara nyingi usiokuwa na maana, kwa ajili ya kununua uungaji mkono wao — badala ya kutumia msingi wa ushahidi na mantiki.

## …na mabaya

Kuna sababu nyingine nyingi kwa serikali ya uwakilishi iliyochaguliwa kidemokrasia kuweza kufanya maamuzi mabaya. Nguvu za dola hufanya iwe rahisi kwa walio wengi kuwanyonya wengine — hasa katika masuala la kuwalazimisha kulipa kodi au kutaifisha mali zao. Na pale ambapo maamuzi ya walio wengi yanapofanikishwa kupitia nguvu za dola na kile kinachochukuliwa kuwa ni uhalali wa kisheria wa kuwa ‘ya kidemokrasia’, panakosekana ukomo bayana wa kiasi gani unyonyaji huu unaweza kufikia. Kibaya zaidi, huu ni wizi ulioruhusiwa kisheria. Matokeo yake, kitisho cha kupandishiwa kodi na utaifishaji huwavunja watu moyo wa kujituma katika kazi au kulimbikiza mtaji zalishi na utajiri. Pia ni uamuzi usio na tija: wakosoaji wanasema kwamba, watu wanaotumia kipato chao wenyewe huenda wakatumia kipato hicho kwa uangalifu mkubwa na kubana matumizi kuliko wanasiasa wanaotumia fedha wanazozipata kwa nguvu kutoka kwa walipakodi.

Vibaya kupindukia ni kwamba, kupitia hisia potofu za wapiga kura, mara nyingi wanasiasa hufanya maamuzi madhara yanayoonekana wazi. Kwa mfano; karibia wachumi wote hukubaliana na uzuri wa biashara huria, lakini wanasiasa, wakisukumwa na mashaka ya wazalishaji na umma kuhusu kutoka nje ushindani, mara nyingi sana wanaidhinisha sera za kujilinda kama vile ukomo wa kiasi cha kuagiza kutoka nje na ushuru wa forodha. Kwa upande wao, kitisho kinachowakabili

cha wapiga kura kulalamika kwamba ‘wageni kutoka nchi za nje wanachukua ajira zetu’ kina uzito mkubwa zaidi kuliko ustawi utakaonea siku zijazo kutokana na biashara enye kupendelea mabadiliko.

## Inatilia mkazo mipango ya muda mfupi

Ufikiaji mbaya wa maamuzi unachochewa na kigezo kwamba kazi ya viongozi wa kuchaguliwa huchukua kipindi kifupi cha muda. Wanafurahia sifa za muda mfupi kwa kubuni sera zinazotoa majibu kwa matatizo yote ya watu, lakini ni nadra kwao kuendelea kubaki madarakani kwa muda mrefu wa kutosha kuwajibishwa kwa madhara yoyote muda mrefu ambayo sera hizi husababisha. Kwa hiyo wanapata ujasiri wa kisiasa wa kukopa au kuchapisha fedha zaidi kwa ajili ya kuongeza matumizi yao, huku wakiwaacha warithi wao kushughulika na deni la serikali au mfumoko wa bei utakaotokea.

Mfumo wenye mantiki zaidi wa serikali, wanasema wakosoaji, ungezaa sera ziliyokusudiwa kutengeneza ustawi wa muda mrefu wa kwa wananchi wake — siyo ule uliozaa sera zinazotokana na msukumo wa shauku ya muda mfupi ya wanasiasa wanaotafuta kupendwa. Mfumo wenye mantiki usingeruhusu watu zalishi kutozwa kodi na kunyonywa kwa lengo pekee la kuridhisha husuda ya walio wengi au shauku ya walio wengi ya kujipatia manufaa ya bure kwa gharama ya wengine. Lakini bila ya kuwekewa mipaka mikali, mifumo ya ‘kidemokrasia’ hufanya hivyo kwa hakika. Badala ya kusaidia kujenga uwekezaji kwa ajili ya siku zijazo, wanaiba na kutumia mtaji kwa matumizi ya leo hii. Kwa vyovyote vile, hali hii husababisha madhara ya muda mrefu dhidi ya ustawi wa jamii nzima.

Na kwa kuwa karibia kila mmoja anahusika katika mchakato huu kama mpiga kura, wanaambiwa kwamba ni serikali ‘yao’ na

maamuzi yake ni maamuzi ‘yao’. Lugha ya namna hii inaashiria kwamba uonevu au uporaji kwa makundi ya walio wachache unaofanywa na walio wengi ni jambo la kawaida, lenye uhalali kisheria, na kwamba siyo tena ukosefu wa maadili — kama ambavyo ingekuwa endapo kundi jingine lolote lingefanya hivyo.

## Inategemea nguvu za dola

Kwa jinsi yoyote ile maamuzi ya serikali iliyochaguliwa yanavyoweza kuwa mabaya, huwezi kuyakwepa. Maamuzi ya walio wengi hulazimishwa hata kwa wale wasiokubaliana nayo, kupitia kitisho cha faini, kifungo, kunyang’anywa leseni na vibali vya kufanya biashara, na adhabu nyingine nyingi. Na wala hakuna namna yoyote ya kuzikwepa: wananchi wa kawaida wananyimwa haki ya kutumia nguvu dhidi ya mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na serikali inayowanyonya.

Ni kweli kwamba ufikiaji wa maamuzi kidemokrasia husaidia kutatua tatizo la ‘kupe’. Kila mmoja hunufaika na huduma kwa umma kama vile ulinzi na usalama, hivyo inaonekana kuwa ni hitaji la haki kwa kila mmoja kuchangia gharama zake. Shida yake ni kwamba, wanasema wakosoaji, punde tunapokubali msingi kwamba serikali inaweza kuchukua fedha za watu, panakosekana mantinki ya kuweka kituo.

Kwa namna hiyohiyo, inaweza pia kudhaniwa ni jambo la maana kwa serikali kuwa na uwezo wa kudhibiti haki za mtu binafsi na haki za makundi ya watu inapotokea dharura — kwa mfano, kupeleleza au hata kukamata watu wanaotuhumiwa kupanga ugaidi. Hata hivyo, wanasema wakosoaji, pale serikali inapopewa nguvu ya ‘dharura’ panakosekana mipaka bayana ya matumizi yake. Na kama F. A. Hayek (1979) alivyoonesha, ‘Daima dharura zimekuwa kisingizio kinachopelekea mmomonyoko katika kuhakikisha usalama wa uhuru wa watu binafsi …’.

Kwa mfano, mgogoro wa kifedha wa mwaka 2007-8 ulipelekea serikali za nchi za Magharibi kuchukua usimamizi wa mabenki na kulazimisha kanuni nyingi za kisheria kwenye biashara nyingine za kifedha. Muongo mmoja tu baadaye, wakati wa janga la korona, hata nchi za kidemokrasia zenye mwelekeo wa hali ya juu sana wa kupendelea mabadiliko ziliamuru vizuizi vya kushangaza kwenye maisha ya watu (ikiwa ni pamoja na kuwafungia), pamoja na kufunga biashara (kama vile vyumba vya mazoezi, matukio ya michezo, urembo wa nywele na migahawa), kupiga marufuku mauzo ya bidhaa 'zisizokuwa na umuhimu wa lazima', na kupanua kwa kiasi kikubwa sana sekta ya umma. Mapema miaka ya 2020, watu wengi walikuwa radhi kukubali vizuizi kama hivyo kwa hiyari yao kwa dhamira ya kudhibiti virusi vya korona. Hata hivyo, kadri mwaka ulivyozidi kusogea na vizuizi kuendelea (au hata kuongezwa), hasira ya umma dhidi ya vikwazo hivyo ilizidi kuongezeka. Kisha wanasiasa walijikuta wanatumia nguvu za dola kuamuru udhibiti wa idadi kubwa ya wananchi ambao hawakuwa radhi tena kuendelea kuzuiwa na waliolalamika kwamba sasa walikuwa wanaishi chini ya 'utawala wa mabavu'.

Wakosoaji wanatoa hoja kwamba, endapo haki za watu binafsi zinaweza kuminywa kirahisi hivyo katika nchi nyingi za dunia hii zinazofuata demokrasia ya mabadiliko, basi tupo sahihi kuwa na hofu dhidi ya nguvu ambayo walio wengi katika uchaguzi wanaitoa kwa viongozi wetu wa kisiasa. Nguvu zozote zile tunazowapatia zinaweza pia kutumika dhidi yetu — kwa makusudi au bila kukusudia. Wanasiasa wanaweza kukosa uelewa umuhimu mkubwa sana wa ulinzi imara wa muda mrefu wa haki, na wanaweza kushindwa hata kutambua kwamba wanakiuka haki hizo. Na hata pale ambapo wanapotambua, wanakuwa bado wanakabiliwa na motisha zenye msukumo mkubwa wa muda mfupi za kujiongeza mamlaka yao hadi upeo.

Licha ya yote hayo, na kama ambavyo tumeona, nchi za kidemokrasia zimethibitisha kuwa na sifa ya uimara. Inaweza kukubalika kwamba vipindi vya kihistoria ambapo maadili ya

mwelekeo wa mabadiliko yalidumishwa serikalini ni vipindi vile ambapo ustaarabu uliongezeka kwa haraka sana — siyo tu kiuchumi bali katika sayansi, teknolojia, sanaa, elimu, fasihi na fani nyingine nyingi. Hayupo aliyekuwa radhi kuhatarisha hatua kama hizo za maendeleo. Mashaka makubwa ni kwamba tunazihatarisha kwa makosa.

## Inachochea uundaji wa serikali kubwa kupita kiasi

Waunga mkono wa demokrasia wanaamini kwamba haina upendeleo wa kisiasa — inafanya kazi vizuri kabisa kwa watu wanaopendelea serikali ndogo na halikadhalika kwa wale wanaopendelea zaidi uingiliaji kati wa serikali katika mambo ya kijamii na kiuchumi. Lakini tunaona kwa mara nyingine tena, demokrasia imesanifiwa hasa kwa ajili ya *ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja* — hoja yenye maana kubwa kwa wafuasi wa falsafa za Karl Marx kama mnadharia wa Poland, Rosa Luxemburg (1899) alivyoandika, ‘Demokrasia ni sharti la lazima la ujamaa’.

Ingawa wapenda mabadiliko hujaribu kuweka mipaka katika mawanda ya serikali, hakuna njia isiyoegemea upande wowote ya kuchagua ni maamuzi gani hasa  yanapaswa kufanywa kwa pamoja, na yapi yanapaswa kuachwa kwa watu binafsi. Na katika vitendo, demokrasia inaonekana kuwa kinyume na hali inayotarajiwa ya kutoegemea upande wowote kisiasa. Mapema katika miaka ya 1900,  serikali za kidemokrasia zilitumia kwa uchache kiasi cha zaidi ya asilimia 10 ya pato la taifa; lakini hadi mapema miaka ya 2000, kutumia asilimia 40 hadi 50 lilikuwa jambo la kawaida kabisa na hii inatoa picha ya ukubwa wa maamuzi ambayo kwa sasa yanafanywa kwa pamoja na siyo tena kwa watu binafsi kujiamulia wenyewe.

Kwa kipindi cha karne ya ishirini, huduma za pamoja zimetokea kutawala sehemu kubwa ya maisha — kuanzia ustawi wa jamii hadi huduma za afya, makazi, elimu, bima, uchukuzi, mahitaji muhimu, uzalishaji na mengine mengi. Pengine huko kutanuka kulipata uhalali wa kisheria kutokana na kutanuliwa kwa wigo wa haki ya kupiga kura katika chaguzi za umma, hasa kwa wanawake. Na kadri bajeti ya serikali ilivyozidi kuwa kubwa kufuatia vita kuu mbili za dunia, ndivyo makundi mengi zaidi yenye maslahi yalivyotafuta upendeleo mkubwa zaidi kutoka serikalini — jambo ambalo wanasiasa, katika uchu wao wa kupata kura, waliruhusu.

Misukumo hiyohiyo imedumu hadi leo hii. Dhamira ya wanasiasa ya kusaka kura, na kile kinachozingatiwa kuwa ni busara na uhalali wa kisheria wa chaguo la wengi, huchochea hata vyama vyenye kupendelea 'mabadiliko', vyenye kushikilia 'desturi za kale' au vyenye mtazamo wa 'soko huria' kupanua mchakato wa ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja kwa kina kirefu zaidi katika maeneo mengi ya kiuchumi, kijamii na kwenye maisha ya watu binafsi. Wanasiasa wanatafuta pia mvuto na kura kwa kushabikia miradi mikubwa ya serikali, inayovutia, lakini ambayo mara nyingi hutumia gharama kubwa na kupoteza fedha, mara nyingi pia ikitekelezwa kwa fedha ya mkopo, badala ya kutoa hoja zenye mashiko za usimamizi mzuri wa fedha. 'Aina yetu ya demokrasia ni rushwa, kwa kiwango cha juu kabisa', kama mwandishi wa Kimarekani, Gore Vidal, alivyosema katika kitabu cha *Armageddon* (1987). Na yote haya yanaweza kuzaa serikali kubwa zaidi kuliko vile ambavyo watu wengi wanataka.

## Ina gharama zilizojificha

Wakati ambapo manufaa ya mifumo ya kidemokrasia yanafahamika kirahisi, mara nyingi gharama zake za kifedha, kijamii na kimaadili huwa hazitiliwi maanani. Kinyume kabisa na

kuhimiza muafaka wa kijamii, wanasema wakosoaji, demokrasia kwa hakika inachochea tabia mbaya — kwa kuwa na vyama vya siasa vinavyopambana kama magenge kutafuta mvuto na ukuu, wanasiasa waliojikita kwenye uchaguzi unaofuatia badala ya kujikita katika kujenga mustakabali mwema wa muda mrefu wa taifa, na makundi yenye ushawishi ambayo bila kujali hutumia mfumo huo kujipata huduma maalumu kwa gharama za watu wengine.

Hivyo, wanaendelea wakosoaji, siyo jambo la kushangaza kuona kwamba demokrasia imetupatia serikali kubwa zaidi, inayogharimu zaidi na ambayo kwa kiasi kikubwa zaidi mamlaka yake yamelimbikizwa sehemu moja kwa kipindi cha karne moja iliyopita. Wanasiasa, wafanyabiashara na makundi mengine yenye maslahi; wote wana shauku ya kupanua sekta ya umma na kukamua zaidi uwezo au upendeleo kutoka katika sekta hiyo. Kadri makundi tofauti yanavyopiga kura ya kujipatia wao wenyewe manufaa zaidi na kuwabebesha gharama watu wengine, ikiwa ni pamoja na vizazi vya siku zijazo ambavyo havina nguvu ya kubisha, ndivyo ambavyo kodi na deni linavyopaa juu kwa kasi.

> Demokrasia ni mahali ambapo chaguzi nyingi za viongozi hufanyika, kwa gharama kubwa sana, bila ya kuzingatia masuala, na kupitia wagombea wanaoweza kubadilishana.
> –Gore Vidal (1991), *Mtazamo kutoka Klabu ya Diner*

Siyo rahisi kuzuia misukumo hii au kuliondoa tabaka la wanasiasa linayoidhibiti. Siasa ina *vizuizi virefu vya kuingia*, kama wachumi wasemavyo: ni vigumu kwa vyama vipya na vidogo zaidi to kutoboa njia ya kuingia serikalini, hasa katika mifumo ya upigaji wa kura ya ‘ushindi kwa wingi wowote wa kura’. Hivyo, kwa uchache kuna changamoto ya maana katika teuzi zinazoendelea kufanyika kwa upendeleo. Lakini kukua kwa harakati zinazotafuta kumfurahisha kila mtu kunaweza kuashiria kwamba hali hii inabadilika.

# 8. DEMOKRASIA IMETIWA CHUMVI?

‘Demokrasia’ imefaulu kuikaribia hadhi ya kufikirika ya kuonekana kama mletaji wa amani, ustawi, haki na uhuru. Hii ndiyo sababu viongozi ni hodari sana wa kutumia neno hilo katika serikali zao wenyewe, hata pale ambapo katika uhalisia ni uongozi wa mtu mmoja. Pia ndiyo sababu inayofanya watu wanaoishi katika nchi za demokrasia ya mabadiliko mara nyingi kutilia chumvi uwezo wa demokrasia. Tunahitaji kuchuja mambo yaliyokuzwa kupita kiasi na kuona ni kiasi gani uhalisia kinachostahiki.

## Demokrasia ni mfumo bora kabisa

Mara nyingi huwa inasemwa kwamba demokrasia ndiyo mfumo bora kabisa wa kisiasa — au kwa kipimo chochote, wenye unafuu kuliko yote. Kwa bahati mbaya, tungehitaji kwanza kujaribu mifumo mingine yote tunayoweza kuifikiria kwa ajili yakujua jambo hili kwa uhakika. Na hata ukirejea nyuma, ni viwango gani tunavyopaswa kutumia tunapohukumu mfumo wa kisiasa? Kwa mfano, demokrasia ni nzuri katika kuwahusisha wananchi katika mambo ya umma lakini inaweza kuwa mchakato wa taratibu sana na usio rahisi kufikia maamuzi wakati wa migogoro. Inaweza kupotoshwa, lakini inaonekana bora zaidi kuliko mifumo mingi katika upande wa kuinua kiwango cha ustawi, kushamiri na uhuru wa watu. Ukweli ni kwamba, utafiti uliofanywa na wachumi wa Kimarekani, Robert Sheriaon, Ryan Murphy na Benjamin Powell (2020) uligundua kwamba demokrasia ina uhusiano mkubwa sana na uhuru wa kiuchumi. Lakini kusema kwamba ndiyo mfumo ‘bora kabisa’ linabaki kuwa suala la maamuzi ya mtu binafsi.

Hakuna mtu anayejidanganya kwamba demokrasia ni kitu kisichokuwa na dosari au -kilichojaa hekima yote. Ukweli ni kwamba, demokrasia imesemekana kuwa ni aina mbovu kuliko zote ya serikali isipokuwa aina nyingine zote ambazo zimejaribiwa katika vipindi tofauti vya nyakati.
— Sir Winston Churchill (1947), *Hansard*, November 11

## Ni utawala wa watu

Mara nyingi demokrasia huitwa 'utawala wa watu'. Kusema hivi ni makosa. Katika nchi za demokrasia ya kisasa, watu hawatawali; wanachagua watawala wao. Hawafanyi maamuzi juu ya sheria; wawakilishi wao ndiyo huamua.

Zaidi ya hayo, 'watu' siyo mtu mmoja mwenye kufanya maamuzi bali ni mamilioni ya watu wenye mitazamo tofauti — na mara nyingi shindani — juu ya mambo ya umma. Hawakubaliani katika mambo mawili; kwanza katika mambo yanayopaswa kuwa malengo ya sera ya umma, na pili ni jinsi ya kufanikisha malengo hayo. Hawawezi na hawakubaliani juu ya namna ya 'kutawala'. Demokrasia haizai aina fulani yamuafaka wenye uadilifu na wenye kustahimilika: kinachokuwepo ni maoni ya kundi lolote lile linaloweza kukusanya kura zaidi kuliko makundi mengine. Wakosoaji wanasema kwamba, mchakato huu siyo 'utawala wa watu' bali umekaa zaidi kama genge la mapambano.

## Ni serikali itokanayo na ridhaa

Demokrasia inasemekana kuwa 'serikali itokanayo na ridhaa'. Kwa kiwango fulani kauli hii ni kweli. Lakini wakosoaji wanatoa hoja kwamba uhalisia wa demokrasia ni kwamba maamuzi ya kutunga sheria hufanywa na tabaka la kisiasa la watu wenye uwezo katika jamii. 'Ridhaa' pekee ya umma ni ridhaa adimu kutoka kwa walio wengi miongoni mwa watu wote, ambao huchukua hatua ya kwenda kupiga kura katika chaguzi za

viongozi ambazo kwa kawaida hufanyika kila baada ya miaka mingi kupita.

Aidha, huwezi kuambiwa kuwa umetoa 'ridhaa' endapo watu wengine ndiyo wanafanya maamuzi kwa niaba yako. Lakini hicho ndicho kitu kinachotokea katika demokrasia. Walio wengi huamua juu ya sera, na wengine wote hawana budi kuikubali la sivyo wakabiliane na adhabu kama vile faini au kifungo. Hata pale ambapo unapiga kura dhidi yao, walio wengi bado hutawala maisha yako na kuvamia mfuko wako wa fedha kama dikteta yeyote anavyofanya.

Na hata kile kinachozingatiwa kuwa ni 'ridhaa' ya wapiga kura hakina mantiki na wala haikitokani na taarifa kamili. Siyo tu kwamba wapiga kura ni mbumbumbu juu ya taarifa za kina za masuala yanayowahusu, bali hakuna pia mpiga kura anayeweza kutabiri matukio ya baadaye. Hivyo, hawawezi kubashiri kwa uhakika kamili jinsi ambavyo wagombea watafanya kazi, na wala hawawezi kuona athari pana zaidi (nzuri au mbaya) za sera zao kwa siku zijazo. Kwa maneno mengine, wanasema wakosoaji, kura zao hazina kabisa msingi wenye mantiki.

Bryan Caplan (2007) anatoa hoja kwamba mambo ni mabaya kupindukia. Wapiga kura, anasema, wana hisia potofu za upendeleo au chuki na wamepoteza mantiki *kutokana na mfumo*. Wanadhani mambo yanakuwa mabaya zaidi pale ambapo hayapo hivyo; Wanaamini kwamba kutengeneza ajira ni muhimu zaidi kuliko kutengeneza thamani; ni wabaguzi dhidi ya wageni kutoka nchi za nje na hufanya upendeleo wenye lengo la kulinda viwanda vya ndani; na wanayumbishwa kupita kiasi na matukio ya hivi karibuni lakini yasiyokuwa na maana, kama vile idadi ya medali ambazo nchi yao imepata katika mashindano ya Olimpiki. Ubaguzi wote huu huishia katika maamuzi ya kisera yasiyo na mantiki, yanayovuruga mambo na kusababisha madhara *kutokana na mfumo*.

## Kila mmoja ana kauli

Inadaiwa kwamba demokrasia ‘humpatia kila mmoja kauli sawa’ katika sera ya umma. Hata hivyo, siyo ‘kila mmoja’ anaruhusiwa kupiga kura. Katika kipindi kirefu cha historia, hata mataifa yenye kupendelea mabadiliko kwa kiwango cha juu sana yaliwanyima wanawake haki ya kupiga kura, pamoja na wanaume wasiokuwa na mali na waliotoka katika makundi ya kikabila ya walio wachache. Na watu wenye haki ya kupiga kura *wanaochagua* kutopiga kura — mara nyingi huwa ni nusu au zaidi ya watu wote katika nchi — hawana kauli kabisa katika matokeo. Lakini tunaona tena, hata pale unapopiga kura, nafasi ya kura yako kuamua kwa hakika matokeo ya uchaguzi katika nchi kubwa ni moja ya makumi (au hata mamia) ya mamilioni.

> Demokrasia ni nadharia ambayo watu wa kawaida wanajua kitu gani wanataka na wanastahili kukipata kwa njia yoyote ile.
> — H. L. Mencken (1915) *KurasaChache za Notisi*

Na wala kura za watu hazipewi uzito ulio sawa. Kura za watu wanaoishi katika wilaya ‘salama’ za upigaji wa kura — kule ambapo mara zote chama kilekile hushinda — zinapewa uzito wa kiwango cha chini kuliko kura za watu wanaotoka katika eneo la ‘mchanganyiko’. Na kutokana na sababu zinazoeleweka za kidemografia, baadhi wilaya za upigaji wa kura zinaweza kuwa na watu wengi zaidi wenye haki ya kupiga kura kuliko maeneo mengine. Hivyo, endapo kila wilaya huchagua mwakilishi mmoja tu, kura za watu wanaonaishi katika wilaya ndogo zaidi zinakuwa na uzito mkubwa zaidi.

Hata hivyo, uwakilishi unaweza kuwa wa hila kwa sababu za kisiasa pia. Kwa mfano, Urusi ya Kisovieti uwakilishi uliofikia mara tano zaidi kwa wakazi wa mjini, katika jitihada za makusudi za za kuwashinda waiopenda mabadiliko wa mashambani mara baada ya kuundwa kwake. Wanasiasa wa Kimarekani nao pia walikuwa na historia ndefu ya kuunda wilaya za upigaji wa kura

zenye maumbo ya ajabu kwa ajili ya kufanya ziwe ‘salama’ kwa wenzao waliokuwa madarakani. (Ramani ya wilaya mojawapo kama hiyo, iliyotengenezwa mwaka 1812 chini ya Gavana wa Massachusetts aliyeitwa Elbridge Gerry, iliishia kuonekana kama sura ya mjusi)

## Demokrasia inachochea usawa

Mifumo ya kidemokrasia mara nyingi husifiwa kwa kutetea usawa katika medani ya siasa (au ‘usawa wa raia’) na utu wa watu. Lakini mifumo mingine inaweza pia kuwa na usawa katika medani ya siasa; na tunaweza bado kuheshimu utu wa watu hata pale ambapo hatuwaruhusu kupiga kura.

Pia inadaiwa kwamba ushiriki wa kidemokrasia unachochea kujithamini na kujikubali. Hata hivyo, ingekuwa kitu cha ajabu kuunda mfumo wa upigaji wa kura kwa ajili ya malengo haya mahsusi. Tungeweza kuwanyima haki ya kupiga kura wafungwa wanaojitenga katika katika tumaini la kupandisha juu hali zao za kujithamini, kwa mfano. Na kuna njia bora zaidi za kuinua kiwango cha kujithamini na kujikubali kuliko chaguzi za viongozi.

Kwa namna hiyohiyo, demokrasia inasemekana kuzaa hali ya kutenda haki na usawa, na kuzuia masuala ya kisiasa na kijamii kuhodhiwa na vikundi vidogo vya watu. Hata hivyo, kuna kila sababu kuamini kwamba makundi ya watu wenye maisha mazuri zaidi bado yana ushawishi usiolingana na wengine. Mawaziri wakubwa na maofisa wa serikali wana kawaida ya kuwa matajiri zaidi kuliko wastani, na ndani ya tabaka hili kuna wahitimu wengi zaidi kutoka mashule na vyuo vikuu vyenye kutoza ada kubwa. Pia, watu wa tabaka la kati ndiyo hakika wanaoonekana kunufaika zaidi kuliko maskini katika huduma za umma, kama vile kiinua mgongo, mashule na huduma za afya; lakini tena, ndiyo wanaotawala mdahalo wa kisiasa, jambo linalowasaidia

kuhakikisha kwamba maamuzi ya kisiasa yanafanyika kwa kuwapendelea. Ushawishi wao unaweza kuwa moja ya sababu kwanini katika nchi nyingi, sekta ya umma imekua kubwa sana — kubwa zaidi kuliko vile ambavyo ingehitajika endapo lengo lake la pekee lilikuwa ni kutoa fedha na huduma kwa kiasi cha watu wachache.

## Demokrasia huleta hisia ya jumuiya

Hoja nyingine ni kwamba demokrasia huleta ‘hisia ya jumuiya’ na huzalisha ‘muafaka’. Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa zaidi kwa hisia ya mtu kuwa sehemu ya jumuiya fulani kupatikana kupitia ushiriki wa watu katika vilabu vya uanachama, vyama vya kujitolea, makundi ya makanisa ya kuungana mkono na taasisi nyingine zote katika *asasi za kiraia*. Na wakati serikali ya uwakilishi iliyochaguliwa na watu inaposaidia katika kufanya maamuzi ya pamoja kwa amani, huwa ni vigumu kufikia muafaka wa pamoja. Midahalo katika chaguzi za viongozi na bungeni huwa ni mashindano baina ya makundi tofauti na yenye maslahi yanayopingana. Inaweza kuwa midahalo mikali sana kwa kuwa washindi huwa na nguvu ya kulazimisha mtazamo wao kwa walioshindwa.

Katika masoko ya kiuchumi, watu kuchagua bidhaa na huduma kwa ajili yao wenyewe, siyo kwa ajili ya watu wengine. Watu tofauti wanaweza kufanya chaguzi binafsi zozote zile wanazopenda — bidhaa za Apple au Android, chai au kahawa, nyekundu au bluu — na bila ya chaguzi zao kufanya mabadiliko yoyote kwenye chaguzi za wengine. Chaguzi za kisiasa, hata hivyo, hufanywa kwa ajili ya kila mmoja. Pale walio wengi wanapochagua idadi fulani ya wagombea, kila mmoja hana budi kukubali matokeo. Pale chama kinachotawala kinapoamua juu ya sera fulani — tuseme — kujenga barabara mpya au uwanja wa ndege, kila mmoja hana budi kukubaliana nayo, ikiwa ni pamoja

na wale ambao makazi na njia zao za kujipatia riziki vitabomolewa katika mchakato huo.

Asili ya ulazima wa maamuzi ya kisiasa, na kigezo kwamba makundi ya walio wengi yana wigo mpana wa kuweza kufanya maamuzi kuhusiana na mambo mengi sana, inamaanisha kwamba chaguzi za watu wengine zinaweza kuwa na athari kubwa sana katika maisha yako na ustawi wako mwenyewe. Kama mwanafalsafa wa Kimarekani, Jason Brennan (2016) anavyodokeza katika kitabu *Dhidi ya Demokrasia*, siasa hugeuza jirani zako kuwa watu wenye uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa adui, kuliko rafiki. Hiki ni kinyume kabisa cha 'hisia ya jumuiya'.

## Demokrasia hutulinda dhidi ya watawala wabaya

Katika kipindi kirefu cha historia ya mwanadamu, maisha yetu yalikuwa chini ya utawala wa mtu mmoja mwenye nguvu zote — mabwana wa vita, watawala wa kifalme, watawala wakuu, machifu, watu wa tabaka la juu, makabaila, walinzi wa himaya, madikteta na wengine. Mara nyingi, hawa watawala walikuwa na madaraka juu ya kuishi na kufa kwetu. Kwa hakika, mifumo ya kidemokrasia inaweza kufanya iwe vigumu zaidi kwa viongozi kujilimbikizia madaraka au kutumia madaraka hayo kufanya maovu na kiholela. Lakini wanasiasa na maofisa wa serikali bado wana maslahi binafsi ya kwao wenyewe — kwa mfano kupandisha juu hadhi na mishahara yao wenyewe, au kuchepusha fedha za umma kwa watu wanaowaunga mkono. Mchakato wa kidemokrasia huwapa madaraka na uhalali wa kisheria unaoonekana wazi wa kujiingiza katika maslahi hayo, hata pale ambapo maslahi ya watu wengine yanadhurika katikamchakato huo. Ni mchakato unaoweza hata kukaribisha watawala wabaya, kuliko kutukinga dhidi yao.

Na wala hatuwezi mara zote kutegemea utoaji wa kidemokrasia wa haki kutuokoa. Unaweza kutuhifadhi dhidi ya matendo maovu na holela ya viongozi wetu, lakini kama kama ukiritimba mwingine wowote, unaweza kuwa mchakato wa taratibu sana na ghali. Na kwa vile ni sehemu ya serikali, mfumo wa kusimamia haki unaweza kupindishwa ili kutumikia maslahi ya watu wenye amri katika mamlaka. Hatimaye, njia ya uhakika kuliko zote ya kulinda usalama wa maisha yetu, mali, uhuru wa kujieleza na haki nyingine za msingi siyo demokrasia au mahakama za kisheria, bali ni nguvu ya umma wenye kuthamini maadili ya kimabadiliko. Ili demokrasia iweze kudumisha haki zetu na kutuletea sisi sote manufaa yake ya juu kabisa, ni jambo lenye umuhimu wa lazima kwa wapenda mabadiliko na waumini wa demokrasia kutangaza maadili hayo na kuhamasisha thamani yake kwa umma. Na sharti tuendelee kwa uhodari, pia kuwa macho na dosari zinazopatikana ndani ya mchakato wenyewe wa ufikiaji wa maamuzi ya kidemokrasia.

# 9. JINSI MAAMUZI YA KIDEMOKRASIA YANAVYOFIKIWA

Kansela wa Ujerumani wa karne ya kumi na tisaa, Otto von Bismarck, anadhaniwa wakati fulani aliwahi kusema kwamba endapo unapenda sheria au mkate wa nyama, hupaswi kamwe kushuhudia maandalizi ya chochote kati ya vitu hivyo. Na hakika kuna sababu nzuri ya kuwa na mashaka kuhusiana na namna ambavyo nchi za kidemokrasia hufikia maamuzi yake. Demokrasia inatarajiwa kutafsiri maoni ya watu wengi na kuyaingiza katika mkusanyo mmoja wa maamuzi ya pamoja. Lakini tunahitaji kuwa macho na mahali, namna na sababu za mchakato huu kuwa wa kiwango cha chini zaidi ya kitu kisichokuwa na dosari.

## Chaguzi za viongozi

Chaguzi za viongozi, kwa mfano, zina mipaka dhahiri kama mbinu za kuchagua baina ya wagombea au sera. Kwa kuanzia, hazifanyiki mara kwa mara — nyakati fulani kila baada ya miaka minne au mitano tu, au miaka zaidi. (Kinyume chake, katika soko la kibiashara, tunaweza kuchagua bidhaa za upendeleo wetu katika saa yoyote ya siku.) Uchaguzi ambao chaguzi za viongozi hutoa kwa wapiga kura nao pia una ukomo mkali. Idadi kubwa sana ya masuala anuwai na mazito yanayohusu umma hupelekwa kwa wapiga kura kama vifurushi, na pengine huwasilishwa na wagombea wawili au watatu tu. (Kwa mara nyingine tena tunaona, soko hutupatia chaguzi kutoka kwenye wigo mpana wa bidhaa, siyo vifurushi vichache tu.) Kisha, maamuzi ya walio wengi hulazimishwa kwa kila mmoja.

Pia kuna fumbo kama ilivyo katika mchezo wa ‘mwamba, karatasi na mkasi’. Wapiga kura wanaweza kumpendelea mgombea mmoja dhidi ya mgombea wa pili (kama vile karatasi dhidi ya mwamba) na huyo mgombea wa pili dhidi ya mgombea wa tatu (kama vile mwamba dhidi ya mkasi); lakini tena, wanaweza kabisa kumpendelea mgombea wa tatu (mkasi) kuliko mgombea wa kwanza (karatasi). Kwa sababu ya hali kama hii, utaratibu unaotumika kumpata mshindi wa kura unaweza kupelekea tofauti kubwa katika matokeo. Kwa mfano, nchini Ufaransa na katika nchi nyingine ambapo wagombea wanaoongoza katika duru za awali za upigaji wa kura huenda katika kura ya mwisho ya marudio, ni jambo lililozoeleka kwa mgombea kuwatangulia wengine katika duru ya kwanza lakini kushindwa vibaya sana katika duru ya pili ya uchaguzi baina ya wagombea wawili walioongoza.

## Watu wenye haki ya kupiga kura

Watu wenye haki ya kupiga kura wana mlolongo mrefu wa dhamira tofauti. Wanaweza kuwa ni wafuasi wa maisha wa chama fulani mahsusi, bila ya kujali hoja yoyote ile. Wanaweza kuwa na dhamira ya kutaka tu kusabaisha usumbufu kwa chama kinachotawala. Au wanaweza kupiga kura kwa dhamira pekee itokanayo na mambo binafsi au yanayohusu eneo lao, kama vile kufungwa kwa hospitali iliyokuwa karibu. Huenda hata wasipige kura kwa ajili ya kitu hasa wanachokitaka, lakini wakampigia kura mgombea wasiyempenda, kama mpango maalumu wa kumwondoa mgombea mwingine wasiyempenda zaidi. Au wanaweza kukanganyikiwa kabisa kuhusiana na masuala yao lakini bado wakajihisi kuwa na dhima ya kupiga kura. (Kuna idadi ya kushangaza ya wapiga kura wanaokuwa bado hawajaamua wamchague nani hadi wanapokuwa katika kibanda cha kupigia kura wakiwa na karatasi ya kura mbele yao.)

Chaguzi za viongozi siyo michakato inayotoa mfano bora au yenye mantiki, kwamba wapiga kura waliofanya tafakari ya kina, walio na taarifa kamili na wasio na upendeleo, ndiyo wanaofuatilia masuala kwa uangalifu na kupiga kura kwa ajili ya kile wanachoona kuwa ni bora kabisa kwa manufaa ya muda mrefu ya nchi kwa ujumla wake.

## Wagombea

Hata mwanasiasa anayesukumwa kwa kiwango cha juu sana kutumikia maslahi ya umma analazimika kutafuta kura ili apate uongozi na kufanikisha chochote. Kwa maana hiyo hii 'dhamira ya kusaka kura' ni kichocheo kikubwa kwao, jambo ambalo kwa mara nyingine tena huvuruga mchakato wa ufikiaji wa maamuzi.

Kwa mfano, wanasiasa wana kawaida ya kujikita kwa wapiga kura 'wenye msimamo wa kati'. Ni wazi kwamba, kuna idadi kuwa zaidi ya watu miongoni mwa wapiga kura wenye misimamo ya kati kisiasa kuliko miongoni mwa wale wenye misimamo mikali, na kuna uwezekano mkubwa zaidi wakashawishika kubadili mitazamo yao kuliko wale wenye misimamo mikali. Lakini pale wagombea na vyama vyao vyote wanapojiweka katikati, wanawanyima wapiga kura uchaguzi wa kweli — hasa wale wapiga kura wenye mitazamo imara isiyoning'inia katikati.

Pia wanasiasa hujikita kwa ukaribu zaidi katika makundi yenye ushawishi, ambayo yanaweza kuwasaidia kuvuna idadi kubwa ya kura kwa sababu ya motisha na miundombinu yao imara — hasa pale yanapoungana kwa pamoja na makundi mengine tena yenye maslahi. Ni 'walio wengi ambao wamepumbazwa' ndio watakaokuja kulipa gharama — lakini hao 'walio wengi ambao wamepumbazwa' wana sauti ndogo.

## Wabunge au wawakilishi

Kwa hiyo wawakilishi wanaochaguliwa kupitia mchakato huu bila shaka yoyote ni waangalizi wasio na upendeleo wa maslahi ya umma. Wanalegeza msimamo hata kabla ya kushinda viti vyao. Wana deni la kulipa kwa makundi yenye maslahi ambayo yanawaunga mkono na deni kwa wakuu wa chama cha kisiasa kinachowapatia chapa ya uchaguzi.

Zoezi la kupitisha sera zao bungeni ni mchakato usiotokana na msingi wa kanuni za maadili pia. Ni mchakato unaoweza kuwasukuma kujihusisha katika utaratibu wa *nipe nikupe*: biashara inayoitwa 'unapiga kura kuunga mkono sera yangu na mimi nitapiga kura kuunga mkono sera yako'. Kwa mfano, mwakilishi mmoja anaweza kupiga kura kuunga mkono pendekezo la mwakilishi mwingine la kujenga shule au hospitali mpya katika wilaya yake, siyo kwa sababu yoyote ya kuamini kwamba inastahili, bali ni katika tumaini kwamba huyo mwakilishi mwingine atamlipa kwa upendeleo katika siku zijazo.

Vivyo hivyo, mapendekezo mengi ya sheria mpya yanaweza kuhusisha bajeti kubwa ili kupata uungwaji mkono unaohitajika sana bungeni. Ndiyo maana, mapema katika miaka ya 1950, Rais wa Marekani Dwight D. Eisenhower alisanifu mpango wake wa barabara kuu zinazounganisha majimbo ili kuyanufaisha majimbo yaliyo mengi. Kufuatia kila mmoja kupigia kura barabara nzuri zaidi jimboni kwake mwenyewe, maseneta na wawakilishi walijikuta wakipiga kura kuchagua mtandao mzima wa barabara, bila kujali kama walifikiri lilikuwa ni wazo jema. Na sheria ya dharura ya mwaka 2008 iliyotungwa kuokoa mabenki ya Marekani yaliyokuwa taabani ilikuwa na kurasa mbili tu mwanzoni ilipowasilishwa Bungeni. Lakini kwa kuwa kila mmoja alijua kwamba sheria hiyo *ilitakiwa* kupitishwa, wawakilishi walidai kila aina ya upendeleo kama malipo ya uungaji mkono. Sheria iliishia kuwa na kurasa 451, ikiwa imesheheni upendeleo kama vile misamaha ya kodi kwa viwanda vya nguo, pombe kali,

vyombo vya uvuvi, viwanja vya mashindano ya mbio za magari na hata watengenezaji mishale ya miti.

> Wanaofanya kazi ya siasa na watunga sera hutumia motisha zinazotolewa na washawishi wa wanasiasa na makundi yanayotoa shinikizo kwa serikali kusukuma mbele bila huruma ukubwa wa shughuli za serikali. Ni lini, katika kumbukumbu zilizopo, kumewahi kuwa na mchakato wa maana wa kufuta sheria zilizopitishwa?
> — Craig Smith na Tom Miers (2011), *Demokrasia na Kuanguka kwa Nchi za Magharibi*

## Maofisa wa serikali

Maofisa wa serikali wenye jukumu la kusimamia utungaji wa sheria zote hizi siyo malaika hata kidogo, wenye kuwajali wengine kuliko wao wenyewe. Wanaweza kujitwika ufahari wa kuwa watumishi wa umma, lakini bado wana maslahi binafsi ya kwao wenyewe. Kwa mfano, endapo wanaweza kupanua taasisi zao wenyewe, basi bajeti, mishahara, hadhi, usalama wa ajira zao na madaraja ya vyeo; vyote vinaweza kuboreshwa.

Na wanaweza kutumikia maslahi yao wenyewe katika njia nyingine. Kwa mfano, sheria zina maana pana katika utekelezaji wake, na mara nyingi zinahitaji maofisa wa serikali kama vile mamlaka za udhibiti kuamua ni kanuni hasa gani zinapaswa kuwekwa na jinsi gani kanuni hizo zinapaswa kutafsiriwa na kutekelezwa. Kufuatia ukweli kuwa maofisa hawa ni wataalamu katika maeneo yao wenyewe ya kiserikali (pengine ni wataalamu zaidi kuliko wanasiasa wanaopitisha sheria), wanaweza kirahisi kuongeza ugumu wa tafsiri ya sheria — jambo linalohitaji tena maofisa zaidi wa serikali kulisimamia.

Wanaweza pia kujiachia wao wenyewe uwezo mkubwa sana wa kuamua jinsi sheria zinavyofanya kazi. Jambo hili kwa upande wake huwapa hadhi na heshima kwa sababu inafanya wafanyabiashara na umma kuwa tegemezi wa tafsiri yao ya

kanuni au uwezo wao wa kuamua nani anapaswa kupewa mikataba, ufadhili au leseni. Nyakati fulani wanaweza hata kuwa na uwezo wa kujipatia hongo au upendeleo kutokana na maamuzi yao.

## Wategemezi wa siasa

Vyombo vya habari, makundi yenye ushawishi, washauri mabingwa, na wale ambao hutegemea matumizi ya serikali; wote wana shauku ya kudumisha na kupanua mchakato wa ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja.

Kwa mfano, watangazaji wanahitaji kujaza mzunguko wao wa habari wa masaa 24 unaohitaji uangalifu mkubwa. Bahati nzuri kwao ni kwamba, wanasiasa wapo tayari kufanya lolote ili kutoa mitazamo yao na ‘kumwaga’ sera zao. Vyombo vya habari pia vinanataka ‘kuwa wa kwanza’ kutoa habari kabla ya wengine — tunaona kwa mara nyingine tena, wanasiasa kutoka serikalini wanavifanyia hisani vyombo vya habari kwa ‘kuvujisha’ sera mapema kabla ya tangazo lolote rasmi, ili umma upate kusikia upande wao wa shilingi hata kabla ya wapinzani wao kujua kitu gani kinatokea.

Washauri mabingwa na makundi ya kampeni wanaweza kujionesha wao wenyewe kama wataalamu na kujidai kuwa hawana upendeleo, lakini nao pia huleta maslahi yao wenyewe katika mdahalo. Makundi ya kampeni, yaliyojikita kwa kiasi kikubwa kwenye jambo fulani la msingi, yana uwezekano mkubwa zaidi wa kutoa wito wa matumizi zaidi ya umma au punguzo la kodi kwa ajili ya jambo hilo, bila ya kufikiri sana kuhusu athari zake kwa walipakodi kwa ujumla zaidi.

Mwisho, kuna watu binafsi ambao ni tegemezi kwa serikali. Waajiriwa wa serikali ni kundi kubwa la wapiga kura, kundi

ambalo halina uwezekano wa kuchagua serikali ndogo zaidi yenye kiwango cha chini cha urasimu. Lakini kuna mamilioni wengine, kama vile wanufaika wa kiinua mgongo na ustawi wa jamii, na wale wanaofanya ugavi katika vyombo vya serikali. Katika baadhi ya nchi zilizopiga hatua, idadi ya watu wanaoitegemea serikali kwa nusu au zaidi kipato chao ndiyo walio wengi miongoni mwa watu wote katika nchi. Maslahi yao ni kupanua ukubwa wa serikali; siyo kuokoa fedha za walipakodi.

## Hitimisho

Demokrasia ni mfumo bora zaidi katika njia nyingi kuliko mingine, kama mifumo ya serikali ya utawala wa mtu mmoja, lakini tunapaswa kuwa makini na mfumo huo. Pale tunapoongelea 'demokrasia' na ufikiaji wa maamuzi kidemokrasia, kwa hakika tunaongelea siasa na ufikiaji wa maamuzi kisiasa. Na kama ambavyo watu wengi wataafiki, mchakato wa kisiasa ni tofauti kabisa na kitu kisichokuwa na dosari.

Kwa hiyo, ili kujihakikishia manufaa makubwa kabisa ya demokrasia, ni lazima tubakie katika uhalisia wa namna ambavyo mfumo huu unafanya kazi kwa hakika. Tunapaswa kuwa macho na dosari zake, na pale inapowezekana, kufanya jaribio la kusahihisha au kupunguza ukali wa dosari hizo. Tukifanikiwa, matunda yake yanaweza kuwa makubwa.

# 10. SHINIKIZO JUU YA DEMOKRASIA

Ingawa karibia kila mmoja anadai kupendezwa na dhana ya demokrasia, watu wengi wamekuwa na mashaka makubwa zaidi kuhusu utendaji wake halisi. Wanapenda demokrasia lakini hawapendi siasa. Wanaona demokrasia kama njia ya haki inayomshirikisha kila mmoja, inayoruhusu mdahalo wa wazi wa masuala yanayohusu umma, na kuishia katika kile kinachochukuliwa kuwa ni utekelezaji wa sera zilizokubaliwa kwa amani na bila upendeleo. Hata hivyo, wanaona siasa na wanasiasa kama ndumilakuwili, wanaojitumikia wao wenyewe na maslahi yao binafsi. Katika kura za maoni zinazoonesha imani ya umma kwa watu wa fani tofauti, wanasiasa hujikuta wakiwa mkiani, au karibu na mwisho.

Hii yote siyo dosari ya wanasiasa wenyewe. Siyo rahisi kwao kutafsiri mitazamo anuwai ya mamilioni ya watu na kuiweka katika sera moja ambayo kila mmoja anaweza kuiunga mkono. Na hata kufanya hivyo ni vigumu zaidi leo hii, pale ambapo safari na uhamiaji vimefanya makundi mengi ya watu katika nchi kuwa katika mchanganyiko ulio tofauti zaidi. Wanasiasa pia wana mitazamo imara lakini inayopingana, kitu kinachopelekea kutoa hoja nzito sana — na kufanya umma ufikiri kwamba wana shauku kubwa zaidi kupata alama za ushindi kuliko kufanya mambo ya msingi. Ili kufikia makubaliano yoyote yale, mara nyingi inawalazimu kulegeza msimamo — kitu kinachowafanya waonekane kukiuka zaidi hata msingi wa kanuni za maadili.

Jambo hili siyo kitu cha pekee kwa demokrasia au kitu ambacho ni kibaya zaidi katika nchi za kidemokrasia. Kinyume chake, demokrasia inaweza kuchochea ukweli na uwazi katika mdahalo wa umma. Wanasiasa kutoka nchi zenye mwelekeo wa demokrasia ya mabadiliko wanaweza kwa ujumla wao kuaminika na kushiriki kwa kiwango cha chini katika rushwa ukilinganisha

na wale wanaotoka katika mifumo mingine. Kwa mfano, kati ya nchi kumi na tano zinazochukuliwa kuwa na kiwango cha chini cha rushwa, kwa mujibu wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Berlin – Transparency International (2019), kumi na nne zinahesabiwa na Kitengo cha Intelejensia ya Kiuchumi (2019) kama 'nchi kamili za kidemokrasia'. (Mfano wa peke yake ni Singapore, ambayo inahesabiwa kama 'nchi ya kidemokrasia yenye dosari'.)

## Kukataliwa kwa siasa za wenye nguvu na ushawishi

Kwa maneno mengine, wanasiasa katika nchi za kidemokrasia wanaweza kwa kiasi fulani kukwepa lawama; lakini bado, katika nchi za kidemokrasia, matendo yao yanaonekana wazi zaidi katika jicho la umma na pia wazi zaidi kwa wakosoaji. Jambo hili kwa upande wake linaweza kuwa ndiyo sababu ya nchi hizi kukosolewa zaidi.

Katika nchi nyingi, ukosoaji wa umma dhidi ya wanasiasa umepelekea kushuka kwa idadi ya watu wanaojitokeza katika chaguzi za viongozi na kukua kwa uungaji mkono wa kile kinachoitwa harakati 'zinazotafuta kumfurahisha kila mtu' na vyama ambavyo kwa upande wake vinafurahi kuchangamkia hali hii ya kuvunjika moyo kupitia wanasiasa wanaokubalika na watu wengi. Viongozi wanaotafuta kumfurahisha kila mtu hujichukulia wao wenyewe kama waumini wa kweli wa demokrasia, wanaolinda maslahi ya halaiki ya watu wa kawaida wasiowakilishwa. Wanaweza kushawishi watu kwa kutumia utata wa masuala kama vile uhamiaji au ustawi — lakini utaona tena, watu wana muda kidogo sana wa kutafakari mambo kama hayo yenye utata.

## Mazingira katika dunia inayobadilika

Migogoro ya kiuchumi nayo pia imechochea umma kutoridhishwa na siasa za kidemokrasia. Mara nyingi sana hutokea kwa demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko kuhusishwa na ukuaji wa kiuchumi: kama Acemoglu na Robinson (2012) walivyogundua, mafanikio ya kiuchumi hupatikana kupitia uwapo wa taasisi sahihi za kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, mdororo wa kiuchumi katika Nchi za Magharibi baada ya mgogoro wa kifedha wa mwaka 2007-8, kuporomoka kwa uchumi kutokana na janga la korona mwaka 2020 , na uwezo duni ulioonekana wazi wa wanasiasa katika kushughulikia migogoro hii, vinaweza kuwa vimedhoofisha imani ya umma katika demokrasia.

Sababu nyingine ya kupelekea hali ya kutoridhika inaweza kuwa kwamba baadhi ya masuala ya kiulimwengu yamekua makubwa mno kupita uwezo wa siasa za kitaifa kuweza kuyadhibiti au kuamua. Mabadiliko ya tabia-nchi ni suala mojawapo: watu wanalalamika kwamba kitendo cha kupigia kura azimio la kupunguza uzalishaji wa gesi ya kaboni katika nchi zao wenyewe hakina maana hadi pale nchi nyingine zitakapofanya hivyo pia. Usalama, ugaidi na uhamiaji yanaweza pia kuhitaji utatuzi unaoratibiwa kimataifa.

Vyombo vya kimataifa hujaribu kuziba pengo lililopo katika masuala haya ya kiulimwengu — Umoja wa Ulaya ukiongoza katika sera ya mazingira, benki kuu zikijaribu kuthibiti mtikisiko wa kiuchumi, halikadhalika na mahakama za kimataifa pia. Lakini vyombo vya kimataifa kama hivyo vina mipaka mikali. Vinakosa utambulisho wa kitamaduni na lugha, vitu ambavyo wapiga kura wanaweza kujioanisha navyo, na mataifa yanayounda vyombo hivyo yanaweza kupingana vikali sana katika mambo mawili; malengo na mbinu. Kwa hiyo watu huvichukulia vyombo hivi kama taasisi zilizojitenga mbali na zisizowajibika kwao, na badala yake hutoa wito wa uthubutu zaidi wa kitaifa — jambo ambalo

viongozi wanaotafuta kumfurahisha kila mtu kwa mara nyingine tena hupenda sana kulichangamkia.

## Mabadiliko katika mfumo wa kisiasa

Changamoto nyingine ni kwamba kuongezeka kwa ukubwa na ugumu wa tafsiri ya maamuzi ambayo sasa yanafanywa kupitia mchakato wa kisiasa umefanya siasa kuwa shughuli ya watu wenye fani ya siasa. Mara nyingi wananchi wa kawaida wanahisi kuwa wana jukumu dogo. Ni wachache sana wanaofanya chochote zaidi ya kupiga kura. Ni sehemu ndogo ya walio wachache ndiyo wanaojiunga na vyama au makundi ya kampeni. Kutokana na vyama kupoteza wanachama, vimekuwa tegemezi zaidi kwenye kampeni za hila, haiba za watu binafsi, vipande vifupi vya sauti iliyorekodiwa na kubahatisha — kitu kinachofanya wapiga kura kushuku kwamba wamefanyiwa ghiliba.

Teknolojia ya kisasa ya vyombo vya habari inaweza kusaidia wanasiasa kuonekana wazi zaidi, lakini kwa kiasi kikubwa imekazia zaidi jicho lake kwa viongozi wa chama kuliko wawakilishi wa kawaida. Ni mawaziri na mawaziri wakuu ambao ndiyo huonekana kwenye midahalo ya televisheni, wakilenga kuinua juuhadhi na mamlaka yao na kuongeza udhibiti wao wa vyama vyao. Jambo hili linahamishia nguvu katika mhimili serikali na kuiondoa katika mikono ya wawakilishi wanaotarajiwa kuidhibiti.

Wakati huo huo gharama inayoongezeka ya chaguzi za viongozi hufanya fedha kuwa muhimu zaidi, jambo linalopelekea umma kuhoji ni nani anayelipa gharama za siasa zao. Wanapiga kura kuwaondoa wanasiasa, kitendo kinachoishia kwa wanasiasa hao kupata kazi zenye marupurupu mazuri katika kampuni inayotaka kuchota maarifa yao ya ndani ya kisiasa na mfumo wa udhibiti.

Hii inapalilia kikamilifu dhana ya kwamba wanasiasa wapo tu kwa ajili yao wenyewe. Kwa mara nyingine tena, hili siyo jambo la pekee kwa demokrasia; huonekana kwa wazi zaidi chini ya mfumo huu.

Wingi na ugumu wa masuala yaserikali pia vina maana ya kwamba maamuzi zaidi na zaidi hufanywa na maofisa na ‘wataalamu’ wa serikali kuliko kufanywa wawakilishi wa kuchaguliwa. Ni nadra kwa wanasiasa kupata muda wa kusoma na kuelewa sheria zote ambazo siyo rahisi kuzitafsiri, wanazopelekewa kwa ajili ya kuzipitisha. Ukweli ni kwamba, nyingi kati ya sheria zinazopitishwa katika nchi za demokrasia ya kisasa huandikwa na watumishi wa umma na siyo rahisi hata kidogo kutafsiri maana zake kiasi kwamba bado wanahitajika wataalamu wengine kuzitafsiri na mawakala wa kusimamia utekelezaji wake. Hivyo, tunaona kwa mara nyingine tena wanasiasa wanapoteza nguvu. Na mengi kati ya majopo ya utaalamu yanayoundwa kufanya mapitio ya sheria huchaguliwa kutoka tabaka la watu wenye uwezo katika jamii ya wanataaluma, majaji au watumishi wa umma walio mbali zaidi na umma kuliko hata wanasiasa wenyewe.

## Mabadiliko miongoni mwa watu wenye sifa ya kupiga kura

Watu wenye sifa ya kupiga kura nao wamebadilika pia. Kufuatia kuongezeka kwa utajiri, wigo mpana zaidi wa elimu na urahisi mkubwa sana kwa watu kusafiri, vizuizi vya ubaguzi wa matabaka vimepungua sana. Ni rahisi zaidi kwa watu kutoka familia maskini kutumia vipaji vyao, kuwa matajiri na hata maarufu, na kutikisa desturi zilizopo za kiuchumi na kisiasa. Lakini tunaona tena, watu katika uchumi unaoporomoka hutokea kuhisi kuwa hawathaminiwi na wala hawashirikishwi, jambo

linalokuza utambulisho wa kitaifa na kutafuta kumfurahisha kila mmoja.

Teknolojia nayo pia imebadilisha siasa. Kwa mfano, watu wengi zaidi sasa wanapata habari kutoka katika vyanzo vya mtandao wa intaneti. Mitandao ya kijamii hufanya hali kuwa rahisi zaidi kwa makundi ya walio wachache kukutana na wengine wenye mtazamo kama wao — na kuungana mkono baina yao, bila ya kuwahitaji wanasiasa. Na huduma nyingi (kwa mfano, utangazaji, mahitaji muhimu, simu na uchukuzi) ambazo wakati fulani zingeweza tu kutolewa na mashirika makubwa ya umma yaliyokuwa chini ya udhibiti wa wanasiasa zinaweza sasa kutolewa na makampuni madogo zaidi ya watu binafsi kwa njia mpya tofauti na shindani. Siyo tu kwamba jambo hili hushusha kiwango cha umuhimu wa wanasiasa kwa watu wanaotumia huduma hizi; bali pia hufanya watu kujiuliza kwanini hawawezi kuwa na uchaguzi kama huo katika huduma za umma kama vile mashule au kiinua mgongo, badala ya kuwaachia wanasiasa kuamua kwa niaba yao.

Kizazi kinachobadilika —kizazi cha baada ya vita kuu ya pili ya dunia katika Nchi za Magharibi na kuongezeka kwa idadi ya vijana wa kisasa kwingineko — pia kumeathiri mitazamo. Vijana wanalalamika kwamba kizazi cha wazee kinachotawala siasa kimetumia nguvu zake za kisiasa kuelekeza mambo katika upendeleo wao wenyewe. Kwa maana hiyo, kizazi cha wazee kimepiga kura ya kujichagulia wenyewe manufaa manono kama vile kiinua mgongo, bima dhidi ya matatizo ya kijamii na huduma za bure za afya, kwa sehemu fulani zikilipiwa kupitia deni ambalo wanakiachia kizazi cha vijana kuja kulilipa. Ni chanzo kingine cha hali ya kutoridhika na mchakato wa kawaida wa kisiasa.

## Hitimisho

Kwa sababu zote hizi, umma umezidi kujitenga na wanasiasa wake wa kidemokrasia. Na hivyo, kumetokea ongezeko la vyama vyenye wafuasi wachache wenye siasa kali na matendo ya ajabu. Hofu ya wale wanaounga mkono demokrasia ni kwamba kejeli ya umma dhidi ya tabaka la sasa la wanasiasa inaweza kuongezeka na kusababisha watu kupoteza zaidi imani katika mchakato wenyewe wa kidemokrasia. Hali kama hii inaweza kuwa bahati mbaya iliyopindukia, kulingana na manufaa mengi ya ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko. Hivyo, ni muhimu kwetu elewa chanzo cha hali ya sasa ya kutoridhika na kutafuta njia za kufanya siasa za kidemokrasia kuwa na maana zaidi kwa watu wote.

# 11. MUSTAKABALI WA USHIRIKI

## Aina za ushiriki

Baadhi ya watu hudhani kwamba matatizo ya demokrasia yanaweza kuondolewa kupitia njia inayoleta aina mpya za ushiriki wa umma. Mfano wao mkamilifu ni demokrasia 'shirikishi', ikiwa zaidi kama demokrasia katika maana yake ya kale, ambapo wananchi wanahusika moja kwa moja katika ufikiaji wa maamuzi. Wanalinganisha hali kama hiyo dhidi ya mbinu ya mkusanyiko inayotumika ya leo kwa lengo pekee la kuhesabu kura za watu na kutoa idadi yake.

*Upigaji kura wa lazima* ni pendekezo mojawapo. Ni ushiriki dhaifu ambapo mtu hana kitu cha kufanya zaidi ya kupiga kura tu, lakini tumaini ni kwamba utachochea pia maslahi mapana zaidi katika mdahalo wa umma. Nchi kadhaa tayari zina upigaji kura wa lazima, maarufu zaidi ikiwa Australia lakini pia nchi nyingine za kidemokrasia kama vile Uruguay, Ubelgiji na Luxembourg. Bado kuna ushahidi mdogo kwamba jambo hili lina athari yoyote katika matokeo ya uchaguzi au ubora wa mdahalo wa umma.

Pendekezo jingine ni *demokrasia ya moja kwa moja* kama vile kura za maoni na haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya mabunge, jambo ambalo humpatia kila mmoja haki ya kuzipigia kura ya moja kwa moja sheria zinazotungwa. Tunaona kwa mara nyingine tena, utaratibu huu tayari umetumika katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya majimbo ya Marekani pia yana utaratibu wa kupiga kura ya maoni ambao unawezesha wapiga kura kuzuia matumizi ya sheria zilizopoteza mvuto. Jimbo la California linaruhusu wananchi kutoa mapendekezo ya sheria mpya na hata mabadiliko ya Katiba ya Jimbo.

Mkakati wa tatu ni *jaribio la kutumia utafiti kupitia maoni ya umma kwa njia mpya zinazofaa*. Sampuli inayowakilisha watu wote katika nchi huchaguliwa kwa ajili ya kukusanya maoni yao. Halafu, wanakaribishwa pamoja katika kikao cha mwisho wa wiki ili kujadili matokeo. Wanapewa muhtasari wa hoja hizo. Wanajadili masuala hayo baina yao wenyewe, baina yao na wataalamu na pia baina yao na wanasiasa. Kisha masuala hayo yanapigiwa kura kwa mara nyingine tena, kuona tofauti gani imejitokeza baada ya kufanya mjadala wenye taarifa kamili, ikilinganishwa na matokeo ya awali. Utaratibu huu, inasemekana, husaidia wabunge au wawakilishi kuelewa maadili ya kweli ya umma kwa usahihi zaidi.

Kibadala cha utaratibu kama huu ni *majopo ya wananchi*, ambapo kundi dogo lakini lenye uwakilishi mpana, kwa kawaida watu 12-24, hukutana pamoja na kuwahoji mashuhuda wenye utaalamu, kisha kushiriki katika mjadala wa masuala yanayoibuka. Dhana ni kwamba matokeo yake yanakuwa na ushawishi mpana zaidi katika chaguzi za umma, na zile za wabunge au wawakilishi.

Watu wengi wamevutiwa na *demokrasia kwa njia ya kidijitali*. Takribani theluthi mbili ya watu ambao hawapigi kura kupitia sanduku la kura wanadai kwamba wangepiga kura kupitia mtandao wa intaneti endapo wangeweza kufanya hivyo. Watetezi wa dhana hii wanaonesha kwamba mifumo inayotumia mtandao wa intaneti huruhusu wapiga kura kupokea taarifa ya kina zaidi kuhusu masuala na hoja kabla ya kufikia uamuzi wao.

Teknolojia ya habari na mawasiliano tayari inajitokeza kwenye mchakato wa kidemokrasia. Australia imetangulia katika uanzishaji wa jukwaa la ‘MiVote’, ambalo huwapatia watu wenye haki ya kupiga kura mchanganyiko wa mitazamo mingi tofauti wa masuala yote makuu ya kujadiliwa bungeni. Iceland, mnamo mwaka 2008, ilitumia intaneti katika mchakato wa mageuzi yake ya kikatiba. Estonia inajiita yenyewe ‘taifa la kimtandao’. Na mifumo ya mashine inayojifunza na kutafsiri ya

lugha sasa inafanya liwe ni jambo linalowezekana kufanyika kwa midahalo mikubwa sana ikihusisha watu kutoka duniani kote.

Je, ni kweli kwamba teknolojia inasaidia mdahalo wa umma kufanywa na watu walio na taarifa kamili? Ushahidi hauashirii hivyo: wakati teknolojia inawasaidia watu kupata kiasi kikubwa cha taarifa na kuwawezesha kupigia kura wigo mpana wa masuala (siyo kuchagua tu wagombea wa uongozi), kimantiki wanabaki kuwa mbumbumbu kwa sababu muda wao ni haba, na kura zao kama mtu mmojammoja bado zinapewa uzito mdogo.

## Hoja zinazotetea ushiriki

Jibu mojawapo lingeweza kuwa; kuhusisha watu zaidi katika mchakato wa ufikiaji wa maamuzi. Na kuna hoja nyingine zinazotetea pia jambo hili. Watu wengi huchukulia kitendo chenyewe cha kuwahusisha wananchi katika maamuzi ya kijamii kuwa ni kitu chema. Kinapelekea watu kufikiri juu ya masuala yao. Kinakuza ufahamu wao wa masuala ya kijamii. Kwa kuwaweka watu katika nafasi bora zaidi ya kuwa na taarifa kamili, kinapaswa kuwaongoza pia katika kufanya chaguzi bora zaidi. Na zinaweza kufanywa katika ngazi zote — serikali zinaweza kutumia kikamilifu hekima ya watu kutoka nchi nzima katika maswali muhimu ya kitaifa, wakati ambapo wapangaji katika jengo moja la makazi wanaweza kutumia dhana hiyohiyo kuamua  jinsi ya kusimamia jengo lao.

Kuna hoja zenye mantiki pia. Mbinu ya mtindo kizamani wa kupiga kura  huifanya demokrasia kuwa mfumo ambao mamlaka yake yamelimbikizwa sana sehemu moja, kuwa yenye usumbufu, inayokwenda polepole na yenye ukomo katika mawanda yake. Wanasiasa hawawezi kuzingatia mitazamo ya kila mmoja na kuifanyia kazi, jambo linalopelekea kutungwa kwa sera inayofanya kazi vizuri katika baadhi ya mambo na kufanya vibaya

katika mengine. Ufikiaji wa maamuzi uliogatuliwa hufanya kazi haraka zaidi na kuzalisha sera zinazofaa zaidi kwa watu wa mahali husika na kwa hiyo ni imara zaidi. Wakati ambapo mtindo wa kizamani wa siasa unaweza tu kuvurumisha taarifa kwa wapiga kura *wote kwa pamoja* kupitia kaulimbiu na vipande vifupi vya sauti iliyorekodiwa, mifumo inayotumia mtandao wa intaneti huwapatia uwezo wa kuzifikia tovuti zote zenye kutoa taarifa za maana. Na aina hii ya demokrasia shirikishi inaweza kukomesha udhibiti unaofanywa na vyama vilivyojizatiti, inaruhusu fikra mpya kushamiri na kubadilisha masuala ya kijamii kushughulikiwa kwa haraka zaidi.

## Hoja zenye mantiki dhidi ya ushiriki

Wakosoaji hawajashawishika bado. Wanatoa hoja kwamba mbinu za demokrasia ya moja kwa moja kama vile kura za maoni au haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya mabunge bado zinahitaji wapiga kura kuwekeza muda mwingi na jitihada kubwa katika kujifunza namna ya kujadili masuala yanayoibuka, hata ingawa kura zao kama mtu mmoja mmoja bado zinabeba uzito mdogo sana. Na endapo hatuwezi kutarajia wapiga kura kufanya maamuzi yatokanayo na kuwa na taarifa kamili, basi huenda ni vizuri zaidi kuacha shughuli za utawala kwa wawakilishi wao wenye nafasi bora zaidi ya kuwa na taarifa kamili. ‘Demokrasia siyo hali inayoongoza mambo ya umma kwa kujiendesha yenyewe, ambapo watu wanakutana kila siku bila mwisho’, aliandika kiongozi mwanamapinduzi wa Ufaransa, Maximilien Robespierre (1794). ‘Demokrasia ni hali ambapo watu, kama himaya huru …hufanya kwa ajili yao wenyewe mambo wanayoweza kufanya vizuri na hufanya mambo wasiyoweza kuyafanya kupitia wajumbe wao…’.

Zaidi ya hayo, uzoefu wa Marekani unaashiria kwamba *haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya mabunge* vitaongozwa kwa

kiasi kikubwa na msukumo wa vyama vya siasa vilivyojizatiti, kwa kuwa vinapata fedha nyingi sana na vina uwezo wa kufanya kampeni. Mara nyingi pia, utaratibu huo wa raia kuwa na haki au uwezo wa kutoa maoni yao nje ya mabunge huwa umesanifiwa vibaya au huchochewa na makundi yenye maslahi yanayotafuta njia ya kuwanyonya walipakodi au kupambana na makundi yenye maslahi kinzani — ndiyo maana kila uchaguzi hushuhudia wafanyabiashara wakipoteza mamilioni ya dola za Kimarekani kupambana na mapendekezo maovu au yasiyofaa. Na mfumo huu huzalisha maamuzi ya kifedha na kisheria yanayobadilika mara kwa mara.

*Utaratibu wa kura za maoni* unaonekana kutoendana na demokrasia ya uwakilishi — ambayo maana yake kuu ni kuwaepushia wapiga kura ulazima wa kufanya uamuzi wa kila jambo na badala yake kuiacha kazi hiyo kwa wawakilishi wao. Kwa hiyo basi, kura za maoni hufanyika kwa malengo gani? Je, kura ya maoni inaweza kutumika katika utungaji wa sheria (ambapo baadhi sheria zinazokinzana sana na zisizondelea mabadiliko huwa na uwezekano mkubwa wa kupitishwa)? Je, kura ya maoni huwapa wawakilishi maelekezo ya namna ya kupiga kura (na kitu gani hutokea endapo wawakilishi watapiga kura kwa namna nyingine)? Au hufanyika tu kwa lengo la ushauri (na kama ni hivyo, kwanini tusitegemee tu maoni ya watu)? Mara nyingi hakuna majibu bayana ya maswali haya. Lakini, japokuwa jukumu halisi la kupiga kura za maoni ndani ya demokrasia ya uwakilishi linaweza kutokuwa bayana, inaweza kabisa kuwa shughuli yenye matokeo chanya. Ushahidi uliokusanywa na mwanataaluma wa Kimarekani anayeitwa John G. Matsusaka (2004) unaashiria kwa hoja ya nguvu kubwa kwamba kura za maoni zinazopigwa na watu wa mahali husika zinaweza na husaidia katika kutatua mivutano ya kisiasa na kuokoa fedha za walipakodi.

Na kwa upande wa *demokrasia kwa njia ya kidijitali*, wakosoaji wanasema kwamba bado utaratibu huu utaongozwa kwa

msukumo wa nguvu kutoka kwenye vyama vilivyojizatiti na makundi yenye ushawishi na fedha nyingi. Na baadhi ya wananchi, hasa wazee, wanaweza kuwa na uwezekano mdogo wa kushiriki kupitia mtandao wa intaneti, na hivyo, kudhoofisha dhana ya usawa katika medani ya siasa.

Kuhusiana na mifumo *ambayo kiini chake ni maoni ya umma*, wakosoaji kama vile Jason Brennan (2016) wanatoa hoja kwamba inafanya maamuzi *mabaya zaidi* kuliko mbinu ya mkusanyiko wa kufikia mapatano. Makundi ya majadiliano yana kawaida ya kufanya uchambuzi wa kina kwa hekima, siyo kuchangamkia tu fikra mpya. Washiriki huongozwa kirahisi na watu wenye nguvu ya kujenga hoja na mitazamo mizito. Kinadharia, wawezeshaji wasioegemea upande wowote wanapaswa kuwa na uwezo wa kusahihisha jambo hili: hata hivyo ni kitu kisichoepukika kwa wawezeshaji kuwa na uwezekano mbubwa wa kuleta hisia zao wenyewe katika mjadala. Kwa upande mwingine, watu wenye mitazamo iliyopoteza mvuto wanaweza kuona haya kuitamka mbele ya kadamnasi — ingawa wapo radhi kabisa kueleza mitazamo hiyo bila ya kujulikana kwenye kibanda cha kura. Hivyo tunaona kwa mara nyingine tena, makundi ya majadiliano yatakuja na mapatano na hoja za kuhitimisha za kikundi cha watu ambazo haziwakilishi maoni kamili ya umma kwa mapana yake.

## Msingi wa hoja dhidi ya ushiriki

Wakosoaji pia wanatoa hoja kwamba ushiriki kupitia vyombo rasmi siyo wa 'kidemokrasia' zaidi kuliko kitu ambacho tayari kipo. Wananchi tayari wanawasiliana moja kwa moja kwa idadi kubwa ya watu kupitia mitandao ya kijamii na njia nyingine za habari na mawasiliano, ambayo ni aina ya ushiriki wa karibu na mpana zaidi kuliko vyovyote vile ambavyo jopo la wananchi lingeweza kuwa. Na haipo bayana endapo mbinu ya ushiriki rasmi zaidi husaidia kwa hakika kutoa elimu na mwanga kwa watu wote

wenye sifa ya kupiga kura. Upigaji kura wa lazima, kwa mfano, hautoi dalili ya kuongeza maarifa ya wananchi katika masuala ya kisiasa, au kubadilisha matokeo ya uchaguzi.

Katika hali yoyote ile, wakosoaji wanaendelea, tatizo siyo elimu bali ni *motisha.* Taarifa lukuki zinavurumishwa kila siku kwa wapiga kura; wanazipuuza tu kwa sababu wana mambo yao binafsi ambayo ni muhimu zaidi kwao. Na hata hivyo watu hutofautiana sana katika upande wa shauku zao. Ni wachache tu wanaojiunga na vyama, kusambaza vipeperushi, kuhudhuria mikutano ya kisiasa au kujitolea fedha kwa makusudio mbalimbali. Hivyo kwanini tunalazimika kudhani kwamba kila mmoja angetaka kushiriki mjadala wa masuala ya umma endapo angepewa nafasi? Wengi wanaweza kujenga picha ya kiza kichwani.

Ushiriki kupitia taratibu zilizo rasmi, wanahitimisha wakosoaji wake, kwa ufupi hauna manufaa kwa watu wengi. Hawatauthamini, kuuheshimu, au kuitumia fursa kwa busara. Kwa asili huu siyo ushiriki bora au wa ‘kidemokrasia’ zaidi kuliko ule ambao tayari tunao.

## Je, ni kweli tunahitaji ‘demokrasia zaidi’?

Kuna sababu nyingine zenye nguvu, anasema Brennan (2016) zinazofanya demokrasia ‘shirikishi’ ambayo ni pana zaidi kuweza kwa hakika kuzaa matokeo mabaya zaidi. Tunajua kwamba wapiga kura wana umbumbumbu wa kutisha kuhusiana na mambo ya umma; dhana kwamba ushiriki unaweza kwa namna fulani kuwafanya wageuke na kuwa wataalamu wa sera ni upuuzi mtupu. Huenda haiwezekani hata kuwafanya wabadilike na kuwa wanafunzi mahiri — na wangepambana na jaribio la kufanya hivyo. Mambo mengine kama vile kazi, makazi, familia na shughuli wanazopenda kufanya ni mambo ya dharura zaidi au

yenye umuhimu mkubwa kwao. Kwa hiyo, kuwafanya wajihusishe katika siasa ni jambo lenye madhara kwao: linachepusha muda wao kutoka kwenye mambo wanayothamini na shughuli wanazotaka kufanya, na kuuelekeza kwenye jambo wasilothamini au kutaka kulifanya.

Kwani kuna haja gani kwa siasa kuchukua sehemu kubwa namna hiyo ya maisha yetu? Haioneshi kufanya watu kuwa macho zaidi na mambo ya kijamii au kuwa na maadili zaidi; na ina uwezekano mkubwa zaidi wa kuwapotosha. Uchu wa madaraka ya kisiasa unashawishi, kama yalivyo matazamio ya kulazimisha mitazamo yako mwenyewe kwenye maisha ya wengine. Maana kuu ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko ni kuweka ukomo wa uwezo kama huo na hivyo kuzuia wale waliopo katika mamlaka kufanya uonevu na unyonyaji kwa wengine. Lakini kadri utaratibu huo wa kufikia maamuzi kwa njia ya pamoja unavyozidi kupewa uhalali wa kisheria kwa kuuita ‘demokrasia shirikishi’, ndivyo ilivyo rahisi zaidi kuendelea kuwa hivyo, na kuwa vigumu zaidi kwa makundi ya walio wachache kupinga.

Tujiulize kwa mara nyingine tena, kwanini wanaharakati wengi sana wa kisiasa ni hodari kupita kiasi katika kudai demokrasia ‘zaidi’ au ya ‘kina’? Pengine ni kweli wanaamini kwamba inaimarisha tunu muhimu kama vile usawa katika medani ya siasa, au kuongeza zaidi uwazi, au ukuaji wa maadili, au kupunguza madaraka ya wajuzi wa mambo ya kisiasa. Lakini panaweza kuwapo maelezo kidogo ya kujitetea. Pengine wanataka tu kujipatia uhalali wa kisheria na kupanua wigo wa ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja, wakififikiri ni njia bora zaidi ya kuisimamia jamii kuliko kuachia maamuzi hayo kwa watu binafsi. Pengine wanatambua kwamba wapiga kura wana kawaida ya kutarajia uingiliaji mkubwa zaidi wa serikali katika shughuli za watu kuliko wawakilishi wao wa kuchaguliwa. Au pengine wanadhani uingiliaji mkubwa zaidi wa serikali utatoa ajira nyingi zaidi na hadhi ya juu kwa wanataaluma kama wao.

## Dhana ya demokrasia yenye ukomo

Kama ni kweli kwamba wapiga kura hawawezi kufikiri kwa mantiki, wala hawana taarifa kamili, wana ukabila na wanajali tu maslahi yao binafsi, swali la kujiuliza siyo jinsi ya kuwabadilisha (linaloonekana kutokuwa na mategemeo ya kufaulu), bali ni kwanini 'wao' ndio wanaopaswa kuwa na madaraka yoyote juu ya watu wengine. Hii siyo hoja ya *demokrasia zaidi*, bali *demokrasia yenye ukomo zaidi* — kwa ajili ya kuwa na serikali inayodhibitiwa ambayo haina ulazima wa kufanya maamuzi tuyonaweza kufanya sisi wenyewe, lakini iliyojikita kwenye jukumu lake la msingi la kulinda haki zetu, uhuru na usalama wetu.

Mtazamo wa demokrasia yenye kupendelea mabadiliko ni kwamba, tuliutengeneza mfumo huo kwa ajili ya kutulinda, na siyo kutudhibiti. Siyo utaratibu kwa ajili ya kuruhusu makundi ya walio wengi kusimamia sehemu kubwa za maisha ya kila mmoja. Ni njia tu ya kuchagua wawakilishi wanaoweza kuwa na taarifa kwa ubora zaidi, shauku kubwa zaidi na uwezo mkubwa zaidi wa kufanya yale maamuzi machache yanayotakiwa kufanywa kwa pamoja. Kuliko kujaribu kuwafanyia wapiga kura kitu ambacho hawataki kuwa, ingekuwa vizuri zaidi kujenga taasisi ili kuunda serikali bora kabisa kadri inavyowezekana kutokana na jinsi wapiga kura walivyo.

# 12. DEMOKRASIA NA MIPAKA

Kuanguka kwa Ukuta wa Berlin mwaka 1989 kulifanya serikali za kidikteta kujiweka katika hali ya kujihami. Uhalisia wa ukatili uliofanywa na Urusi ya Kisovieti ulianikwa, na kwa ujumla tawala zenye kulazimisha utii zilianza kupoteza uhalali wa kisheria. Demokrasia ya aina fulani ilionekana kuwa mbadala wa pekee. Vuguvugu la mageuzi lilienea Ulaya Mashariki, Amerika Kusini, Afrika (hasa kwa kukomesha ubaguzi wa rangi mwaka 1994), Asia Kusini, Asia Kusini Mashariki, hata kwa muda fulani nchini China. Nchi zaidi na zaidi zikatambuliwa kama nchi 'huru' katika medani za a kimataifa.

Mwanasayansi ya siasa wa Kimarekani, Francis Fukuyama (1992) aliwahi hata kuongelea 'mwisho wa historia' — dunia ambayo demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko lilikuwa imeshamiri mahali pote. Wanasiasa wa Nchi za Magharibi wanachukulia kwamba ni kazi yao kufanya dira hiyo itimie kwa kueneza demokrasia duniani kote. Madikteta walikutana na changamoto. Fursa za ufadhili wa kigeni na biashara zilitolewa kwa sharti la nchi kukomesha rushwa, kufanya mageuzi katika serikali zao na kuruhusu taasisi za kidemokrasia.

Hata hivyo, siyo rahisi namna hiyo kujenga au kuunda upya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko. Kama jaji wa Mahakama Kuu ya Marekani; Anthony Kennedy (1999) alivyogundua: 'Demokrasia ni kitu ambacho huna budi kujifunza kizazi baada ya kizazi. Ni sharti ifundishwe'. Na ukweli ni kwamba, ilichukua karne za mgogoro na umwagaji damu kwa baadhi ya mataifa kujifunza na kuanza kufuata demokrasia ya kisasa. Leo hii, kwa kutazama mifano mingi iliyopo kwa sasa kuhusiana na demokrasia, pengine mataifa machanga ya

kidemokrasia yanaweza kuasisiwa kwa haraka na kwa njia ya amani zaidi.

Bado kuna vikwazo vinabakia. Ili iweze kufanya kazi na kuzaa matunda yake, demokrasia inahitaji wananchi wenye kuikubali, kuielewa, kuithamini na kuiheshimu. Lakini watu ambao daima wameishi chini ya serikali ya kidikteta mara nyingi wanakuwa na hofu na uelewa potofu wa demokrasia. Kuna nyakati, madikteta kama vile Hosni Mubarak wa Misri na wale wa mataifa mengine ya Mashariki ya Kati na Kaskazini ya Afrika waling'olewa madarakani na kisha nafasi zao kuchukuliwa na tawala za 'kidemokrasia' ambazo kwa namna fulani hupendelea mabadiliko ya kiwango cha chini sana. Hii ni kwa sababu wanamapinduzi wanaochaguliwa kushika madaraka hujenga taswira vichwani mwao kuwa walio wengi huwapatia madaraka yenye nguvu zote. Kwa kukubaliana na viashiria vya demokrasia, japo wanakiuka misingi yake, viongozi hao hudai uhalali wa kutambulika kimataifa licha ya kuwa hawastahili. Katika maeneo mengine, madikteta kama vile Josip Tito wa Yugoslavia walifanikiwa kuzima mgogoro baina ya makundi hasimu ya itikadi za kitaifa, kidini au kikabila nchini mwao, hali iliyochelewesha tu vita vilivyosababisha uharibifu mkubwa sana, vilivyolipuka mara tu walipoondolewa. Hii inaonesha kwamba hofu za watu kuhusiana na mpito kutoka utawala wa kidikteta hadi utawala wa kidemokrasia zina uhalali kwa kiasi fulani.

## Makosa ya nchi za Magharibi

Demokrasia haiwezi kupandwa kirahisi tu kwenye ardhi mpya kwa mategemeo ya kuachwa ishamiri yenyewe. Inahitaji palizi na uangalifu. Na wala demokrasia haiwezi yenyewe tu kuleta ustawi, haki, uhuru na usawa katika nchi ambayo mambo haya hayajulikani na ambapo huchukuliwa kuwa ya kigeni. Inasikitisha kuona kwamba, wanasiasa wa Nchi za Magharibi

waliamini kuwa wangeweza kufanikisha yote hayo na hata zaidi. Na kwa sababu waliamini kwamba demokrasia huzalisha uhuru na ustawi (wakati katika uhalisia ni maadili yenye kupendelea mabadiliko ambayo ndiyo huzaa mambo haya), walifikiri kwamba nchi maskini sana zingejenga taasisi zao wenyewe za kidemokrasia kwa shauku, mara tu baada ya kuwa huru dhidi ya udikteta.

Hata hivyo, raia wa nchi za Magharibi wameishi kwa muda mrefu sana chini ya taasisi za kidemokrasia zenye kupendelea mabadiliko kiasi kwamba wanazichukulia kuwa ni kitu cha kawaida. Wanadhani kwamba utoaji wa haki, utawala unaozingatia sheria, haki, imani na uaminifu vinapatikana kila mahali — au vitafufuka na kuchipua mara moja punde ukandamizaji unapokoma. Wanadhani nchi zote zina hisia inayofanana ya utaifa, na kwamba kuna tabaka la kati lililoelimika na lenye kupendelea mabadiliko ambalo litaelewa na kusukuma mbele mageuzi ya kidemokrasia.

Bado kuna nchi zilizoishi chini ya utawala wa ‘mtu’ mmoja kwa karne na karne, na huenda zisiwe na lolote miongoni mwa mambo haya, wala kuwa na dhana yoyote bayana juu ya mambo hayo. Kunaweza kuwa na chuki yenye mizizi mrefu sana na kiwango cha chini cha kuaminiana baina ya makabila au makundi mengine. Watu wanaweza kuamini kwamba nchi yao haiwezi kusonga mbele bila ya uongozi imara wa utawala wa mtu mmoja. Wanaweza kuona nchi zilizojizatiti kidemokrasia kuwa ni dhaifu, zilizonyongea na kukosa mshikamano. Wanaweza kuendelea kuthamini umoja madhubuti wa kitaifa dhidi ya uhuru, desturi dhidi ya ustawi, au dini dhidi ya sheria.

Ryan Murphy (2018) ameonesha kwamba, hata baada ya kuzingatia vigezo vingine vyote, utawala wa mtu mmoja hauwezi kwa vyovyote vile kuzaa matokeo bora zaidi ya kiuongozi. Hata hivyo, inaweza isiwe rahisi namna hiyo kuishawishi dunia juu ya manufaa ya demokrasia.

## Matatizo ya nchi changa za demokrasia

Ukweli ni kwamba, pale nchi zinapokubali kutumika kwa viashiria vya demokrasia — chaguzi za viongozi, mabunge, mahakama za kisheria —zinaweza kuwa bado hazijakubali uhalisia wa demokrasia. Kuna uwezekano wa kuwa na utawala usiozingatia sheria. Mahakama za kisheria zinaweza kunuka rushwa. Kuna uwezekano wa kukosa uhakika wa kupata haki au haki kutolewa kwa wachache. Utaratibu wa kusawazisha tabia au matendo ili yakubaliane na dini unaweza kuingilia au kuzuia uhuru wa mtu binafsi. Chaguzi za viongozi zinaweza kuwa bandia, zisizokuwa na uchaguzi wa kweli wa wagombea na kura kuhesabiwa kwa upendeleo. Bunge linaweza kuhodhiwa na chama kimoja pekee. Washindi wa uchaguzi wanaweza kutumia 'mamlaka yao ya kidemokrasia' kuwatesa wapinzani.

Na kuna uwezekano wa kukosekana kabisa hisia ya pamoja ya utaifa. Migogoro baina ya watu wa asili tofauti, kikabila, kitamaduni, kiitikadi au kidini inaweza kuzaa kisasi cha kudumu na mfarakano. Vyama hasimu vya siasa vinaweza kuzaa taifa legelege na lisilotengemaa. Wakati fulani watu pekee wenye mamlaka na heshima wanakuwa ni wale mabwana wa vita wanaopingana. Watu wanaweza kuona nguvu za kijeshi kama njia pekee ya kutuliza hali ya mambo; au njia muhimu sana katika kulazimisha imani yao ya kidini au itikadi yao ya kisiasa kwa wengine.

Kwa hiyo, serikali imara ya kijeshi inaweza kabisa kuwa mashuhuri zaidi kuliko dhana yoyote ya serikali huru ya kidemokrasia. Wakati huohuo, wakereketwa wa kidini na kisiasa wanaweza kuwachukulia wapinzani wao kama waovu wasioweza kupata wokovu, na demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko kama uhasama dhidi ya misingi yao kwa sababu inavumilia mitindo mbadala ya maisha. Pindi wakereketwa kama hao wanapokuwa radhi kutumia ugaidi au nguvu za kijeshi kusukuma mbele dira yao, inaweza isichukue muda mrefu kabla ya taasisi zinazoanza

kupiga hatua katika nchi ya demokrasia changa kukanyagwa-kanyagwa.

## Majaribio yaliliyoshindwa ya kulazimisha maadili ya kidemokrasia

Ingawa matazamio ya kuanzisha demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko katika maeneo yenye matatizo kama hayo hayatoi dalili za kufanikiwa, serikali nyingi za mataifa ya Magharibi zimekuwa hodari katika kujaribu kufanya hivyo, zikiamini kwamba demokrasia ndiyo suluhisho bora kabisa. Na zikiamini kwamba demokrasia huchochea amani, uhuru na ustawi, serikali hizo zinaweza kutamani nchi nyingine zifurahie pia manufaa haya. Zinaweza kuona misingi ya kidemokrasia, kama vile chaguzi huru za viongozi na haki kwa watu wote kupiga kura katika chaguzi za umma kama njia ya kusukuma mbele mageuzi ya kijamii na kisiasa. Zinaweza hata kuichukulia demokrasia yenyewe, kama mfano bora au mkamilifu, na pia kama ushuhuda wa misingi muhimu kama vile utu wa mwanadamu na usawa katika ulingo wa kisiasa.

Hata hivyo majaribio yao haya ya 'kuagiza' demokrasia na 'kuiingiza' katika nchi nyingine yamekutana na mafanikio yenye ukomo na mara nyingi yamekuwa kitu kisichofaa kabisa. Kwa mfano, Vita ya Iraq ya mwaka 2003 na kuendelea, ilianza ikiwa na lengo lililokuwa na ukomo la kuondoa utawala wa kidikteta wa mtu mmoja. Inaonekana kulikuwa na dhana kwamba, mara tu baada ya lengo hili kufikiwa, fikra, misingi na taasisi za demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko vingefufuka na kuchipua kwa namna fulani. Hata hivyo, jambo hilo lilithibitika kuwa ni hali ya kutarajia mazuri kupita kiasi. Na inasikitisha kuona kwamba, kuondolewa kimfumo kwa wafuasi waaminifu wa utawala huo kuliacha taasisi za msingi (polisi, mahakama, utumishi wa umma) bila viongozi — na kusababisha machafuko,

kupotea kwa hali ya kuaminiana na kufanya iwe vigumu *zaidi* kuanzisha mageuzi ya kidemokrasia.

## Taasisi za kimataifa

Je, taasisi za kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa zinaweza kufanya kazi nzuri zaidi ya kuipeleka dunia katika demokrasia? Zipo sababu nyingi za kubaki na mashaka juu ya dhana hii.

Kwanza, vyombo vya kimataifa kama vile Benki ya Dunia au Shirika la Fedha Duniani mara nyingi huchukuliwa kama ukoloni mamboleo — nchi za Magharibi zikitumia utajiri wao kulazimisha dhana yao fulani ya serikali kwa wengine. Kwa mfano, wanaweza kuyanyima msaada wa fedha mataifa yasiyokubaliana na dira yao ya uwajibikaji wa umma.

Pili, mashirika mengi ya kimataifa huegemea sana upande wa mataifa makubwa zaidi au yaliyopata kuwa na nguvu duniani. Kwa mfano mataifa ya China, Ufaransa, Urusi, Uingereza na Marekani yana nguvu ya kupiga kura ya veto kupinga azimio lolote la Umoja wa Mataifa; lakini mataifa ya Japan, Ujerumani na India ni makubwa zaidi kiuchumi kuliko Uingereza na Ufaransa.

Tatu, watu wengi wanahoji endapo Umoja wa Mataifa unaweza kweli kuwa nguvu inayoaminika ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko wakati ambapo Baraza la Haki za Binadamu la umoja huohuo linajumuisha mataifa kama vile Kongo na Eritrea yaliyopo katika nafasi mbaya kwenye orodha ya kimataifa ya uhuru wa watu.

Ukosoaji wa nne ni kwamba taasisi za kimataifa huwakilisha serikali, siyo watu. Mara nyingi serikali hizo hupuuzwa na hata kuchukiwa na raia zake wenyewe, au sehemu kubwa ya watu

wake. Lakini bado utakuta wajumbe kutoka nchi hizo wakijielekeza kuongea kwa niaba ya nchi nzima. Vyombo vilivyoundwa kwa mtindo huu havina uwezekano wa kuaminika kuwa vichocheo vya mageuzi ya kidemokrasia.

## Dunia ya kidemokrasia?

Kwa kipindi cha walau karne moja, wafuasi wa falsafa ya udhanifu wamekuwa na ndoto za kuunda serikali moja ya kidemokrasia duniani. Kuna matatizo makubwa katika fikra hii pia.

Kwanza, demokrasia haina uwezekano wa kufanya kazi katika ngazi ya kidunia. Namna gani itawezekana kwa idadi ya watu bilioni 7.8 kuweza kushiriki katika mchakato wa uchaguzi? Tunawezaje kutengeneza muundo wa serikali ya dunia ambayo itamwakilisha kila mmoja bila upendeleo — bila ya mataifa yenye nguvu kubwa ya kiuchumi  au idadi kubwa ya watu kuwa na udhibiti? Na kwa kuzingatia tofauti zilizopo duniani za fikra, utamaduni, historia, biashara, urafiki au uadui na misimamo, itawezekanaje kwa mtu yeyote kujielekeza katika kuiwakilisha ‘dunia’ kwa namna yoyote ile?

Hata majaribio ya kadiri ya mataifa kuja pamoja na kuunda serikali moja ‘kuu’ juu ya serikali zao yamethibitika kuwa magumu. Kwa mfano, zipo karibia nchi thelathini zinazowakilishwa katika Bunge la Umoja wa Ulaya. Hili ni bunge linalochaguliwa na watu wote, lakini kufuatia kuwa na mataifa mengi sana na vyama vingi mno vinavyohusika, pamoja na maslahi mengi sana tofauti ya kitaifa, limejikuta lina mamlaka au madaraka kidogo sana. Maamuzi halisi hufanywa na wajumbe wasiochaguliwa wa vyombo vya serikali za kitaifa. Wakosoaji wanalalamikia ‘uhaba wa demokrasia’ lakini ni vigumu kupata

njia ambayo demokrasia inaweza kusanifiwa na kufanya kazi nje ya mipaka ya mataifa.

Pili, kadri idadi ya taasisi inavyozidi kuwa kubwa zaidi, ndivyo inavyokuwa vigumu zaidi kuzifanya ziwe wazi na zenye kuwajibika kwa watu wanaodhaniwa kuwakilishwa na taasisi hizo. Kwa serikali ya dunia, umbali (kimwili na kisitiari) baina ya serikali na raia wake, ukiongeza na mchanganyiko unaoweza kusababisha mtafaruku wa lugha mbalimbali, tofauti ya mitazamo katika masuala ya kimataifa itakuwa kubwa sana kuweza kutoa uwakilishi wa kweli, uangalizi makini au hata kuwezesha mawasiliano. Wapiga kura watakuwa mbali zaidi na chombo kama hicho kuliko hata walivyo mbali serikali yao wenyewe ya ndani.

Pia kumbuka kwamba mifumo ya kisheria ya nchi tofauti haifanani. Ikiwa imejengwa kipindi cha karne na karne, mifumo hiyo imekuwa na mizizi mirefu, na hutoa taswira tofauti katika mipangilio ya kihistoria, kitamaduni, kijamii na lugha. Huchipuka kutoka katika madhanio tofauti na pia hufanya kazi kwa misingi tofauti. Inatoa hadi hitimisho la mitazamo ya sheria na utoaji wa haki inayotofautiana kabisa na kupingana. Ni kutarajia mazuri kupita kiasi, kuamini kwamba tofauti kama hizo zinaweza kupuuzwa na kisha mifumo anuwai sana kama hiyo kusawazishwa. Lakini demokrasia inaweza tu kuwapo katika msingi uliokubaliwa wa utawala unaozingatia sheria.

## Mfumo kwa ajili ya makundi madogo?

Demokrasia hufanya kazi kirahisi zaidi ndani ya makundi madogo. Katika nchi ndogo zaidi, kuna uwezekano mkubwa sana wa watu kuwa na maadili yanayofanana, mitandao yenye nguvu ya mahusiano baina ya watu, hisia ya kuwa wamoja, kiwango cha juu cha kuaminiana. Katika jamii kubwa zaidi kuna uwezekano

wa kuwa na makundi mengi tofauti yenye maadili yasiyofanana, na ambapo watu hawafahamiani kwa ukaribu kiasi hicho. Inaweza kuwa vigumu zaidi kufanikisha suala la watu kuaminiana.

Hata hivyo bado jamii kubwa zaidi *zinaweza* kuwa na kiwango cha juu cha kuaminiana, na pia nchi za kidemokrasia zilizojengwa katika msingi huo — japokuwa, kama Vincent Ostrom (1997) anavyoeleza, mchakato wake unaweza kuwa mgumu na wenye kuchukua muda mrefu. Panaweza kuwepo pia taratibu maalumu kwa ajili ya kuwezesha taasisi za kidemokrasia kufanya kazi. Kwa mfano, nchi zinazoundwa na watu wenye tofauti kubwa baina yao, kama vile asili au lugha tofauti, zinaweza kutumia mifumo ya shirikisho inayoweka ukomo wa kiwango ambacho maamuzi yanaweza kufanywa kwa pamoja: Uswisi na Kanada ni mifano yake. Linaweza pia kuwa jambo la umuhimu wa kipekee kutambua kwamba nchi za kidemokrasia ambazo ni kubwa kabisa kwa eneo la ardhi (kwa mfano, Kanada, Marekani, Australia na India) zinafuata mifumo ya shirikisho.

Kwa mara nyingine tena, kuna mifano mingi sana duniani kote ya nchi ambazo zimeunda serikali za kidemokrasia katika maeneo yasiyotoa tumaini la mafanikio au matokeo kwa siku zijazo. Nyingine zinazotafuta manufaa ya demokrasia zina chaguzi nyingi za kuiga na kuzifanyia mabadiliko katika mazingira yao wenyewe. Yamkini isiwe rahisi, lakini (kufuatia malalamiko yao yote dhidi ya wanasiasa) watu wengi wanaoishi katika nchi ambazo kwa kiasi chake zinafuata demokrasia ya mabadiliko bado wanatoa hoja kwamba hakika ilistahili jitihada iliyotumika.

# 13. FUNZO KUTOKANA NA UZOEFU

## Je, kweli tunahitaji demokrasia?

‘Demokrasia liliwahi kuwa neno baya’, aliandika mwanasayansi ya siasa wa Kanada, C. B. Macpherson (1966). ‘Kila mtu aliyekuwa mtu fulani alijua kwamba demokrasia, katika hisia yake ya asili ya utawala wa watu au serikali kulingana na utashi wa halaiki ya watu, ingekuwa kitu kibaya — kinachotoa hatari ya kuua uhuru wa mtu binafsi…. Halafu, ndani ya miaka hamsini, demokrasia ikawa kitu kizuri’.

Demokrasia inaweza kuwa dhana inayokubalika kwa watu wengi, lakini ni vigumu zaidi kuielewa, na kuitumia, kuliko watu wengi wanavyodhani. Inategemea sana utamaduni wa kuheshimu haki za mtu binafsi, utawala unaozingatia sheria, ustahimilivu, na taasisi zenye kuaminika — vitu ambavyo vyote kwa pamoja vinaweza kuchukua muda mrefu kujijenga. Hii ndiyo sababu majaribio ya kuleta demokrasia katika tamaduni nyingine (kama vile tawala zilizofuatia baada ya udikteta kung’olewa Afrika Kaskazini, Mashariki ya Kati na Asia) mara nyingi yameishia katika majanga na kutengeneza tu aina tofauti ya udhalimu — wa makundi ya walio wengi, wa kiitikadi, au wa misimamo mikali ya kidini.

Watu hujenga picha vichwani mwao kuwa demokrasia inafanana na aina fulani timilifu ya ‘serikali ya watu, inayotokana na watu na kwa ajili ya watu’, kama alivyosema Rais wa Marekani Abraham Lincoln (1863) katika hotuba yake ya Gettysburg. Lakini demokrasia ya kisasa siyo kitu kama hicho: watu huchagua tu wawakilishi ambao baada ya hapo ndiyo ambao hufanya maamuzi. Endapo wewe upo katika upande ulioshindwa, ni vigumu kwa kitu hicho kuwa serikali ‘kwa ajili’ yako. Na hao ‘watu’ ndiyo akina nani hasa? Ilichukua karne kadhaa kwa

wanawake kupata haki ya kupiga kura; na kuna baadhi ya nchi zimegawanyika sana baina ya 'watu' wa makabila tofauti. Pia kuna hoja pana zaidi ya kifalsafa kuhusu haki ambayo idadi yoyote ya walio wengi wanapaswa kuwa nayo ili 'kuwatawala' walio wachache katika mazingira yoyote yale.

Demokrasia inaweza kuimarisha maadili ya maana kama vile usawa na kujumuisha watu wote katika medani ya siasa, utoaji wa haki, uwajibikaji na uhusika wa jamii katika mambo yanayohusu watu wake. Mwandishi wa riwaya kutoka Uingereza; E. M. Forster (1951) alitoa 'shangwe mbili kwa demokrasia', 'mosi kwa sababu inakubali mchanganyiko wa mitazamo tofauti na pili kwa sababu inaruhusu ukosoaji'. Lakini hata pale ambapo demokrasia ni nzuri kwa kadri ilivyo, yenyewe peke yake haitoshi. Haina budi kuzaa matokeo mazuri pia. Tunaweza kuihalalisha demokrasia endapo tu *inafanya kazi*.

## Kipi kinahalalisha demokrasia?

Kama alivyogundua mchumi wa siasa wa karne ya ishirini kutoka Austria; Joseph Schumpeter (1942), huenda ni kweli kabisa kuwa katika zama za Enzi za Kati, umma wa watu ulipiga kura ili kufikia uamuzi wa kuwachoma moto wachawi. Na hata leo hii bado kuna maeneo ambapo makundi ya walio wengi yanaamini kwamba inakubalika kabisa kuyatesa makundi ya walio wachache ya watu wasiokubaliana nao.

Hata hivyo, hatupaswi kudhani kwamba walio wengi wana mamlaka yasiyoweza kuhojiwa ya kuwatawala wengine, au kwamba maamuzi ya walio wengi yanakuwa moja kwa moja ni 'haki' na 'halali'. Baada ya kupitia uzoefu wa mifumo mbadala, watu wa leo hii walioelimika zaidi, wenye maarifa makubwa zaidi na wenye kupendelea mabadiliko wamefikia hitimisho kwamba utawala wa walio wengi siyo kipimo cha thamani ya utu. Mambo

kama ustahimilivu na kuthamini maisha ya wengine yapo juu zaidi ya utawala huo.

Lakini endapo demokrasia haipo kwa ajili ya kutoa kipimo sahihi cha madaraka ya walio wengi, tunaweza kutumia kipimo gani kuhukumu kama kweli inafanya kazi? Kuna uwezekano mwingi: kwa mfano, inaweza kutazamwa endapo kweli inapunguza mgogoro na kuruhusu kupokezana madaraka kwa amani, au endapo ni kweli maamuzi yake yamepitia tafakuri ya kina, yamejikita katika hali halisi na yameleta ufanisi.

## Ni ipi taswira ya demokrasia endelevu?

Ili iweze kufanya kazi na kudumu, demokrasia inahitaji kuendelea kujikita kwenye lengo lake kuu — ambalo kwa nadharia yenye kupendelea mabadiliko ni kuhifadhi haki za binadamu, kupunguza matumizi ya nguvu, na kufanya maamuzi katika yale mambo machache (na katika mambo hayo tu) ambayo ni sharti yafanyiwe maamuzi lakini maamuzi ambayo hayana budi kufanyika kwa pamoja. Ni sharti kwa demokrasia kutanguliza haki kwanza na kuzitambua kama kitu chenye umuhimu wa lazima kwa ajili ya kulinda watu binafsi dhidi ya uonevu unaofanywa na wengine au unaofanywa na serikali. Bila ya kuwa na sifa kama hizo, tawala za kidemokrasia zinakuwa na uwezekano mdogo wa kudumu kwa muda mrefu.

> Tawala za kidemokrasia daima zimekuwa mboni za vurugu na ushindani…na kwa ujumla kama ambavyo zimekuwa na umri mfupi katika maisha yao ndivyo ambavyo zimekuwa katili katika vifo vyao.
> — James Madison (1787), *Federalist No. 10*

Bado kuna idadi ya chini iliyowekwa ya taratibu za kufuata na taasisi zinazoweza kusaidia katika kuipatia demokrasia maisha marefu bila shaka yoyote. Panahitajika kuwapo kwa kanuni za lazima za kudhibiti madaraka yanayotokana na kura ya walio

wengi pamoja na wawakilishi wao. Ni sharti kuwe na chaguzi huru za viongozi, zinazoendeshwa kwa haki na ambazo ni shindani, zinazowapatia watu wenye haki ya kupiga kura mchanganyiko wa kweli wa watu wa kuwachagua. Ni sharti kuwe na ulinzi mkubwa zaidi wa uhuru wa kiraia, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa watu kukusanyika bila ya vitisho kutoka kwenye mamlaka za serikali. Ni sharti kusiwe na makundi ya kijeshi, warithi wa kifalme au watu wenye misimamo mikali ya kidini wenye nguvu ya kuingilia chaguzi zinazofanywa na umma au chaguzi zinazofanywa na wabunge au wawakilishi.

Leo hii, haki kamili ya kupiga kura kwa watu wazima inaonekana kuwa jambo lenye umuhimu wa lazima, na ingekuwa vigumu kuwa na demokrasia ya kisasa bila ya kuwa na haki hiyo. Lakini bado tunahitaji kukubali kwamba kuna nyakati wapiga kura hufanya maamuzi mabovu kabisa — kwa mfano mwaka 1932, walifanya Nazi kuwa chama kikuu katika bunge la Reichstag, Ujerumani. Na hata katika nchi zenye kiwango cha juu sana cha kupendelea mabadiliko, siyo kwamba mara zote wapiga kura huchagua kile wanachoamini kuwa ni bora kabisa kwa nchi yao, bali kile wanachoona ni bora kabisa kwa ajili yao wenyewe. Vilevile wapiga kura wengi ni tegemezi wa serikali katika kuendesha maisha yao, kitu ambacho kwa namna yoyote ile hugusa hisia zao katika chaguzi za upigaji wa kura. Baadhi wapiga kura wanaweza hata kukosa umahiri wa kufanya chaguzi za maana. Hatuwaruhusu majaji wasio mahiri kuamua juu ya uhuru wa mtu, anadokeza Jason Brennan (2016), hivyo kwanini tunaruhusu wapiga kura wasio mahiri kuchukua uhuru wa kila mmoja? Hata hivyo hakuna njia isiyo na utata wala kuegemea upande wowote ya kukubaliana na umahiri wa watu wenye haki ya kupiga kura: tunabaki tu kuwa na tumaini kwamba demokrasia ina uimara wa kutosha kuhimili makosa yao.

‘Haijawahi kamwe kutokea demokrasia ambayo haikuwa na madhara kwake yenyewe’, aliandika Rais wa pili wa Marekani,

John Adams (1814). Hata hivyo bado demokrasia ndiyo mfumo imara kuliko yote, na inabaki kuwa kama fumbo, endapo watu wapo huru kuachana nayo. Huko ni kupiga kura kwa kutumia miguu yako na kutuma ujumbe wenye nguvu zaidi kwa wenye mamlaka kuliko kitendo cha kutumbukiza tu karatasi kwenye sanduku la kura. Kama serikali zinafanya kazi ya kutumikia manufaa ya watu, kama Jayme Lemke (2016) alivyosema, zinakuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kusalia madarakani; lakini endapo hazifanyi hivyo, na kung'olewa, kunaweza kukawa na shinikizo kubwa zaidi la kufanya mageuzi katika hali ya mambo. Mifumo ya shirikisho inaweza kuwa njia rahisi ya kuepuka hali isiyoridhisha, kwa kuwa watu binafsi wanaweza kuhama bila shida sana na kuishi katika jimbo jingine lenye mifumo tofauti ya kiserikali. Hata hivyo mpaka leo hii, kuhamia nchi nyingine ndiyo uchaguzi unaozidi kukua.

## Mbadala wa mifumo ya kidemokrasia

Demokrasia inaweza kuwa na matatizo, lakini hayawezi kujitatua yenyewe  kwa kuwa na demokrasia 'zaidi'. Upigaji wa kura ya moja kwa moja ya mapendekezo ya sheria kupitia kura za maoni na haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya mabunge vinaweza kuzaa matokeo yenye utata na yenye kutafuta kumfurahisha kila mtu, wakati ambapo mifumo ambayo kiini chake ni maoni ya umma na utaratibu wa kupiga kura kupitia mtandao wa intaneti vinaweza tu kuongeza dosari ambazo tayari zipo. Kuna masuala muhimu pia — watu wa kawaida hawana shauku wala muda wa kupoteza katika kujadili sera, jambo linalomaanisha kwamba utungaji wa sera unaweza kutekwa na wale wanaovutiwa na shughuli hiyo, lakini wasiowakilisha umma. Na kitendo cha kufikia maamuzi kwa kura ya walio wengi kuonekana kuwa na uhalali zaidi kisheria, utaratibu wa 'ushiriki' kama huo unaweza hata kuwa kitisho kikubwa zaidi kwa makundi ya walio wachache.

Lakini tena, tunahitaji kiasi gani cha ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja? Jamii zina uwezo wa wa kushangaza wa kujipanga wao wenyewe bila ya kuhitaji maamuzi ya pamoja au amri kutoka juu. *Mfumo wa asili unaotokana na matendo ya hiyari ya mwanadamu* kama mchumi F. A. Hayek (1988) wa Austria alivyouita, umetuzingira mahali pote: katika masoko, kwa namna kama ile inayopelekea lugha kukua, katika taasisi za mtandaoni kama vile Wikipedia na muhimu sana katika sheria iliyozoeleka ambayo hujengeka kwa asili kupitia maingiliano baina ya watu binafsi. Kitu pekee kinachohitajika ni kanuni chache rahisi za kuangalia matendo na maadili. Au kirahisi, *usiwadhuru watu na usichukue mali zao*, kama mwanaharakati wa kisiasa wa Kimarekani; Matt Kibbe (2014) alivyosema katika kitabu chake kinachokwenda kwa jina hilohilo.

Kwa msingi huo wa kimaadili, watu wanaweza kuunda jumuiya zao wenyewe — mashirika ya asasi za kiraia au hata serikali ndogo ya jamii ya watu. Kuwa na tawala ndogondogo nyingi tofauti za jamii huwapa watu uchaguzi na fursa ya kuikwepa tawala fulani wanayohisi inawapuuza au kuwanyonya. Jambo hili bila shaka lisingewezekana chini ya 'serikali ya dunia'. Licha ya hayo, kanuni zinazounda mfumo wa asili wa jamii unaotokana na matendo ya hiyari ya mwanadamu hufanya kazi kirahisi zaidi kwa maridhiano katika makundi madogo. Demokrasia ni mkusanyo wa taasisi za mwanadamu ambazo msingi wake ni makubaliano na imejielekeza katika kufikia mwafaka. Jambo hili linahitaji uhusiano miongoni mwa wanadamu: demokrasia haitendi kazi kinadharia.

Teknolojia, kwa mara nyingine tena, hutupatia uwezo mkubwa zaidi wa kuongoza maisha yetu wenyewe bila ya kuhitaji watu wengine kufanya mipango inayohusu maisha yetu kwa niaba yetu. Teknolojia ya habari na mawasiliano huwezesha makundi madogo kujipambanua na kujiunga pamoja kwa ajili ya maslahi yao ya pamoja. Nani tena anahitaji serikali kubwa? Huduma za

umma na bima ya masuala ya kijamii vinaweza kufanyika kwa njia mpya zilizorekebishwa kulingana na malengo ya watu binafsi; shughuli za biashara zinaweza kufanywa huria kama ilivyo katika mifumo mipya ya biashara kati ya mtu na mtu inayoibuka kwenye mtandao wa intaneti.

Kwa hakika, hoja kwamba watu hawawezi kujitawala wenyewe (wakati fulani ikitumika kuwanyima wanawake na watumwa haki ya kupiga kura) inaonekana ikiendelea kupoteza mashiko. Watu ni wabunifu. Leo hii, wanaweza na wanafanya wenyewe uratibu wa shughuli zinazohusu maisha yao — na mipango yao ya kukodisha teksi, malazi wanapokuwa likizoni, usafirishaji wa vifurushi, malipo kwa mahitaji muhimu ya lazima na mengine zaidi — kwa ufanisi mkubwa na njia changamano za kistaarabu zaidi kupitia mtandao wa intaneti, badala ya kuhitaji jamii nzima kufanya maamuzi ya pamoja kwa niaba ya kila mmoja.

## Demokrasia siyo kila kitu

Wenye shauku kubwa ya demokrasia wanatamani kuona demokrasia zaidi — ikieneza kwa mapana zaidi katika nchi nyingine na wao wenyewe kupanua wigo wa ufikiaji wa maamuzi kwa njia ya pamoja. Wanapaswa badala yake kukubali kwamba ufikiaji wa maamuzi kwa kura ya walio wengi ni jambo lenye dosari, na kwamba maamuzi ya 'watu' (kwa tafsiri yoyote ya 'watu' hao) hayana uhalali wa moja kwa moja kisheria — kama ilivyokuwa katika kuwachoma moto wachawi.

Kinyume chake, demokrasia ni sifa mojawapo tu ya serikali bora, ikiandamana na utawala unaozingatia sheria, haki za mtu binafsi, ustahimilivu, uhuru wa kutoa maoni na mengine mengi. Ili iweze kufanya kazi vizuri, demokrasia haina budi kuwa na ukomo katika mawanda yake unaoishia tu kwenye shughuli zake zenye umuhimu wa lazima, na kuacha uwanja salama ambapo watu

binafsi wanaweza kufanya mambo yao kadri wapendavyo. Na inapaswa kuwa na ukomo katika matendo yake, kwa namna inayokataza matumizi mabaya ya nguvu na madaraka dhidi ya watu. Hili linaweza kuhitaji udhibiti uliotajwa kikatiba, usawazishaji wa nguvu baina ya mihimili ya dola, na asilimia kubwa ya uwiano kutoka miongoni mwa walio wengi katika kufikia baadhi maamuzi. Lakini hii *demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko* inahitaji pia utamaduni na uelewa wa kina.

Demokrasia inahitaji uangalifu mkubwa. Inahitaji ushirikiano miongoni mwa wanadamu kwa kiwango cha hali ya juu sana. Inahitaji udhibiti binafsi wa mtu mwenyewe, hasa yule anayetoka upande wa walio wengi au mwenye nafasi ya mamlaka. Inatuhitaji tusamehe manufaa ya mtu binafsi na hamu ya kutaka kuridhika mapema kwa ajili ya kitu kitakachodumu kwa muda mrefu zaidi. Inatuhitaji tukubali makosa yetu na kujifunza kutoka katika makosa hayo kwa utashi na uaminifu wetu. Demokrasia siyo sawa na bidhaa iliyofungashwa tayari dukani kwa sababu ni sharti irekebishwe kulingana na mazingira yoyote yale ya kihistoria na kitamaduni inayoshughulika nayo. Inahitaji ukubalifu wa pamoja wa kila aina ya kanuni, katika mambo mawili; mtazamo mashuhuri wa kidunia unaoiwezesha demokrasia kufanya kazi na mapatano machache zaidi (mithili ya ‘tabia zilizokubalika’) yanayopelekea ifanye kazi vizuri. Inahitaji jamii huru inayofanya mambo yake kwa uwazi — jamii ya watu sikivu na idadi inayofaa ya watu, lakini ambayo ipo radhi kutengeneza mahusiano na jamii nyingine duniani zinazofanya mambo yao kwa uhuru na uwazi.

Kama ilivyo kwa wanasiasa wetu, wanaweza kujielekeza katika kuimarisha utaratibu wao binafsi wa kuwasimamia wananchi, badala ya kujaribu kusimamia utaratibu wa wananchi wenyewe. Na kuna mifano hai kwa nini uingiliaji kati wa kisiasa unapaswa kupunguzwa: jamii ni ngumu sana kwa mamlaka kuu yoyote kuifanyia mipango yake, kuisimamia au hata kuielewa.

Hakuna haja ya kuthibitisha uhalali wa uhuru wa mtu binafsi: unapambana mwenyewe na athari za matokeo ya jambo lolote unalofanya. Hata hivyo, kuna haja ya kuthibitisha uhalali wa demokrasia, kwa sababu *wengine* wanapambana na athari za matokeo ya jambo unalofanya wewe.

Je, tuipe sifa demokrasia kama kitu chenye uhalali uliothibitishwa? Bado ni majaribio katika kupiga hatua za maendeleo. Demokrasia ina uhusiano wa karibu zaidi na maadili yenye mwelekeo wa mabadiliko kama vile kuheshimu haki za binadamu, na pia uhuru wa kwenda mahali popote na kutajirika, tofauti na mifumo mingine. Mara baada ya kujizatiti, demokrasia imethibitika kuwa na uimara wa kushangaza na wenye kustahimilika. Na taasisi za kidemokrasia, hata pale zinapokuwa na dosari, hutoa jukwaa ambapo wanaounga mkono maadili yenye mwelekeo wa mabadiliko huweza kutoa hoja za utetezi wao na kufafanua manufaa ya kweli ya demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko katika ustawi na maadili.

# 14. NUKUU KUHUSIANA NA DEMOKRASIA

## Udhalimu wa walio wengi

Demokrasia isiyo na kikomo, ni kama utawala wa serikali ya wachache, ni udhalimu ulioenea kwa idadi kubwa sana ya watu.
— Aristotle (c. 350 KK) *Siasa*

Demokrasia siyo uhuru. Demokrasia ni mbwa mwitu wawili na mwanakondoo mmoja wanaopiga kura kuchagua kitoweo cha kula wakati wa mlo wao wa mchana. Uhuru unatokana na kuzingatiwa kwa haki fulani ambazo mtu hapaswi kunyimwa, hata kwa asilimia 99 ya kura.
— Marvin Simkin (1992) 'Haki za Mtu Binafsi', *Los Angeles Times*

## Madaraka hulevya

Punde tu watu wanapokuwa na madaraka, wanapotoka na wakati mwingine wanakuwa punguani pia, kwa sababu kuwa na madaraka huwainua hadi mahali ambapo uaminifu wa kweli kamwe haulipi.
— E. M. Forster (1951) *Shangwe mbili kwa demokrasia*

Serikali zote hukumbwa na tatizo linalojirudia: *Madaraka huwavutia watu wenye matatizo ya utambuzi, hisia na tabia*. Siyo kwamba madaraka hupotosha bali ni sumaku inayowanasa wapenda rushwa.
— Frank Herbert (1965) *Dune*

Ninashawishika kufikiri kwamba ni nadra kwa watawala kuwa juu au bora zaidi ya kiwango cha kawaida, ama kimaadili au kitaaluma, na mara nyingi wamekuwa chini ya kiwango. Na ninafikiri kwamba ni jambo la maana kupitisha, katika siasa, msingi wa kuwa tayari kwa hali mbaya zaidi…
— Karl Popper (1945) *Jamii ya Uwazi na Adui Zake*

## Utamaduni wa demokrasia

Endapo uhuru na usawa, kama inavyodhaniwa na baadhi ya watu kuwa hupatikana zaidi katika demokrasia, vingekuwa bora kabisa pale ambapo wengine wote nao pia wangepata mgao katika serikali kwa ukubwa uleule.
— Aristotle (c. 350 KK) *Siasa*

Kwa kumtoa kafara mtu binafsi kwa serikali, watawala wa dunia ya Kirumi walidhoofisha taratibu unyofu halisi uliyoiweka dunia hiyo. Waliwageuza wachapakazi waliojiheshimu kuwa wabinafsi.
— Sir Arthur Bryant (1984) *Ndani ya Bahari ya Rangi ya Fedha: Historia ya Uingereza na Watu wa Uingereza*

Hakuna mwakilishi anayepaswa kufuata kama kipofu maoni ya chama, pale ambapo yanakinzana moja kwa moja fikra zako mwenyewe bayana; ni kiwango cha utumwa ambacho hakuna mtu anayejithamini ambayeangeweza hata kufikiria.
— Edmund Burke (1741) *mambo ya Muungwana na Jarida la London*

Ni sharti dunia ifanywe kuwa salama kwa ajili ya demokrasia. Ni sharti amani yake kupandwa juu ya misingi mikuu iliyojaribiwa ya uhuru wa kisiasa.
— Woodrow Wilson (1917) *Hotuba katika Baraza la Wawakilishi juu ya Vita*

# NYONGEZA YA KUJISOMEA

## Maelezo kwa ufupi

Beetham, D. (2005) *Demokrasia: Mwongozo kwa Wanaojifunza*. London: Oneworld Publications.
Utangulizi rahisi, unaotamka misingi na taasisi zinazohitajika ili demokrasia iweze kufanya kazi na kulinganisha jinsi ambavyo demokrasia inajengeka katika uhalisia. Kitabu hiki kinaelezea matatizo ya nchi changa za demokrasia, hali ya kutoridhishwa na siasa kwa ujumla zaidi, na mibadala shirikishi.

Butler, E. (2012) *Uchaguzi wa Umma: Mwanzo.* London: Taasisi ya Masuala ya ya Kiuchumi.
Mwongozo rahisi wa jukumu la binafsi-maslahi miongoni wapiga kura, makundi yanayotoa shinikizo kwa serikali, wanasiasa na maofisa wa serikali, na jinsi ambavyo jambo hili linavyosababisha mashaka juu ya ufanisi na hali ya kutoegemea upande wowote ya maamuzi ya kidemokrasia.

Butler, E. (2013) *Misingi Mikuu ya Jamii Huru.* London: Taasisi ya Masuala ya ya Kiuchumi.
Ufafanuzi rahisi wa misingi inayotegemeza uhuru wa kijamii na kiuchumi pamoja na demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko, kama vile ustahimilivu, utoaji wa haki, haki ya kumiliki na kutumia rasilimali na usawa.

Crick, B. (2003) *Demokrasia: Utangulizi Mfupi Sana*. Oxford University Press.
Kitabu hiki kinafuatilia nyendo za historia ya demokrasia kuanzia Ugiriki ya Kale na kuelezea masuala kama vile siasa za kutafuta kumfurahisha kila mmoja, taasisi ya serikali bora, na uananchi.

Cartledge, P. (2018) *Demokrasia: Maisha*. Oxford University Press.
Mkusanyo mkubwa wa historia unaofuatilia chimbuko la demokrasia kuanzia Ugiriki ya Kale hadi Jamhuri ya Kirumi, mifumo baada ya enzi ya zama za kati,  Katiba ya Marekani na hadi nchi zinazofuata demokrasia ya mabadiliko leo hii — na jinsi ambavyo kila mfumo umeshuhghulika na suala la haki dhidi ya makundi ya walio wengi.

Weale, A. (2007) *Demokrasia*. London: Palgrave.
Kwa kiasi fulani ni kitabu cha kinadharia na kifalsafa lakini kinaibua maswali mazuri kuhusiana na asili ya demokrasia, changamoto zinazoikabili, na namna pekee inavyoweza kufanyiwa tathmini kupitia kuheshimu maadili yetu yaliyoota mizizi.

## Changamoto na wakosoaji

Achen, C. na Bartels, L. (2017) *Demokrasia ya Waumini wa Uhalisia*. Princeton University Press.
Uchambuzi mzuri wa matatizo yatokanayo na umbumbumbu wa wapiga kura, ukabila na kujikita katika mambo ya muda mfupi. Watunzi wa kitabu hiki wanapinga haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya mabunge na njia nyingine shirikishi za utatuzi wa mambo; wao wakipendelea chaguzi za mara kwa mara za viongozi zinazofanyika kila baada ya kipindi fulani cha muda na kuzuia serikali kujilimbikizia madaraka.

Brennan, J. (2016) *Dhidi ya Demokrasia*. Princeton University Press.
Mwanafalsafa anaonesha ubaguzi wa kimfumo wa wapiga kura, akitoa hoja kwamba hawawezi 'kuelimika' kupitia mifumo shirikishi, na kwamba wanaendelea tu  kuwa mbumbumbu zaidi kupitia mifumo hiyo waliyoiweka wao wenyewe. Anatoa hoja

kwamba demokrasia hufanya chaguzi ngumu kuonekana kitu rahisi, hujiegemeza kwenye matumizi ya nguvu, hewezesha watu binafsi kuwatawala wengine na hivyo hufanya wageni kuwa maadui.

Caplan, B. (2007) *Kisa cha Kufikirika cha Busara za Mpiga Kura*. Princeton University Press.
Maelezo ya kisasa ya jinsi ambavyo wapiga kura wana ubaguzi uliojengeka kimfumo — hasa dhidi ya soko, dhidi ya wageni kutoka nje, ubaguzi utokanao na kutarajia kupita kiasi uwezekano wa kutokea mabaya na kuishia kufanya mambo yasiyo na faida — unaovuruga matokeo ya mfumo wa kidemokrasia na kutupatia jibu kwanini demokrasia hushindwa kufanya kazi.

Karsten, F. na Beckman, K. (2012) *Kupita Demokrasia*. Scotts Valley, CA: CreateSpace.
Uhakiki wa kimantiki na rahisi kutoka katika mtazamo wenye kupendelea mabadiliko, unaoelezea kwamba demokrasia ni dhana ya kufikia maamuzi kwa pamoja na sasa katika mgogoro. Watunzi wa kitabu hiki wanatoa mfululizo wa visa vya kufikirika — muundo wa utawala wa uongozi unaotokana na kuchaguliwa na watu, haki, uhuru, kuvumiliana, nk. — ambavyo vinahusiana na demokrasia na kutoa dondoo ya matatizo yake — ikiwa ni pamoja na urasimu, ruzuku kwa watu wa hali ya chini na kujikita katika mambo ya muda mfupi. Wanatetea dhana mpya ya kuwa na serikali ndogo zaidi kupitia sheria nyepesi za msingi.

Ostrom, V. (1997) *Maana ya Demokrasia na Uteketeke wa Nchi za Kidemokrasia.* University of Michigan Press.
Uchunguzi wa hali za kijamii na kitamaduni zinazohitajika kwa ajili ya mfumo wa kidemokrasia kushamiri, na kwa ajili ya suala gumu la kuhifadhi uhuru mtu binafsi na uhuru wa asasi za kiraia mbele ya serikali 'za kidemokrasia' zenye nguvu kubwa sana. Pia kinachunguza ugumu unaojitokeza katika kujenga jamii za kidemokrasia ndani ya mabara tofauti, na hasa katika nchi zinazoibuka kutoka kwenye ukoministi.

Smith, C. na Miers, T. (2011) *Demokrasia na Kuanguka kwa Nchi za Magharibi*. Mji wa Kihistoria : Chapa ya Kitaaluma.
Kitabu hiki kifupi kinatoa hoja kwamba demokrasia inazalisha udhalimu mpya unaodhoofisha maadili yenye mlengo wa mabadiliko ambayo yamejengwa juu yake — kama vile utawala unaozingatia sheria, ustahimilivu, haki ya kumiliki na kutumia rasilimali, masoko huru, uhuru wa asasi za kiraia na uhuru wa kijamii. Wanasiasa wanaona demokrasia kama chanzo kinachofaa cha kujipatia nguvu kwa ajili ya miradi yao wenyewe, jambo linalopelekea kuwa na taifa la vitisho.

Stoker, G. (2007) Sababu ya *Siasa kuwa Suala Muhimu: Kuifanya Demokrasia Itende Kazi.* New York: Palgrave Macmillan.
Kitabu hiki kinaonesha kwamba siasa ni sehemu isiyoepukika ya demokrasia kwa sababu maamuzi ya pamoja ni muhimu sana kwa kila mmoja. Lakini siasa imekuwa 'fani ya kitaaluma' inayoacha umma ukiwa umefarakana — na hubezwa kupitia vyombo vya habari kutokana na namna inavyotangazwa. Kitabu kinatoa wito wa uwajibikaji mkubwa zaidi, ukomo wa matumizi ya chama, mwananchi kuwa na uwezo wa kupiga kura ya kutokuwa na imani na wigo mkubwa zaidi kwa watu kujiamulia mambo katika maeneo yao.

# Rejea nyinginezo

Acemoglu, D. na Robinson, J. (2006) *Chimbuko la Kiuchumi la Udikteta na Demokrasia.* Cambridge University Press.

Acemoglu, D. na Robinson, J. (2012) *Sababu ya Kuanguka kwa Mataifa.* New York: Crown Publishing Group.

Adams, J. (1814) Barua kwa John Taylor (XVIII). Washington, D.C.: Makavazi ya Taifa (https://founders.archives.gov/documents/Adams/99-02-02-6371).

Alves, A. na Meadowcroft, J. (2014) Mteremko wa Hayek wenye Utelezi, uimara wa uchumi mseto na ukubwa wa ghiliba za kujitafutia faida kubwa zaidi. *Fani za Kisiasa* 62(4): 843-861.

Aristotle (350 KK) *Siasa*.

Attlee, C. (1957) Hotuba iliyotolewa Oxford, 14 Juni.

Brennan, G. na Buchanan, J. M. (1980) *Nguvu ya Kutoza Kodi. Misingi ya Uchanganuzi wa Sera ya Fedha*. Cambridge University Press.

Butler, E. (2015a) *Falsafa ya Kisasa ya Mwelekeo wa Mabadiliko: Utangulizi.* London: Taasisi ya Masuala ya ya Kiuchumi.

Butler, E. (2015b) *Magna Carta: Utangulizi.* London: Adam Smith Institute.

Burke, E. (1774) Hotuba kwa Wapiga Kura wa Bristol (https://www.econlib.org/book-chapters/chapter-vol-4-miscellaneous-writings-speech-to-the-electors-of-bristol/)

Burke, E. (1790) *Tafakari za Mapinduzi nchini Ufaransa*. London: James Dodsley.

Kitengo cha Intelejensia ya Kiuchumi (2019) Orodha ya Ubora wa Demokrasia 2019 (http://www.eiu.com/topic/democracy-index).

Forster, E. M. (1951) *Shangwe Mbili kwa Demokrasia*. New York: Harcourt, Brace na Wenzao.

Fukuyama, F. (1992) *Mwisho wa Historia na Binadamu wa Mwisho*. New York: Free Press.

Hayek, F. A. (1944) *Kuuendea Utwana*. London: Routledge.

Hayek, F. A. (1979) *Sheria, Kanuni za Kisheria na Uhuru*, Toleo la 1. London: Routledge.

Hayek, F. A. (1988) *Majivuno katika Hatari ya Kifo: Dosari za Ujamaa*. London: Routledge.

Hobbes, T. (1651) *Dubwana*. London: Andrew Crooke.

Hume, D. (1758) *Insha za Maadili na Siasa*. Edinburgh: Alexander Kincaid.

Kennedy, A. (1999) Mahojiano kutoka *Mstari wa Mbele*: Haki Inauzwa. Mfumo wa Matangazo ya Umma.

Kibbe, M. (2014) *Usiwadhuru Watu na Usichukue Mali Zao*. New York: Harper Collins.

Lawson, R., Murphy, R. na Powell, B. (2020) Viashiria vya Uhuru wa Kiuchumi: Utafiti. *Sera ya Kisasa ya Kiuchumi* 38(4): 622-642.

Lemke, J. S. (2016) Ukinzani wa Maamuzi ya Kisheria na Sheria ya Mali za Wanawake Walioolewa. *Uchaguzi wa Umma* 166(3): 291–313.

Lincoln, Hotuba ya Gettysburg ya Mwaka 1863 (http://www.ourdocuments.gov/doc.php?doc=36&page=transcript).

Locke, J. (1689) Tasnifu ya Pili ya Serikali. Ndani ya *Tasnifu Mbili za Serikali.* London: Awnsham Churchill

Luxemburg, R. (1899) *Mageuzi au Mapinduzi ya kijamii?* (https://www.marxists.org/archive/luxemburg/1900/reform-revolution/).

Machiavelli, N. (1513) *Mrithi wa Ufalme*. Rome: Antonio Blado d'Asola.

Macpherson, C. B. (1966) *Demokrasia Halisi ya Dunia*. Oxford: Clarendon Press.

Matsusaka, J. G. (2004) *Kwa ajili ya Wengi au Wachache: Chanzo, Sera ya Umma na Demokrasia ya Marekani*. Chicago University Press.

Mencken, H. L. (1956) *Ripoti ya Walio Wachache.* Baltimore: Johns Hopkins University Press.

De Mesquita, B. B., Smith, A., Siverson, R. M., Morrow, J. D. (2003) *Mantiki ya Kudumu kwa Siasa*. Cambridge, MA: Massachusetts Institute of Technology Press.

Mill, J. S.  (1861) *Taswira ya Serikali ya Uwakilishi*. London: Parker, Son, na Bourn

Montesquieu, C.-L. (1748) *Kiini cha Sheria* (https://oll.libertyfund.org/title/montesquieu-complete-works-vol-1-the-spirit-of-laws).

Murphy, R. (2018) Uongozi na kipimo cha utawala wa mtu mmoja. *Uchumi wa Siasa za Kikatiba* 30: 131-148.
Orwell, G. (1946) Siasa na Lugha ya Kiingereza. *Horizon* 13(76): 252-265.

Pericles wa Athens (c. 404 KK) Hotuba ya Mazishi. Katika *Historia ya Vita vya Peloponnesia.*

Popper, K. R. (1945) *Jamii ya Uwazi na Adui Zake*. London: Routledge.

Ridley, M. (2020) *Jinsi Uvumbuzi Unafavyonya Kazi*. London: Fourth Estate.

Robespierre, M. (1794) *Ripoti ya Misingi ya Maadili ya Umma*. Philadelphia: Benjamin Franklin Bache.

Schumpeter, J. (1942) *Ubepari, Ujamaa na Demokrasia.* New York: Harper & Brothers.

de Tocqueville, A. (1835) *Demokrasia nchini Marekani*. London: Saunders na Otley.

Transparency International (2019) *Orodha ya Nchi zinazoongoza kwa Ufisadi.* Berlin: Transparency International.

Vidal, G. (1987) *Armageddon*. London: Grafton.

# Istilahi za msingi

**Utawala wa mtu mmoja**
Kutoka katika neno la Kigiriki *autos* (binafsi) na *kratos* (nguvu). Ni aina ya serikali ambapo mtu mmoja (*kwa Kiingereza 'autocrat'*) anakuwa na udhibiti wa madaraka bila ya kukabiliwa na kizuizi chochote cha kisheria au upigaji wa kura .

**Haki na uwezo wa raia kutoa maoni yao nje ya bunge**
Shauri, lililoitishwa na kundi la wapiga kura, ili kupitisha sera, kushinikiza kura bungeni, au kuitisha kura ya maoni.

**Katiba**
Mkusanyo wa mapatano, sheria na vigezo tangulizi vya mambo unaoeleza bayana jinsi gani serikali inavyoundwa na kutenda kazi, na mipaka ya madaraka ya wale wanaohusika.

**Serikali ya kikatiba**
Aina yoyote ya serikali ambapo madaraka yametafsiriwa na kuwekewa ukomo kupitia sheria ya msingi, mapatano au katiba iliyoandikwa. Hii inajumuisha *tawala ya kikatiba ya kifalme* ambapo ukuu wa nchi ni nafasi ya kurithi, *demokrasia ya kikatiba* ambapo wananchi wenye sifa wanaweza kuchagua na kuwawajibisha wale waliopo madarakani, na *utawala wa kikatiba wa serikali ya wachache* ambapo mamlaka yanahodhiwa na kikundi.

**Demokrasia**
Kutoka katika neno la Kigiriki *demos* (watu) na *kratos* (nguvu). Ndani ya Ugiriki ya Kale, ni aina ya serikali ambapo watu waliokuwa na haki ya kuitwa wananchi wa jiji ambalo lilikuwa ni himaya huru walikutana pamoja kujadiliana katika mdahalo na kuamua juu ya sheria na sera. Leo hii, ni aina yoyote ya serikali

ambapo watu wenye haki ya kuitwa wananchi huchagua wawakilishi wanaojadili na kuamua juu ya sheria na sera.

**Dikteta**
Kutoka katika neno la Kilatini *dicto* (kupanga masharti). Mtawala mwenye madaraka yanayompa nguvu zote katika nchi, hasa zaidi yule aliyetwaa udhibiti kwa nguvu.

**Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko**
Ni aina ya demokrasia inayotoa kipaumbele cha haki na uhuru wa mtu binafsi dhidi ya utawala wa walio wengi. Demokrasia ya mwelekeo wa mabadiliko inasifika kwa kufanya chaguzi za uongozi kwa uhuru na haki, kutenganisha madaraka baina ya mihimili ya dola, ustahimilivu na utawala unaozingatia sheria.

**Utawala wa serikali ya wachache**
Kutoka katika neno la Kigiriki *olígos* (wachache) na *arkho* (utawala). Ni aina ya serikali inayodhibitiwa na kundi dogo kama vile familia au kamati ya kijeshi.

**Kura ya kutokuwa na imani**
Utaratibu unaotumika ambapo watu wa mahali husika wenye haki ya kupiga kura wanaweza kuwafukuza wawakilishi wao kutoka madarakani nje ya ratiba ya kawaida ya uchaguzi.

**Kura ya maoni**
Kura inayopigwa na watu wote wenye sifa ya kupiga kura kuhusiana na jambo fulani, ambayo kwa kawaida huitishwa na serikali. Matokeo yanaweza kuwa lazima kwa bunge na serikali kutekeleza, au kuchukuliwa kama ushauri tu.

**Jamhuri**
Kutoka katika neno la Kilatini *res publica* (jambo la watu). Ni aina ya serikali ambapo madaraka siyo ya kurithi lakini hupatikana kupitia uchaguzi wa umma au uteuzi unaofanywa na wawakilishi wa kuchaguliwa na kuna nyakati unafanywa na

vikundi vya utawala wa wachache au utawala wa mtu mmoja. Kwa kawaida, madaraka katika jamhuri huwekewa ukomo kupitia mapatano yaliyoafikiwa au katiba iliyoandikwa. Kwa kawaida mkuu wa nchi huwa ni rais.

**Utenganisho wa madaraka**

Ni mfumo uliokusudiwa kuweka ukomo wa kujilimbikizia nguvu kwa kutenganisha shughuli za utawala katika mihimili tofauti kama vile serikali, bunge na mahakama. Mara nyingi sana, nguvu za kutunga sheria ni hugawanywa zaidi baina ya mabaraza mawili tofauti ya bunge.

## KUHUSU TAASISI YA MASUALA YA KIUCHUMI (IEA)

Taasisi hii ni shirika la utafiti na elimu (Namba ya usajili namba. CC 235 351), lenye wajibu wa udhamini. Dhima yake ni kuboresha uelewa wa mifumo mikuu ya jamii huru kwa kufanya uchanganuzi na kueleza kinaganaga jukumu la masoko katika kuleta ufumbuzi wa matatizo ya kiuchumi na ya kijamii.

Taasisi hii hufanikisha dhima yake kupitia:

- programu za uchapishaji za ubora wa hali ya juu
- kongamano, semina, mihadhara na matukio mengine
- ziara kwa wanafunzi wa shule na vyuo
- kupitia na kuonekana katika vyombo vya habari

Taasisi hii, ambayo iliasisiwa mwaka 1955 na marehemu Sir Antony Fisher, ni shirika la kielimu, siyo shirika la kisiasa. Haifungamani na chama au kikundi chochote cha kisiasa na haifanyi shughuli iliyokusudiwa kuathiri uungwaji mkono kwa chama chochote cha siasa au mgombea kwenye uchaguzi wowote au kura ya maoni, au katika siasa kwa wakati mwingine wowote. Inajiendesha kwa gharama zinazopatikana kupitia mauzo ya machapisho, ada za kongamano na ufadhili wa hiyari.

Kwa kuongezea katika safu ya machapisho ya taasisi hii, pia huchapisha jarida mara nne kwa mwaka, liitwalo *Economic Affairs*.

Taasisi hii husaidiwa katika kazi zake na Baraza la Ushauri wa Kitaaluma [mashuhuri la kimataifa] na jopo adhimu la Washirika wa Heshima. Pamoja na wanataaluma wengine, hufanya mapitio ya machapisho ya taasisi ambayo yanayotazamiwa, maoni yao yakipitishwa kwa sauti moja kwa waandishi. Kwa hiyo maandishi yote ya taasisi hii hupitia mchakato kama huo unaotoa uhuru mkubwa wa kufanya marejeo kama unavyotumika na majarida mashuhuri ya kitaaluma.

Machapisho kutoka Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi (IEA) hutumiwa sana darasani na katika kozi zinazotolewa mashuleni na kwenye vyuo vikuu. Pia yanauzwa duniani kote na mara nyingi hutafsiriwa/au kuchapishwa tena upya.

Tangu mwaka 1974 taasisi hii imesaidia kuunda mtandao wa kimataifa wa taasisi kama hii zipatazo 100 kutoka zaidi ya nchi 70 duniani. Zote hizo ni taasisi huru lakini zinafuata dhima ya taasisi hii.

Mitazamo inayotolewa kwenye machapisho ya Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi ni ya waandishi, na siyo ya Taasisi (ambayo haina mtazamo wa kufanya biashara), Wadhamini, wajumbe wake wa Baraza la Ushauri wa Kitaaluma au watumishi wa ngazi za juu.

Wajumbe wa Baraza la Ushauri wa Kitaaluma wa taasisi, Washirika wa Heshima, Wadhamini na Watumishi wameorodheshwa kwenyeukurasa ufuatao.

---

Taasisi inatambua kwa shukrani msaada wa kifedha kwa ajili ya programu yake ya machapisho na kazi nyingine utokanao na ukarimu wa marehemu Profesa Ronald Coase.

## KUHUSU TAASISI YA LIBERTY SPARKS (LS)

Taasisi hii ni shirika la utafiti na elimu (Namba ya usajili namba. R2/000243), lenye wajibu wa udhamini. Dhima yake ni kuboresha na kukuza uelewa wa watu kwenye mifumo ya kiuchumi,kisiasa na jamii huru kwa kujikita zaidi kwenye sera za umilikiji mali binafsi,utawala wa sheria,masoko huria na haki za watu kama vichocheo vya maendeleo na mafanikio ya watu na jamii yote kwa ujumla.

Taasisi hii hufanikisha dhima yake kupitia:

- programu za tafsiri na uchapishaji wa kazi bora za waandishi wa hali ya juu
- Makongamano, semina, mihadhara na matukio mengine
- Ziara kwa wanafunzi wa shule na vyuo
- Kupitia na kuonekana katika vyombo vya habari
- Tafiti na ushawishi

Taasisi hii, ambayo iliasisiwa mwaka 2017 na Evans Exaud,ambaye ni mkurugenzi mtendaji mkuu wa shirika kwa sasa, ni shirika la kielimu, siyo shirika la kisiasa. Haifungamani na chama au kikundi chochote cha kisiasa na haifanyi shughuli iliyokusudiwa kuathiri uungwaji mkono kwa chama chochote cha siasa au mgombea kwenye uchaguzi wowote au kura ya maoni, au katika siasa kwa wakati mwingine wowote. Inajiendesha kwa gharama zinazopatikana kupitia mauzo ya machapisho, na ufadhili wa hiyari.

Kwa kuongezea katika safu ya machapisho na tafsiri taasisi hii, imetafsiri na kuchapisha kitabu cha Adam Smith Mtangulizi,Chimbuko la Ubepari,Safari za Jonathan Gullible na Utangulizi wa Ujasiriamali .kwa lugha ya kiswahili na Misingi ya yamii huru kwa lugha ya Chichewa inayotumika sehemu kubwa ya malawi,Zimbabwe na pande zingine za Africa ambazo zote ni kazi bora na safi za Eamonn Butler.

Taasisi hii imeendelea kujitanua na kupata washiriki kutoka sehemu mbalimbali za mipaka ya nchi kama Kenya,Uganda na Malawi huku ikipata washiriki wenye nia ya pamoja ya kujenga jamii huru na yenye mafanikio.

Taasisi ya Liberty Sparks
Sinza,Kijuweni
Simu: +255 736 164 141

P.O.Box: 66662
Baruapepe: info@libertysparks.org
Tovuti: www.libertysparks.org
Tanzania | Kenya |Uganda

Institute of Economic Affairs

Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi
2 Lord North Street, Westminster, London
SW1P 3LB Simu: 020 7799 8900
Faksi: 020 7799 2137
Baruapepe: iea@iea.org.uk
Tovuti: iea.org.uk

Mkurugenzi Mkuu & Mshirika wa Ralph Harris Mark Littlewood

Mkurugenzi wa Taaluma na Utafiti Profesa Syed Kamall

Wadhamini

Mwenyekiti: Neil Record
Kevin Bell
Profesa Christian Bjørnskov
Robert Boyd
Linda Edwards
Robin Edwards
Sir Michael Hintze
Profesa Patrick Minford
Bruno Prior
Profesa Martin Ricketts
Linda Whetstone

Baraza la Ushauri wa Kitaaluma

Mwenyekiti: Profesa Martin Ricketts
Graham Bannock
Dr Roger Bate
Profesa Alberto Benegas-Lynch, Jr
Profesa Christian Bjørnskov
Profesa Donald J Boudreaux
Profesa John Burton
Profesa Forrest Capie
Profesa Steven N S Cheung
Profesa Tim Congdon
Profesa Christopher Coyne
Profesa N F R Crafts
Profesa David de Meza
Profesa Kevin Dowd
Profesa David Greenaway
Dr Ingrid A Gregg
Dr Samuel Gregg
Walter E Grinder
Profesa Steve H Hanke
Profesa Keith Hartley
Profesa Peter M Jackson
Dr Jerry Jordan
Profesa Terence Kealey
Dr Lynne Kiesling
Profesa Daniel B Klein
Dr Mark Koyama
Profesa Chandran Kukathas
Dr Tim Leunig
Dr Andrew Lilico
Profesa Stephen C Littlechild
Profesa Theodore Roosevelt Malloch

Dr Eileen Marshall
Profesa Antonio Martino
Dr John Meadowcroft
Dr Anja Merz
Dr Lucy Minford
Profesa Julian Morris
Profesa Alan Morrison
Profesa D R Myddelton
Dr Marie Newhouse
Paul Ormerod
Profesa David Parker
Dr Neema Parvini
Profesa Victoria Curzon Price
Dr Alex Robson
Profesa Pascal Salin
Dr Razeen Sally
Profesa Pedro Schwartz
Profesa J R Shackleton
Jane S Shaw
Profesa W Stanley Siebert
Shanker Singham
Dr Carlo Stagnaro
Dr Elaine Sternberg
Profesa James Tooley
Dr Radomir Tylecote
Profesa Nicola Tynan
Profesa Roland Vaubel
Dr Cento Veljanovski
Profesa Lawrence H White
Profesa Walter E Williams
Profesa Geoffrey E Wood

Honorary Fellows

Profesa Michael Beenstock
Profesa Richard A Epstein
Profesa David Laidler
Profesa Deirdre McCloskey
Profesa Chiaki Nishiyama
Profesa Vernon L Smith

*Vitabu vingine vilivyochapishwa hivi karibuni na Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi vinajumuisha:*

*In Focus: The Case for Privatising the BBC*
Kimehaririwa na Philip Booth
Hobart Paperback 182; ISBN 978-0-255-36725-7; £12.50

*Islamic Foundations of a Free Society*
Kimehaririwa na Nouh El Harmouzi and Linda Whetstone
Hobart Paperback 183; ISBN 978-0-255-36728-8; £12.50

*The Economics of International Development: Foreign Aid versus Freedom*
*for the World's Poor*
William Easterly
Readings in Political Economy 6; ISBN 978-0-255-36731-8; £7.50

*Taxation, Government Spending and Economic Growth*
Kimehaririwa na Philip Booth
Hobart Paperback 184; ISBN 978-0-255-36734-9; £15.00

*Universal Healthcare without the NHS: Towards a Patient-Centred Health*
*System*
Kristian Niemietz
Hobart Paperback 185; ISBN 978-0-255-36737-0; £10.00

*Sea Change: How Markets and Property Rights Could Transform the Fishing*
*Industry*
Kimehaririwa na Richard Wellings
Readings in Political Economy 7; ISBN 978-0-255-36740-0; £10.00

*Working to Rule: The Damaging Economics of UK Employment Regulation*
J. R. Shackleton
Hobart Paperback 186; ISBN 978-0-255-36743-1; £15.00

*Education, War and Peace: The Surprising Success of Private Schools in*
*War-Torn Countries*
James Tooley and David Longfield
ISBN 978-0-255-36746-2; £10.00

*Killjoys: A Critique of Paternalism*
Christopher Snowdon
ISBN 978-0-255-36749-3; £12.50

*Financial Stability without Central Banks*
George Selgin, Kevin Dowd and Mathieu Bédard
ISBN 978-0-255-36752-3; £10.00

*Against the Grain: Insights from an Economic Contrarian*
Paul Ormerod
ISBN 978-0-255-36755-4; £15.00

*Ayn Rand: An Introduction*
Eamonn Butler
ISBN 978-0-255-36764-6; £12.50

*Capitalism: An Introduction*
Eamonn Butler
ISBN 978-0-255-36758-5; £12.50

*Opting Out: Conscience and Cooperation in a Pluralistic Society*
David S. Oderberg
ISBN 978-0-255-36761-5; £12.50

*Getting the Measure of Money: A Critical Assessment of UK Monetary Indicators*
Anthony J. Evans
ISBN 978-0-255-36767-7; £12.50

*Socialism: The Failed Idea That Never Dies*
Kristian Niemietz
ISBN 978-0-255-36770-7; £17.50

*Top Dogs and Fat Cats: The Debate on High Pay*
Kimehaririwa na J. R. Shackleton
ISBN 978-0-255-36773-8; £15.00

*School Choice around the World … And the Lessons We Can Learn*
Kimehaririwa na Pauline Dixon and Steve Humble
ISBN 978-0-255-36779-0; £15.00

*School of Thought: 101 Great Liberal Thinkers*
Eamonn Butler
ISBN 978-0-255-36776-9; £12.50

*Raising the Roof: How to Solve the United Kingdom's Housing Crisis*
Kimehaririwa na Jacob Rees-Mogg and Radomir Tylecote
ISBN 978-0-255-36782-0; £12.50

*How Many Light Bulbs Does It Take to Change the World?*
Matt Ridley and Stephen Davies

ISBN 978-0-255-36785-1; £10.00

*The Henry Fords of Healthcare: ...Lessons the West Can Learn from the East*
Nima Sanandaji
ISBN 978-0-255-36788-2; £10.00

*An Introduction to Entrepreneurship*
Eamonn Butler
ISBN 978-0-255-36794-3; £12.50

Machapisho mengine ya Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi (IEA)

Taarifa kamili juu ya machapisho mengine na wigo mpana wa kazi za Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi (IEA) zinaweza kupatikana kupitia www.iea.org.uk. Kuagiza chapisho lolote tafadhali angalia hapa chini.

Wateja binafsi

Kuagiza kama mteja binafsi peleka oda yako kupitia:

Clare Rusbridge
IEA
2 Lord North Street
FREEPOST LON10168
London SW1P 3YZ
Simu: 020 7799 8907. Fax: 020 7799 2137
Baruapepe: sales@iea.org.uk

Wafanyabiashara

Kuagiza kama mfanyabiashara peleka oda yako kupitia:
NBN International (IEA Orders)
Orders Dept.
NBN International
10 Thornbury Road
Plymouth PL6 7PP
Simu: 01752 202301, Fax: 01752 202333
Baruapepe: orders@nbninternational.com

Kulipia kwa mwaka

Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi pia hutoa huduma ya kulipia kwa machapisho yake yatakayotoka. Kwa malipo ya mara moja kwa mwaka, kwa sasa £42.00 ukiwa nchini Uingereza, utapokea kila makala itakayochapishwa na Taasisi. Kwa zaidi taarifa, wasiliana na:

Clare Rusbridge
Subscriptions
IEA

2 Lord North Street
FREEPOST LON10168
London SW1P 3YZ
Tel: 020 7799 8907, Fax: 020 7799 2137
Baruapepe: crusbridge@iea.org.uk